epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
0745 700710
LIKE & FOLLOW US
Jumanne Mei 14, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0581676
www.ippmedia.com
nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital

UKURASA WA 3
**Lori** laacha njia, laua watano walioshuka kwenye basi

UKURASA WA 4&5
RIPOTI YA UCHUNGUZI
**Kilichokwamisha** viwango Uwanja wa Mkapa, nchi haina wataalamu



UKURASA WA 8
**Samia** atua Ufaransa kuongoza mkutano wa nishati safi



UKURASA 22
**TEN HAG ALIA NA MAJERUHI MAN UNITED**

# Watiania CHADEMA walia usaili unatisha

• **Wadai** ni jopo lisilo na masihara; Sugu ajigamba ana uhakika...*Endelea ukurasa 2*



Baadhi ya wajumbe wa Kamati Kuu ya CHADEMA wakiwa katika kikao cha kusaili wagombea wa nafasi mbalimbali ndani ya chama hicho jijini Dar es Salaam jana. Kulia ni Naibu Katibu Mkuu, Benston Kigaila, Katibu Mkuu, John Mnyika, Makamu Mwenyekiti (Bara), Tundu Lissu na Makamu Mwenyekiti (Zanzibar), Said Mohamed. **PICHA: ELIZABETH ZAYA**



UKURASA WA 21
## WESLEY GASSOVA AWINDWA WEST HAM UNITED

BAADA ya kuthibitisha wataachana na kocha wao kutoka nchini Scotland, David Moyes, mwishoni mwa msimu huu 2023/24, imefahamika kuwa uongozi wa klabu ya West Ham...

## Mdhibiti bei tiba aja rasmi, tija kitita NHIF hii

UKURASA 2



## CAG: Wateule wako Rais wananiingilia kiutendaji

• **Alia** na nongwa, mawaziri na zabuni...*Ukurasa 18*

**MICHEZO** YANGA SC YATWAA UBINGWA WA 30 UK.24 **KATUNI** UK.6

# Watiania CHADEMA walia usaili unatisha

**Na Elizabeth Zaya**

WATIANIA ya kugombea nafasi za uongozi ndani ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) wamesema usaili wa chama hicho si wa masihara.

Baadhi wamedai kuulizwa maswali magumu, wakiyaita ya "uchokonozi", wakisisitiza maswali yalikuwa mengi zaidi kwa watiania ambao walishawahi kushika nafasi za uongozi ndani ya chama hicho.

Usaili wa watiania jana ulianza sita mchana. Hata hivyo, hadi saa 10 jioni ni Kanda moja tu ya Magharibi ambayo ilikuwa imefanyiwa usaili.

Mwandishi wa habari hizi alishuhudia wajumbe wakitoka ukumbini kwa ajili ya mapumziko ya chakula saa 10:15 jioni.

Baadhi ya wagombea ambao waliofanyiwa usaili walisema maswali wanayoulizwa ndani na wajumbe wa kikao hicho ni magumu.

"Ndugu yangu, huko ndani ni kwa moto, mambo yanayoulizwa ni mengi, wanakuchokonoa kila kitu na vile vichwa vilivyokaa kwenye usaili viko moto, vina madini mengi," alisema mmoja wa watiania.

Alidai kuwa miongoni mwa vitu alivyoulizwa ni namna alivyokitumikia chama, pia mipango na mikakati yake kukiletea ushindi katika uchaguzi zijazo.

"Pia kulikuwa na maswali ya uchokonozi kuhusu mienendo ya kitabia na kama niliwahi kutuhumiwa kwa makosa yoyote," alisema huku baadhi ya wagombea wakilazimika kutoka eneo la ofisi ya chama hicho kwenda kutembea, wakidai "kuvuta muda".

Akizungumzia muda uliotumika kuhoji watiania hao, Mkurugenzi wa Itifaki, Mawasiliano na Mambo ya Nje, John Mrema, alisema mahojiano kwa mtu aliyewahi kugombea au kuwa kiongozi na ambaye ni mpya hayafanani.

"Yule aliyewahi kugombea ni lazima awe na mambo mengi ya kuhojiwa, alikifanyia nini chama, alifanikiwa au alishindwa wapi na kama alishindwa ni kwanini na mengine mengi, ni tofauti na anayeanza," alisema Mrema.

Mtiania ya Uenyekiti Kanda ya Magharibi ambaye anatetea nafasi yake, Gaston Garubindi, alisema alitumia nusu saa kufanyiwa usaili.

"Mimi kwa sababu ni kiongozi, nimehojiwa vitu vingi na lazima watake kujua nimekifanyia nini chama na huko ninakotaka kwenda," alisema Garumbindi.

Alibainisha kuwa jumla ya viongozi na wajumbe walioshiriki katika usaili huo ni zaidi ya 30.

### SUGU ALONGA

Mtiania ya Uenyekiti Kanda ya Nyasa, Joseph Mbilinyi, maarufu Sugu, alipoulizwa kama ana uhakika kwa kuteuliwa na kamati kuu kugombea nafasi hiyo, alisema hana shaka na hilo.

"Nimejipima ndio maana nikaamua kugombea, kama ningeona kuna wingu nisingegombea, hivyo nimejiridhisha nimeamini kwamba nitapita usaili na nitapita kwenye uchaguzi," alisema Sugu.

Kwa mujibu wa taarifa kutoka ndani ya chama hicho, usaili unatarajiwa kukamilika leo.

Taarifa iliyotolewa na chama hicho kabla ya kuanza kwa kikao hicho, mada zilizokuwa zimepangwa kujadiliwa ni tatu, ikiwamo kupokea tathmini ya uchaguzi, kupokea tathmini ya maandamano ya awamu ya kwanza ya mikoa na kuweka mwelekeo wa awamu ya pili ya maandamano.

Nyingine ilikuwa kufanya usaili wa kuteua wagombea nafasi za uongozi katika Kanda Nne za Nyasa, Serengeti, Victoria na Magharibi.

Juzi kamati hiyo ilikamilisha usaili kwa watiania wa nafasi za mabaraza ya chama hicho peke yake.



Rais Samia Suluhu Hassan akiwa kwenye mazungumzo na Waziri anayeshughulikia Masuala ya Maendeleo ya Kimataifa wa Ufaransa, Chrysoula Zacharopoulou, walipokutana jijini Paris, Ufaransa jana. Rais Samia yupo Ufaransa kwa ajili ya kushiriki Mkutano wa Kimataifa wa Nishati Safi ya Kupikia kwa Afrika unaotarajiwa kufanyika leo, pia atakuwa Mwenyekiti Mwenza katika mkutano huo. **PICHA: IKULU**


## NOTISI YA KULIPA DENI NA TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Kampuni ya **WANGI AUCTION MART LIMITED,** kwa idhini waliopewa na **KARK FINANCIAL SERVICES** watauza kwa njia ya mnada wa hadhara magari kama dhamana ya mikopo.Ambapo wateja husika, wameshindwa kulipa mikopo kwa mujibu wa mikataba husika.Hivyo basi, ifahamike kuwa dhamana husika zitauzwa kwa njia ya mnada.Mnada utafanyika sehemu Gari lilipo siku na tarehe kama vilivyoainishwa kwenye jedwali hapa chini.Mnada ni kuanzia saa Tatu kamili asubuhi na kuendelea.(03:00 asubuhi)

| | JINA LA MDAIWA | | DHAMANA ILIYO WEKWA | NAMBA YA GARI | MAHALI DHAMANA ILIPO | KAMPUNI HUSIKA | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | RACHEL ELISHA ABEL | | BMW X3 | T 645 DNN | MWANZA | KARK FINANCIAL SERVICES | 28/05/2024 |
| 2 | CHINAKILA PASCHAL CHIFUNDA | | MITSUBISH CANTER | T 748 CHG | MWANZA | KARK FINANCIAL SERVICES | 21/05/2024 |
| 3 | JUSTINA SIMON KINSHIHI | | TOYOTA COROLLA SPACIO | T 562 EAX | MWANZA | KARK FINANCIAL SERVICES | 21/05/2024 |
| 4 | PAUL ALFRED KINSWAGA | | TOYOTA HILUX | T 628 CAU | MWANZA | KARK FINANCIAL SERVICES | 21/05/2024 |
| 5 | WINNIFRIDA YAPANDA ELIUS | | TOYOTA PASSO | T 673 DCA | MWANZA | KARK FINANCIAL SERVICES | 28/05/2024 |
| 6 | HUSNA ULEDI KAUGA | | TOYOTA RACTIS | T 215 DKG | MWANZA | KARK FINANCIAL SERVICES | 28/05/2024 |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Mnunuzi atalazimika kulipa malipo ya 25% ya fedha taslimu papohapo baada ya nyundo ya dalali kutua na salio la 75% liwe limelipwa ndani ya siku 14 tokea siku ya mnada.
2. Mnunuzi akishindwa kutimiza sharti mojawapo hapo juu, malipo ya awali hayatarejeshwa na mnada utarudiwa.
3. Mali/dhamana itauzwa katika hali ilivyo. Gharama za kubadili umiliki baada ya manunuzi zitakuwa juu ya mnunuzi. Kampuni itasaidia kuratibu tu.
4. Kwa maelezo zaidi, wasiliana nasi kwenye ofisi zetu au tupigie simu: **+255 67 475 5313.**


# Serikali kuanzisha chombo udhibiti bei huduma za afya

**Na Jenifer Gilla**

SERIKALI inakusudia kuanzisha chombo cha kitaifa cha udhibiti wa bei za huduma za afya katika ngazi zote nchini kama inavyofanyika kwenye gharama za maji, umeme na mafuta.

Lengo ni kudhibiti ukuaji holela wa gharama za afya kwa wananchi hususan wasio na bima ya afya. Akiwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hiyo kwa mwaka 2024/25 Waziri wa wizara hiyo, Ummy Mwalimu, aliomba Bunge kuidhinisha Sh. trilioni 1.311.

### KITITA CHA NHIF

Kitita kipya Daktari Bingwa katika ngazi ya rufani mkoa, ada imeongezeka kutoka Sh. 15,000 hadi Sh. 25,000 ambayo ni sawa na kumuona daktari aliyepo ngazi ya kanda na taifa.

Hatua hii inavutia madaktari bingwa kufanyakazi katika hospitali za rufani za mikoa hususan za pembezoni.

Ada ya usajili na kumuona daktari kwa wanufaika wa NHIF kwa ngazi ya wilaya imeongezeka kutoka Sh. 5,000 hadi Sh. 7,000, kwa ngazi ya kituo cha afya ada imeongezeka kutoka Sh. 2,000 hadi Sh. 7,000 na kwa ngazi ya zahanati ada imeongezeka kutoka Sh. 1,000 mpaka 3,000.

Pia itaongeza mapato katika vituo na motisha kwa watumishi wa zahanati, vituo vya afya na hospitali za wilaya na hivyo kuvutia madaktari kufanyakazi katika vituo hivyo.

Kwa mwaka wa fedha 2324 wizara imeidhinisha kitita kipya cha mafao cha Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya kwa mwaka 2023. Kitita hicho kimeoanisha orodha muhimu ya dawa (NEMLIT) pamoja na mwongozo wa tiba wa taifa (STG).

Kitata hicho kitaboresha upatikanaji wa huduma bora za kibingwa na ubingwa bobezi karibu na wanachama.

Aidha kitita hicho kimezingatia maendeleo ya teknolojia ya tiba, hali halisi ya bei katika soko na uwezo wa mfuko kugharamia huduma hizo huku ukiendelea kuwa endelevu kwa kuzingatia ushauri wa taifa, mapendekezo ya tathmini ya uhai na uendelevu wa kipindi kinachoishia Juni 30, 2021.

### VIPAUMBELE

Alitaja vipaumbele ni kuimarisha huduma za kinga dhidi ya magonjwa na kuimarisha upatikanaji na ubora wa huduma za afya zinazotolewa na vituo vya kutolea huduma za afya kuanzia ngazi ya zahanati hadi taifa.

Vingine ni kuimarisha mifumo ya ugharamiaji wa huduma za afya nchini, kuimarisha huduma za afya ya uzazi, mama na mtoto. Kipaumbele kingine ni kuimarisha huduma za matibabu ya ubingwa na ubingwa bobezi nchini, kuendeleza kusimamia afua za tiba asili na tiba mbadala na kuimarisha upatikanaji wa huduma za magonjwa ya kuambukiza, yasiyoambukiza na ya mlipuko.

Alisema katika bajeti hiyo, wizara imetenga Sh. bilioni 117.61 kuimarisha huduma ya kinga dhidi ya magonjwa ikiwamo kuimarisha utekelezaji wa afua za chanjo kwa kuwafikia watoto 3,117,564 wenye umri chini ya miaka miwili, wasichana 871,429 wenye umri wa miaka tisa (9) na wajawazito 3,298,437.

Pia wizara itatumia Sh. bilioni 219.01 kwa ajili ya kuimarisha upatikanaji na ubora wa huduma za afya zinazotolewa na vituo vya kutolea huduma za afya katika ngazi zote ikiwamo kuimarisha upatikanaji wa damu salama.

Wizara pia imetenga Sh. bilioni sita kwa ajili ya kuimarisha mifumo ya ugharamiaji wa huduma za afya nchini kwa kufanya mapitio ya mkakati wa upatikanaji wa rasilimali fedha kwa ajili ya kugharamia huduma za afya.

"Kuanza mchakato wa kuanzisha chombo cha kitaifa cha udhibiti wa bei za huduma za afya katika ngazi zote na kuimarisha uhai na ustahimilivu wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF)," alisema Waziri Ummy.

Kwa mujibu wa waziri huyo Sh. bilioni 17.18 zimetengwa kuimarisha huduma za afya ya uzazi, mama na mtoto, ikiwamo kujenga, kukarabati na ununuzi wa vifaa tiba vya wodi 100 maalum za watoto wachanga wagonjwa waliozaliwa na uzito pungufu.

# Kilio intaneti kusuasua chaingia siku ya pili

**Christina Mwakangale na Jennifer Gilla**

WATUMIAJI wa intaneti nchini na jirani za Afrika Mashariki, hasa wanaotegemea shughuli zao kufanyika mtandaoni, wamejikuta wakiingia siku ya pili pasi na huduma za uhakika kutokana na mawasiliano hayo kupatikana kwa kusuasua.

Waathirika wakubwa wa changamoto hiyo ni pamoja na vyumba vya habari ambamo habari huzalishwa, huku mbinu zilizotumika awali za analogia, zikirejewa kwa baadhi yao.

Mhandisi kutoka kampuni inayosambaza huduma ya intaneti nchini na nchi jirani ya Simbanet, aliyejitambulisha kwa jina moja la Justin, alisema tatizo hilo limetokea eneo la Mtunzini, kilomita takribani 45 kutoka mwambao wa bahari.

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), Jabir Bakari, kwenye taarifa yake jana, alisema mamlaka inaendelea kufuatilia taarifa za upatikanaji intaneti.

Wakizungumza na gazeti hili jana, baadhi ya wananchi ambao ni watumiaji huduma za intaneti, akiwamo Jane Mwasomola, mkazi wa Tunduma, mkoani Songwe, walisema kikundi chao cha kuweka na kukopa kinategemea mtandao wa kijamii wa WhatsApp kuchangisha fedha za siku kutoka kwa kila mwanachama.

Meneja wa Idara ya Mawasiliano na Teknolojia (IT) wa Kampuni ya The Guardian LTD, Allan Mshana, akifafanua kuhusu intaneti, alisema; "kilichoathiri mfumo wa mawasiliano si huduma ya intaneti inayosafirishwa moja kwa moja, bali hata 'back up' (iliyohifadhiwa kwa matumizi).

"Nyaya za kusambazia huduma ya intaneti huwa zipo zinazosafirisha huduma 'live', yaani moja kwa moja, na ipo sehemu inayohifadhi 'back up' kwamba ikitokea dharura, ichukue nafasi, lakini kilichotokea pande zote zimeathirika, kidogo wanaotumia satelaiti wanafanikiwa," alisema Mshana.

# Lori laacha njia na kugonga watu sita, watano wafariki

**Na Godfrey Mushi,** MWANGA

WATU watano wamepoteza maisha baada ya lori aina ya Mitsubishi Fusso kuwagonga watembea kwa miguu sita katika eneo la Lembeni, Wilaya ya Mwanga, mkoani Kilimanjaro.

Lori hilo lenye namba za usajili T 736 AXN lilikuwa linatokea Lushoto, Tanga kwenda Tarakea, Wilaya ya Rombo, Kilimanjaro.

Kamanda wa Polisi mkoani Kilimanjaro, Kamishna Mwandamizi Msaidizi (SACP) Simon Maigwa, alisema lori hilo liliacha njia na kugonga watembea kwa miguu hao ambao walikuwa abiria wa basi dogo, Toyota Coaster lenye namba T 122 DGM.

Kwa mujibu wa SACP Maigwa, basi hilo lilikuwa limeharibika kando ya barabara kuu ya Same/Mwanga.

Alisema ajali hiyo ilitokea Mei 12 mwaka huu saa saba usiku.

"Hao abiria walikuwa nje ya gari (coaster) wakitembeatembea wakisubiri matengenezo ya gari hilo yakamilike. Ghafla waligongwa na Fusso na watano walifariki dunia papo hapo na mmoja kujeruhiwa vibaya," alisema.

Waliofariki dunia katika ajali hiyo wametambuliwa kuwa ni Cosmas Severine (27), Mkazi wa Mbezi, Dar es Salaam na Jackline Mushi (30), Mkazi wa Karanga, Moshi.

Wengine ni Dorothea Massawe (36), Mkazi wa Mbezi, Dar es Salaam, Hiza Hamisi (27), Mkazi wa Mwanga na Lucasia Otaru (49), Mkazi wa Moshi, wote Mkoa wa Kilimanjaro.

Alisema majeruhi wa ajali hiyo ni Christian Kiwango (32), mkazi wa Rombo, Kilimanjaro, ambaye alivunjika mguu wa kushoto na amelazwa katika Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Kaskazini ya KCMC.

Chanzo cha ajali hiyo kimetajwa na Kamanda Maigwa kuwa ni mwendokasi na uzembe wa dereva wa Fusso kushindwa kuchukua tahadhari kwenye mteremko mkali na kona kali na hivyo kusababisha ajali hiyo.

Alisema kwa sasa wanamshikilia dereva huyo, aliyemtaja ni Yahaya Mohamed (28).


**Jinsi Ya Kununua Magazeti Ya Nipashe na The Guardian katika tovuti ya www.ippmedia.com au epaper.ippmedia.com**

**Kupitia tovuti ya epaper.ippmedia.com:**

1. Utafungua tovuti ya epaper.ippmedia.com utachagua toleo unalotaka kununua aidha Nipashe au The Guardian kwa kuclick Read
2. Itakuletea ukurasa mwingine unaotakiwa kujaza taarifa zako na kifurushi unachotaka kujiunga. Kisha unabonyeza "subscribe"
3. Itakupeleka katika ukurasa wa malipo ambapo unaweza kulipa kwa kadi ya benki malipo kwa mtandao wa simu unaoutumia baada ya kujaza kwa usahihi taarifa zako na anuani
4. Kwa namba ya simu unachagua mtandao wa simu unatumia ambapo utaandika namba yako na kutick box la kukubali terms and conditions ndio uende "pay via mobile". Itakuletea maelekezo namna ya kulipa kwa simu kulingana na mtandao unaotumia.
5. Kwa benki unaweka taarifa za kadi yako ndio uruhusu muamala ukatwe katika account yako baada ya kukubali terms and conditions. Ndipo utaingia katika account yako na kusoma toleo ulilolilipia
6. Malipo yakikamilika, utapokea email na message kuwa pesa imepokelewa hivyo utaingia kwa account yako na kuanza kusoma yale matoleo umeyalipia

**Na kwa tovuti ya www.ippmedia.com**

7. Unafungua website yako ya www.ippmedia.com upande wa kulia utaona "E-Paper" utabonyea na kuafuatisha hatua zote 1-6





For more Information Contact 0677 020 701 | Subscription: 0625 174 714 | Email: customerrelations@guardian.co.tz

Nipashe The Guardian

# Siri iliyojificha maboresho ya Uw

Na Sanula Athanas



UWANJA wa Benjamin Mkapa, jijini Dar es Salaam unafanyiwa maboresho lakini tafsiri ya kitaalamu ya kufikiwa hatua hiyo imebeba mjadala wenye sura tofauti.

Kampuni iliyoujenga imesema haikuandaa mchoro wa uwanja huo ambao Shirikisho la Soka Afrika (CAF) limesema haukidhi viwango vya kimataifa.

Beijing Construction Engineering Group (BCEG) ilijenga uwanja huo kuanzia mwaka 2004 hadi 2007 ulipoanza kutumika. Sasa kampuni hiyohiyo imepewa zabuni na serikali kuuboresha kwa gharama ya Sh. bilioni 31.

Meneja Mradi wa kampuni hiyo, Li Liang, katika ufafanuzi wake kwa mwandishi wa habari hizi, anasema walijenga uwanja huo kwa hadhi ya Daraja "B" badala ya Daraja "A" ambalo sasa CAF wanahitaji.

Kwa hadhi uliyonayo sasa, CAF imesema uwanja hauna sifa kutumika kwenye mashindano inayoandaa. Imeelekeza uboreshwe kufikia viwango vinavyohitajika ili utumike kwa mechi zake, ikiwamo michuano ya Mataifa ya Afrika (AFCON) mwaka 2027 ambayo Tanzania itakuwa mwenyeji, ikishirikiana na majirani Kenya na Uganda.

Inspekta Hashim Abdallah, Ofisa Usalama wa Shirikisho la Soka Ulimwenguni (FIFA) nchini, anasema CAF imetoa maelekezo hayo baada ya wataalamu wake kukagua uwanja huo na kubaini haujafikia viwango vinavyohitajika.

"CAF na FIFA wanapokuwa na mechi za mashindano wanayoandaa, wanatoa masharti viwanja viwe na hadhi waliyothibitisha.

"Mfano, mechi za FIFA kuwania kufuzu kushiriki Kombe la Dunia na zile za AFCON, wanatoa maelekezo viwanja vipi vitumike na wenyewe wanaleta timu ya kukagua; ndiyo maana hata sasa, kama umefuatilia, walishakuja kwenye maandalizi ya AFCON 2027," anasema.

Sasa nani abebe lawama? Ni serikali iliyoahidi mwaka 2000 kwamba itajenga uwanja wa kimataifa nchini, watendaji wa serikali waliosimamia mradi, BCEG waliojenga uwanja au aliyeandaa mchoro wa uwanja?

Meneja Mradi wa BCEG, Liang, anasema mchoro wa uwanja huo haukuandaliwa na kampuni yao. Uliandaliwa na taasisi inayoitwa BIAD (Beijing Institute of Architectural Design) anayosema inamilikiwa na Serikali ya China.

"Mchoro wa uwanja huu uliandaliwa na nchi yetu (China). Utaratibu wa nchi yetu katika hii miradi inayoifadhili ni kwamba, sisi (kampuni) tunapewa mradi kwenda kutekeleza; lakini anayeandaa mchoro ni serikali yetu.

"Serikali yetu ina kampuni yake ya uandaaji michoro ya miradi, inaitwa BIAD. Hii ndio iliyoandaa mchoro wa uwanja huu mwaka 2004. Sisi tuliomba kazi, tukajenga kulingana na mchoro wa mradi. Kumbuka nchi yetu (China) ilifadhili ujenzi wa uwanja huu," alisema.

Tarehe 24 Juni 2006, gazeti Daily News - linalomilikiwa na Serikali ya Tanzania, liliripoti kuwa Tanzania ilichangia Sh. bilioni 25 kufanikisha mradi wa ujenzi wa Uwanja wa Taifa (sasa Uwanja wa Benjamin Mkapa) ambao bajeti yake kuu ilikuwa Dola za Marekani milioni 56 (Sh. bilioni 64 wakati huo).

Vilevile, Shirika la Utangazaji la Uingereza (BBC) Juni 6, 2004 liliripoti kuhusu mchakato wa ujenzi huo, likieleza kuwa katika kutekeleza ahadi ya Rais Benjamin Mkapa ya mwaka 2000, ya kujenga uwanja wa kisasa, zabuni ya kujenga uwanja ilitangazwa na serikali mwaka 2003.

BBC ilimnukuu Prof. Juma Kapuya, aliyekuwa Waziri wa Michezo kipindi hicho, akisema kuwa serikali ilitenga bajeti ya Dola milioni 60 kufanikisha mradi huo na kampuni 11 zilijitokeza kuomba zabuni hiyo.

Hatimaye mwaka 2004, Kampuni ya Vinci Construction ya Ufaransa ndiyo iliyofanikiwa kupatiwa zabuni ya ujenzi kwa Dola milioni 154 sawa na Sh. bilioni 397.032 kwa sasa.

Hata hivyo, kukawa na msukumo wa baadhi ya mataifa ya mrengo wa Magharibi yanayosimamia mwenendo wa uchumi wa dunia (Bretton Woods Institutions). Hayakukubaliana na mradi huo, hata Serikali ya Tanzania kulazimika kusitisha zabuni hiyo.

Profesa Deborah Brautigam katika kitabu chake cha 'The Dragon's Gift: The Real Story of China in Africa', anasema, "hoja ilikuwa kwamba nchi maskini iliyotoka kusamehewa madeni makubwa, inapata wapi utashi wa kutekeleza mradi wa gharama kubwa kama huo?"

Baada ya zabuni hiyo kusitishwa, Serikali ya Tanzania ikahamishia China mchakato wa mradi huo. Huko ndiko hata mchoro wa uwanja uliandaliwa. Mchakato uliporejeshwa Dar es Salaam, ilikuwa ni utekelezaji.

Aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Nje, Jakaya Kikwete, Juni 2004 alisafiri kwenda China alikotia saini mkataba wa makubaliano na serikali ya nchi hiyo kujenga uwanja kwa Dola milioni 56, China ikifadhili Dola milioni 20 kugharamia mradi huo.

Hata hivyo, miaka 17 tangu 2007 ulipoanza kutumika, ukaguzi wa CAF nchini unabaini uwanja huo una kiwango cha chini kulinganishwa na malengo ya matumizi hivi sasa, kwa maana uko katika Daraja la Pili, ilhali mahitaji ni ya Daraja la Kwanza.

Katika utekelezaji maelekezo yatokanayo na ripoti ya ukaguzi wa CAF, serikali imechukua hatua; sasa inafanya maboresho kwa kuziba mapengo na kuweka matakwa yote yanayofanya uwanja kuwa na kiwango cha hadhi iliyokusudiwa.

Tanzania imethibitishwa na CAF kuwa mwenyeji wa AFCON 2027 na michuano ya Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN) mwaka huu.

Mwandishi wa habari hizi, Mei 2 mwaka huu, alihitaji ufafanuzi kutoka kwa Ofisa Mnunuzi Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA), Alice Mcharo juu ya:

Kwanza, sababu za kutunuku zabuni kwa kampuni iliyokuwa na kiwango kikubwa kuliko bajeti iliyopangwa na serikali.

Pili, kwanini kampuni iliyoshinda zabuni, Vinci Construction haikujenga Uwanja wa Taifa (sasa Uwanja wa Benjamin Mkapa) badala yake ukajengwa na BCEG?

Tatu, sababu za kutunuku zabuni ya Sh. bilioni 31 kwa BCEG kuboresha uwanja ilhali wataalamu wa CAF wamethibitisha uwanja uliojengwa na kampuni hiyo haujafikia viwango vya kimataifa; na

Nne, hatua zilizochukuliwa au zinazochukuliwa dhidi ya watendaji wa serikali waliosababisha dosari ambazo CAF wamebaini katika mradi huo.

Hata hivyo, Ofisa Mnunuzi Mkuu Alice aliomba mwandishi awasilishe barua kwenye ofisi zao ikiwa na maswali hayo ili majibu yatolewe na Mkurugenzi Mkuu wa PPRA. Mwandishi aliwasilisha barua PPRA siku iliyofuata, yaani Mei 3, mwaka huu. Hata hivyo, hadi tunaingia mtamboni jana, barua hiyo ilikuwa haijajibiwa.

Katika ufafanuzi wake, Meneja Mradi wa BCEG, Liang, anasema, "lengo la ukarabati unaoendelea sasa ni kufikia viwango vya FIFA ili mechi za mashindano ya kimataifa zichezwe kwenye uwanja huo.

"Uwanja huu ni wa Daraja "B", una cheti cha FIFA cha Daraja "B", unafaa kwa matumizi ya ndani. Linapokuja suala la mashindano ya kimataifa, hauna sifa," Liang anasema.

Meneja huyo anaeleza, "CAF walikuja hapa mwaka jana, wakaukagua na kubaini hauna sifa wanazohitaji, ndiyo maana sasa tunafanya maboresho ili kufikia viwango vya FIFA vya uwanja wa Daraja "A", ikizingatiwa Tanzania inajiandaa kuwa mwenyeji wa mashindano ya AFCON 2027."

Mwandishi wa habari hizi alipohitaji kujua kama kuna kipengele katika mkataba wa ujenzi wa uwanja huo kinachoweka masharti ya BCEG kupewa zabuni uwanja unapohitaji ukarabati au maboresho, Meneja Liang alisema:

"Hapana! Hatuna kipengele hicho. Tumepata zabuni hii kwa kuomba baada ya kuwa imetangazwa na Serikali ya Tanzania. Tumefuata taratibu za kupata zabuni. Sidhani kama kigezo cha kwamba sisi ni wajenzi wa uwanja huu kimetumika kutupatia zabuni. Hii ni kazi mpya."

Mwandishi pia alihitaji kujua mchanganuo wa matumizi ya Sh. bilioni 31 zinazotolewa na serikali kuboresha uwanja; naye Meneja Liang alifafanua kwamba vifaa vinavyohitajika vimechangia gharama za maboresho hayo kuwa kubwa.

"Kumbuka tunatakiwa tulete viti vipya 62,000 (uwanja una viti 57,558 kwa ajili ya watazamaji. Viti vingine ni kwa ajili ya akiba). Thamani ya fedha mwaka 2004 ni tofauti sana na ya mwaka huu. Bei za vifaa sokoni ziko juu," anasema.


Meneja Liang anaeleza pia kuwa Serikali ya Tanzania inajenga uwanja mwingine mkoani Arusha wenye uwezo wa kuketisha watazamaji 30,000 ambao ni nusu ya Uwanja wa Benjamin Mkapa, lakini gharama za ujenzi wa uwanja huo wa Arusha ni Dola milioni 112 (Sh. bilioni 286).

## RIPOTI YA UCHUNGUZI

# anja wa Benjamin Mkapa




Mwonekano wa ndani wa Uwanja wa Benjamin Mkapa ambao unafanyiwa maboresho. **PICHA ZOTE: SANULA ATHANAS**



"Ili kufanya uwanja uwe wa Daraja "A" la FIFA, tunaweka taa za kisasa 352. Kwa sasa (Uwanja wa Benjamin Mkapa) ni wa Daraja "B", una taa 260. Kwahiyo, tunaondoa taa zote hizi na kuweka mpya 352 ambazo gharama zake ni kubwa," anasema.

Meneja huyo anafafanua kuwa taa mpya 352 zinazowekwa ni za mfumo wa kisasa ambazo zitawashwa na kuzimwa kidigiti, zikichukua sekunde chache kuwaka kulinganisha na taa 260 zilizopo ambazo zikizimika, hutumia dakika 15 hadi 20 kuwaka upya.

Kuhusu uzingatiaji masharti ya kutumia bidhaa na huduma za ndani (local content) katika utekelezaji miradi, Meneja Liang anasema, "vifaa vinavyopatikana Tanzania kama vile saruji, rangi tunanunua hapa. Tunaagiza nje vifaa ambavyo havipatikani nchini.

"Kati ya wafanyakazi wetu 164 wanaoshiriki ukarabati wa uwanja, 150 ni raia wa Tanzania, 14 tu ndiyo raia wa China.

"Tumeshauri pia mmiliki wa uwanja huu ambaye ni Serikali ya Tanzania, kubadili paa la uwanja. Eneo hili liko karibu na bahari. Maji ya hapa ni ya chumvi.

"Kwa kawaida paa la uwanja linapaswa kubadilishwa baada ya miaka 15, lakini kuwe na ukarabati walau kila mwaka. Hili la uwanja huu (wa Benjamin Mkapa) halijawahi kubadilishwa) tangu uwanja ujengwe (miaka 17 iliyopita).

"Tumeshauri kuongezwe bajeti ili kazi hiyo iwe sehemu ya kazi inayoendelea badala ya kuja kutangaza zabuni nyingine."

Hata hivyo, Meneja Liang anasita kuweka wazi kiasi kinachohitajika kwa ajili ya kubadili paa la uwanja, akieleza kuwa taratibu za zabuni zinamnyima rukhsa kutaja kiwango walichopendekeza kwa serikali.

Msajili wa Bodi ya Usajili wa Makandarasi (CRB), Rhoben Nkori, anaitaja BCEG kuwa moja ya kampuni kubwa za kimataifa zinazotekeleza miradi mikubwa. Ilisajiliwa nchini miaka 20 iliyopita.

Nkori anasema hawajapata malalamiko rasmi dhidi ya kampuni hiyo katika utekelezaji mradi wa ujenzi wa Uwanja wa Benjamin Mkapa.

"Kwa mkandarasi yeyote anayethibitika kufanya makosa, hatua tunazochukua ni pamoja na kufuta usajili wake, kusimamisha mradi anaotekeleza ili apewe mkandarasi mwingine; au kumtaka mkandarasi arudie ujenzi kwa gharama zake," anasema.

Nkori anayethibitisha kuwa na taarifa za kinachoendelea, yakiwamo maelekezo ya CAF, anasema BCEG ilijenga uwanja huo kulingana na mahitaji ya mteja na maelekezo ya kitaalamu wakati huo.

"Huo uwanja kama ilivyoelezwa na wajenzi ni Daraja "B" la FIFA, lakini CAF wanahitaji uwanja wa Daraja "A" kwa ajili ya mashindano yao," anasema.

Msajili Nkori anafafanua, akiwa na maelezo ya kitaalamu kuwa kihandisi kunakuwa na njia mbili za mbadala ambazo ni ama kufanya maboresho kama yanayoendelea sasa au ujenzi wa uwanja/jengo lingine.

Msajili Msaidizi - Fedha na Utawala katika Bodi ya Usajili wa Wahandisi (ERB), Paul Bilabaye, anaungana na Nkori kuwa ofisini kwao pia hawana malalamiko yoyote yaliyofikishwa mezani dhidi ya BCEG.

Hata hivyo, Bilabaye ana ufafanuzi wa kitaalamu kwamba, dosari zilizobainika kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa zimetokana na changamoto ya nchi kutokuwa na wataalamu wa viwanja.

Anasema ERB, wakati inafuatilia ukaguzi wa wataalamu wa CAF, imebaini nchi haina wataalamu wa eneo hilo.

Bilabaye anaeleza kuwa wataalamu wa ndani waliosimamia ujenzi wa uwanja hawakuwa na stadi za kutafsiri vilivyo mahitaji ya moja kwa moja katika ujenzi wa viwanja vya kimataifa.

Anasema kwamba katika ujenzi wa uwanja huo, masharti ya FIFA hayakuzingatiwa, akiwa na maelezo kuwa; "...mimi ni familia ya soka. Nilisimama katikati kupata mzabuni wa kujenga vituo vya michezo vya TFF (Shirikisho la Soka Tanzania) vya Tanga na Kigamboni. Kwenye ujenzi wa vituo hivyo tulikuwa tunaongozwa na viwango vya FIFA.

"Kwahiyo, hata ukienda kwenye vile viwanja vya Kigamboni na Tanga leo hii, hata wakija FIFA watakuta viwango vyao, kwa sababu wao ndio walitupa viwango na walikuwa wanasimamia hivyo."

Bilabaye anaeleza zaidi kwamba, "wakati wa kujenga ule Uwanja wa Mkapa masharti ya FIFA hayakuzingatiwa. Sasa leo unapotaka kuandaa mashindano ya CAF na FIFA yafanyike pale, wanakuletea viwango vyao, unabaini uwanja hauna sifa.

"FIFA wana viwango vyao. Niliangalia wataalamu wa CAF walivyopima udongo wa kiwanja. Yaani waliangalia mchezaji akikanyaga ule udongo, anapata madhara gani? Sisi hatuna wataalamu wa aina hiyo. Hii ndiyo maana jukumu la kuboresha kiwanja cha soka kwenye Uwanja wa Mkapa limebaki mikononi mwao," anasema.

Naye Katibu Mkuu Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Gerson Msigwa, Msemaji Mkuu wa Serikali wa zamani, anasema hakubaliani na dhana "uwanja haukidhi viwango vya FIFA".

Anaeleza kuwa maboresho yanayoendelea hivi sasa kwenye uwanja huo ni "kuondoa vitu vilivyoisha muda wa matumizi yake na kuweka vingine."

Kauli ya Msigwa si tu inakinzana na alichokisema Ofisa Usalama wa FIFA nchini, Inspekta Abdallah aliyekuwa sehemu ya timu ya ukaguzi ya CAF, bali pia inakinzana na kauli ya aliyekuwa Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Balozi Dk. Pindi Chana aliyesema Julai 27 mwaka jana kuwa lengo lao ni kufikia viwango vya FIFA.

Kwa mujibu wa Meneja Mradi wa BCEG, Liang, pamoja na mambo mengine, maboresho uwanjani yanagusa vyumba vya wachezaji kubadilishia nguo, chumba cha mikutano ya waandishi wa habari, eneo la watu mashuhuri (VVIP), kubadili viti vyote vya watazamaji na kibao cha kuonesha matokeo ya mechi, kuweka mfumo mpya wa Tehama, kufumua eneo la kiwanja cha kuchezea kandanda na seti mbili za magoli.

Vilevile, wanabadili viti vya benchi la ufundi na wachezaji wa akiba; taa, mifumo ya umeme, sauti, viyoyozi, majitaka na eneo la riadha pamoja na kuweka lifti mbili mpya, migahawa na kuondoa vitu vingine ambavyo vimepitwa muda wa matumizi. Hivi vilipaswa kutumika kwa miaka saba tu, lakini vimetumika kwa miaka 17.

"Tukumbuke uwanja huu ulianza kutumika mwaka 2007. Vifaa vingi humu vimeshafikia muda wa mwisho wa matumizi; lazima vibadilishwe," Meneja Liang anasema.

Kwa mujibu wa Meneja wa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Mlinde Mahona, maboresho ya uwanja huo yanatarajiwa kukamilika Agosti mwaka huu.

Sasa shughuli za ukarabati zinaendelea katika maeneo mbalimbali ya uwanja. Maeneo mengi yanaboreshwa, lakini pia jengo lenyewe kwa sababu limeshachafuka. Linasafishwa na kurudishwa katika ubora wake.

Mageti yalikuwa yamepata kutu kwa sababu mengi ni ya chuma, sasa yameboreshwa; yamepakwa kemikali za kuzuia kutu kisha wanapaka rangi.

Kuna maboresho kwenye maeneo mengi; mifumo ya sauti inabadilisbwa, mifumo ya umeme inabadilishwa kwa kuwa imekuwa changamoto tangu kipindi cha nyuma. Mifumo ya majitaka - baadhi ya matangi ya maji yalikuwa yameoza, hivyo kutohifadhi maji na kupeleka kwenye mifumo, sasa yanabadilishwa.

Mifumo ya usalama kama kamera za CCTV kwa maana mfumo wa miaka 17 iliyopita unafanyiwa maboresho. Kuna mfumo wa utoaji taarifa za matangazo ya michezo umeshaisha muda wake wa matumizi.

Kuna vitu vingi vinaboreshwa. Kwa ufupi, ninaweza kutaja hivyo kwa leo, lakini tayari maeneo mengi yameshafumuliwa kwa ajili ya kufanyiwa maboresho," Meneja Mahona anasema.

***FUATILIA KESHO MAELEKEZO YA CAF JUU YA HUDUMA ZA CHAKULA NA VINYWAJI UWANJANI**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Nishati safi kupikia ikomboe wananchi na hewa chafu

**MATUMIZI** ya jikoni kwa asilimia kubwa kwa kinamama wa vijijini ni nishati ya kuni na mkaa ambayo huchangia kwa kiasi kikubwa uharibifu wa hali ya hewa.

Moshi wanaovuta kutoka kwenye kuni na mkaa husababisha athari kubwa kwa magonjwa yanayosababishwa na hewa chafu.

Hivyo ulinzi wa afya ya mama, familia, mazingira na taifa dhidi ya mabadiliko ya tabianchi ni lazima uanzie jikoni.

Rais Samia Suluhu Hassan, amekuwa kinara wa kutangaza matumizi ya nishati safi ya kupikia na leo anatarajiwa kuliongoza taifa kufahamu kuwa ili raia wawe na afya na mazingira bora, lazima taifa lianze sasa kubadilisha nishati inayotumiwa kupikia.

Mara kwa mara anapokuwa kwenye majukwaa mbalimbali ya matumizi ya nishati safi ya kupikia, Rais anasema huwezi kumaliza au kupunguza ukataji miti unaoangamiza misitu ili kupata kuni na mkaa kama hutaligusa jiko.

Kampeni ya Rais imefanya mengi, Watanzania wameelezwa umuhimu wa matumizi ya teknolojia za kupikia zinazopunguza madhara kiafya, athari kwa mazingira na kijamii.

Na sasa Rais amelifikisha taifa kwenye kutekeleza Mkakati wa Nishati Safi ya Kupikia 2024 - 2034, aliouzindua wiki iliyopita jijini Dar es Salaam.

Analenga kaya zenye 'jiko safi na salama', ambayo asilimia 80 ya Watanzania watakuwa wanatumia jiko lenye nishati safi ya kupikia ifikapo 2034.

Pamoja na kuwaondoa kinamama katika matumizi ya kuni na mkaa na kutumia nishati safi, pia taasisi kubwa ambazo zinahudumia watu wengi kupata chakula, zinahimizwa kuhama kwenye matumizi ya kuni na mkaa na kuhamia kwenye nishati safi ili kupunguza uharibifu wa hewa na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Hata hivyo, ili kufanikiwa katika matumizi ya nishati safi ipo haja ya kuwa uhamasishaji wa kutumia majiko yanayotumia nishati safi na yapatikane kwa urahisi ili wanayoyahitaji wasipate vikwazo kwa kuyapata.

Ofisi ya Takwimu ya Taifa (NBS) inaeleza kuwa Tanzania Bara ina takribani kaya milioni 13.9.

Kufikia azma hiyo kaya zenye 'jiko safi na wakuu wa mikoa na wilaya wasimamie matumizi ya nishati safi ya kupikia na pia wizara na taasisi za umma kadhalika na sekta binafsi kuzingatia matumizi ya nishati safi ya kupikia ili kulinda mazingira na kuepusha athari nyingi zinazotokana na kutumia nishati zisizo safi.

Mwaka jana Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira iliagiza taasisi zote zinazohudumia watu zaidi ya 100, ifikapo Januari, mwaka huu, ziache kutumia kuni na mkaa kupikia.


Ofisi ya Makamu wa Rais, katika mikakati yake inaeleza kuwa hilo limefanyika na taasisi nyingi zikiwamo za umma kuanzia Magereza, kambi za jeshi, shule za sekondari, vyuo vya ualimu na vikuu vimeanza kutumia nishati safi ya kupikia.

Pia, juhudi zinafanywa na kila taasisi inayohusika na nishati na katika mbio za Mwenge wa Uhuru, mwaka huu, ujumbe mkubwa unaobebwa ni uhamasishaji wa matumizi ya nishati safi kupikia.

Uhamasishaji huo utasaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza matumizi ya kuni na mkaa na kuepusha athari zinazosababishwa na hewa chafu inayotokana na kuvuta moshi mchafu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita. 0713 578284,
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Sabato Kasika

## Muungwana Lazima Nilonge

# Adhabu ya viboko ifanyiwe kazi zaidi

**MACHI** mwaka huu, liliripotiwa tukio la mwanafunzi mwenye miaka sita wa darasa la kwanza kufariki dunia, kutokana na kile kilichodaiwa kuwa ni kuchapwa viboko na walimu.

Miaka ya hivi karibuni, matukio ya aina hiyo kwa wanafunzi, yalikuwa yameanza kupungua, kutokana na kupingwa na wadau mbalimbali wakiwamo watetezi wa haki za binadamu.

Wadau hao wanatamani takwa la kisheria linaloelekeza wakuu wa shule za sekondari na msingi, kuandika taarifa za kuruhusu kutolewa adhabu ya viboko kwa wanafunzi lizingatiwe.

Hata hivyo, inaonekana katika baadhi ya shule, hilo halifuatwi, kwani kuwapo taarifa za kifo cha mwanafunzi kinachohusishwa na viboko ni wazi kuna walakini.

Hivyo, ingekuwa ni vyema iwapo takwa la kisheria ambalo wadau hao lingezingatiwa ili kuepusha madhara yanayosababisha na adhabu za vikobo zisizofuata utaratibu ambao umeelekezwa.

Mdau mmoja anaeleza kuwa Sheria ya Elimu, Sura ya 353, marejeo ya mwaka 2002, inampa mamlaka Waziri wa Elimu kutunga kanuni za masuala mbalimbali zitakazokidhi utekelezaji wa mambo ya sheria hiyo.

Katika ufafanuzi wake, ni kwamba kanuni hizo zinatoa muongozo ni wakati gani adhabu ya viboko inatakiwa kutolewa na kwa kiwango gani na ni nani anapaswa kutekeleza adhabu hiyo.

Vilevile, anasema, kanuni ya 3(1), inafafanua jinsi ambavyo adhabu ya viboko itatolewa iwapo patatokea utovu mkubwa wa nidhamu, au kosa kubwa litakalofanywa ndani au nje ya shule.

Kosa hilo ni lile ambalo litaishushia shule heshima, kama kanuni ndogo ya (2) inasema adhabu ya viboko itolewe kwa kuzingatia umri, jinsi na afya ya mwanafunzi, na isizidi viboko vinne kwa tukio lolote.

Aidha, Waraka wa Elimu No 24 unaeleza wazi kuwa adhabu ya viboko na mwenye mamlaka ya kumuadhibu mwanafunzi ni mwalimu mkuu wa shule husika au mwalimu mwingine atakayeteuliwa na mwalimu mkuu kwa maandishi kila mara kosa linalostahili adhabu hii linapotendeka.

> **Matukio ya aina hiyo, yamekuwa yakihusishwa na adhabu za viboko zinazotolewa na baadhi ya walimu, kitendo ambacho ni kwamba waraka huo unawekwa pembeni na wahusika.**

Lakini, pia waraka unaweka wazi kuwa kila mara adhabu ya viboko inapotolewa sharti iorodheshwe katika kitabu kilichotengwa kwa kusudi hilo na kujaza taarifa zihusuzo adhabu husika.

Hatua hiyo inakwenda sambamba na kumwandika mwanafunzi aliyepewa adhabu, kosa lake, idadi ya viboko na jina la mwalimu aliyemuadhibu. Kwa kuwa waraka unamtambua mwalimu mkuu kuwa ndiye mwenye mamlaka ya kutoa adhabu hiyo.

Pamoja na hayo, waraka pia unaonya kuwa mwanafunzi wa kike anapaswa kupewa adhabu ya viboko na mwalimu wa kike isipokuwa kama shule haina mwalimu wa kike.

Kwa maelekezo hayo, ninadhani kama yangezingatiwa, kusingekuwa na matukio ya wanafunzi, kuvunjwa mikono, kuachwa na makovu mwilini na athari hasi za kiwango kikubwa zaidi hasa vifo.

Matukio ya aina hiyo, yamekuwa yakihusishwa na adhabu za viboko zinazotolewa na baadhi ya walimu, kitendo ambacho ni kwamba waraka huo unawekwa pembeni na wahusika.

Hivyo, si vibaya kuendelea kuwakumbusha walimu kuwa mwaka 2002 Wizara ya Elimu ilitoa Waraka wa Elimu Namba 24 unaohusu adhabu ya viboko na kuweka utaratibu wa utolewaji wake kwa wanafunzi.

Aidha, mwanafunzi anapokataa adhabu ya viboko, sharti asimamishwe shule ili kupisha hatua nyingine za kinidhamu juu ya kosa lake, lakini pia unawaonya walimu kuwa hatua kali za kinidhamu zitachukuliwa dhidi ya yeyote atayekiuka utaratibu ulioidhinishwa na waraka.

Waraka huo pia unapiga marufuku kwa mwalimu yeyote kuonekana na fimbo mkononi kwa lengo la kumuadhibu mwanafunzi, wakati umefika waraka wa adhabu ya viboko uzingatiwe kwa faida ya kila mmoja.

# TANGAZO

IITA Transforming African Agriculture CGIAR

WorldFish

# POSITIONS ANNOUNCEMENT

The International Institute of Tropical Agriculture (IITA) on behalf of WorldFish invites applications for Four positions: **Project Manager, Senior Research Analyst and Research Analyst (2 positions)**

**Background:**
WorldFish is an international, nonprofit research and innovation institution that creates, advances, and translates aquatic food systems science into scalable solutions. We envision an inclusive world of healthy, well-nourished people and a sustainable blue planet, now and in the future. Our mission is to end hunger and advance progress on the 2030 Sustainable Development Goals through science and innovation to transform food, land, and water systems with aquatic foods for healthier people and the planet.

For over 45-years, WorldFish's data, evidence, and insights have shaped practices, policies, and investments to end hunger and advance sustainable development in low- and middle-income countries. We have a global presence across 20 countries in Asia, Africa, and the Pacific, with 460 staff of 30 nationalities deployed where the most significant sustainable development challenges can be addressed through holistic aquatic food systems solutions. Embedded in local, national, and international partnerships, our work sets agendas, builds capacities, and supports decision-making for climate action, food and nutrition security, sustainable fisheries and aquaculture, blue economy, One Health, and AgriTech, integrating gender, youth, and social inclusion.

A core element of the 2030 WorldFish Research and Innovation Strategy: Aquatic Foods for Healthy People and Planet is focused on building the resilience of aquatic food systems to shocks, which is critical during this time of climate, ecological and economic crisis.

WorldFish is part of CGIAR, the world's largest agricultural research and innovation network. For more information, please visit **https://www.worldfishcenter.org.**

## POSITION - PROJECT MANAGER
## IITA-TZ-2024 - WorldFish-004 -NRS- Zanzibar - Unguja

**JOB SPECIFICATION**
**Position Background (short summary of the job)**

The Project Manager for the Asia-Africa BlueTech Superhighway represents the AABS Project at the country level. This role provides leadership in the strategic development and management of the AABS portfolio in country, engagement with new and existing partners, fostering collaborations with national and local partners and serves as the WorldFish contact for the AABS project to the donor (FCDO and BPF).

In collaboration with the AABS Project Lead and the WorldFish country office, the Project Manager coordinates the AABS country operations. The incumbent will regularly engage with other WorldFish country leadership and Headquarter staff.

The Project Manager provides research contributions to the AABS country program in alignment with personal expertise and experience.

**Duty Station:** The position will be based in **Unguja, Zanzibar.**
**Education Qualification and Certification**
- A Master's degree in a relevant discipline such as fisheries, aquaculture, aquatic resources management, international development, environmental science, or related fields, with a minimum of 7 years' experience in leading research projects.
- Project Management Professional (PMP) or similar qualification.
- Proficiency in English and Swahili.

**Skills, Experience and Knowledge (required to perform this job)**
**Competencies:**
- Effective stakeholder engagement and conflict management.
- People and team management, promoting diversity and inclusion and fostering staff wellbeing.
- Excellent communication skills for different audiences.

**Physical Requirements:**
- Regular travel within the country, broader region and globally as required.
- Regular office attendance, encouraging strong attendance across the wider team.

**Desirable Skills/Experience (Nice-to-have to perform this job)**
- Skills in program management, personnel management, and interdisciplinary team leadership.
- Track record of building partnerships with diverse stakeholders, including senior decision-makers and donor agencies.
- Understanding of marine and coastal resources and food system challenges in Tanzania.

**Key Responsibilities**
***Country Project Management and Implementation:***
- Lead the management of the AABS project in the country across all work packages, knowledge management and communications, actively contributing to work planning, budgeting, partner engagement and implementation, ensuring it aligns with FCDO's Blue Planet Fund and COAST priorities.
- Ensure strong linkages between the country project and the overall global program, providing necessary data, reports, and inputs to ensure alignment, knowledge sharing and timely delivery.
- Oversee the delivery, monitoring, and reporting of the project in Tanzania and ensure that the country-level activities feed into the program outcome and MEL system.
- Support country-based scientist and sub-partners to ensure work is implemented in a coordinated way across technical areas.
- Efficiently manage resources, ensuring adequate human, financial, and material assets to ensure timely and quality project implementation.
- Take overall responsibility for the project management process, including implementation, budgeting, risk management, data management, and financial reporting.

**Representation, Engagement**
- Develop and manage relationships with the donor (FCDO), the government, and local stakeholders, effectively representing WorldFish's interests.
- Stay informed about donor and government priorities, country plans and initiatives, and adjust accordingly to ensure alignment with AABS objectives.
- Coordinate WF's engagement with other BPF and FCDO programs to ensure alignment and knowledge sharing.
- Represent AABS at national, and when required, regional and global forums on project management related issues.
- Collaborate with AABS staff and partners to align research projects with national priorities, BPF strategies and FCDO's goals.
- Guide the dissemination and uptake of research findings through stakeholder engagement and through coordination with communication teams.

**Budget Management**
- Support development of the budget across technical areas, guiding budget inputs.
- Monitor the financial position of the country project and ensure alignment with the overall program budget.

**General**
- Undertake other tasks as appropriate, as discussed with the supervisor and WorldFish leadership.

## POSITION - SENIOR RESEARCH ANALYST (Aquatic Food Loss and Waste)
## IITA-TZ-2024 - WorldFish-005 -NRS- DSM

**JOB SPECIFICATION**
**Position Background (short summary of the job)**
The Senior Research Analyst will play a key role in supporting the WP3 activities of the AABS project. Although the primary focus will be activities in Tanzania, there might be cases when some assignments in Kenya and Mozambique are conducted. This role is crucial for conducting targeted research, data analysis, and coordination efforts to implement climate-smart technologies and sustainable practices to reduce aquatic food loss and waste in small-scale fisheries in Tanzania. The position focuses on enhancing the sustainability of fisheries management by reducing loss and waste and improving post-harvest processes within the coastal regions.

**Duty Station:** The position will be based in **Dar es Salaam .**
**Education Qualification and Certification**
- Required qualification is an MSc, with a minimum of five years of relevant experience in the sustainability of Aquatic Foods, such as in Postharvest Food Technology, Agricultural Engineering, Agribusiness, Fisheries, or the Food Industry.
- The qualification should specifically highlight a robust technical understanding and the integration of climate-smart practices and technologies within aquatic food value chains

**Skills, Experience and Knowledge (required to perform this job)**
- **Research and Data Analysis Expertise:** Background in research and data analysis, with a preference for experience in fisheries, agricultural engineering, postharvest technology, or related areas. At least three to five years of experience as a post-harvest specialist in international organisations in developing regions, preferably in Africa.
- **Project Coordination Experience:** Experience in project coordination, particularly in an international or multicultural context.
- **Knowledge of Sustainable Practices:** In-depth understanding of sustainable practices and post-harvest climate-smart technologies in fisheries, agriculture, or related sectors

**Desirable Skills/Experience (Nice-to-have to perform this job)**
- **Cross-Cultural Teamwork:** Proven ability to work with diverse cross-cultural teams.
- **Technical Proficiency:** Skilled in using statistical analysis software and data visualisation tools.
- **Communication Skills:** Excellent communication capabilities, both written and oral, with fluency in English. Proficiency in additional languages relevant to the project locations (Swahili) is highly advantageous.

**Key Responsibilities**
- **Research and Data Analysis:** Conduct comprehensive research and analysis on aquatic food loss, waste, and processing technologies in the target countries—Synthesise data to inform project strategies and decision-making.
- **Project Coordination and Support:** Assist the WP3 lead in coordinating activities across Tanzania, ensuring alignment with project objectives and timely execution.
- **Cross-Country Collaboration:** Facilitate communication and collaboration between project teams in different countries, ensuring cohesive efforts and knowledge sharing.
- **Reporting and Documentation:** Prepare detailed reports, research papers, and presentations to document project progress and findings. Contribute to academic publications and policy briefs.
- **Stakeholder Engagement:** Engage with project stakeholders, including local communities, NGOs, government bodies, and private sector partners, to gather insights and foster collaborative relationships.
- **Innovative Solutions Development:** Contribute to developing and testing innovative, sustainable solutions in fish processing and waste reduction.

**Additional**
This position is an excellent opportunity to join a dynamic, international team working on a high-impact project. The successful candidate will play a crucial role in driving sustainable development and environmental conservation across Tanzania's fisheries sectors. The role demands a blend of technical expertise and innovative thinking, ideal for someone passionate about making a tangible impact in sustainable fisheries management and food systems transformation.

## TWO POSITIONS - RESEARCH ANALYST (Digital Fisheries)
## IITA-TZ-2024 - WorldFish-006 -NRS- Zanzibar Ugunja

**JOB SPECIFICATION**
**About the Project**
Animals, plants and microorganisms harvested and grown in water play a significant role in sustainably feeding and nourishing the world. Globally, 800 million people depend on small-scale fisheries and aquaculture for their livelihoods. But these vital aquatic food systems are hindered by the insecure livelihoods of those in related jobs, their low capacity to adapt to climate change, and the loss of marine nature.
The Asia-Africa BlueTech Superhighway project, supported through the UK's Climate and Ocean Adaptation and Sustainable Transition (COAST) program under the umbrella of the Blue Planet Fund (BPF), will focus on enabling communities to adapt to and mitigate against climate change as well as responsibly and sustainably manage marine and coastal nature and resources resulting in improved food and nutritional security as well as employment and income opportunities. The project will be implemented in two phases over seven years, starting with Phase 1 in Bangladesh, Kenya, Mozambique, Nigeria, and Tanzania.

**About the Position**
WorldFish is looking for a Research Analyst to support activities of AABS Work Package 1- Digital Coast. The primary purpose of this position is to support the Work Package Lead and Scientist based in Zanzibar. The candidate will work in an interdisciplinary team of experts with diverse backgrounds, including data scientists, production systems, gender, climate change, scaling of innovations, science communication, and rural development.

**Duty Station:** The position will be based in **Unguja, Zanzibar.**
**Education Qualification and Certification**
A bachelor's degree in science or economics field.

**Skills, Experience and Knowledge (required to perform this job)**
- Strong working knowledge of MS excel and word.
- Competency with digital smartphone/tablet applications.
- At least 3 years work experience.
- Strong interpersonal skills, and the ability to work in multi-cultural, interdisciplinary teams as well as develop close and effective working relationships with a range of partners.
- Proven ability and willingness to carry out independent fieldwork in remote locations.
- Experience working in communities.
- Commitment to development objectives in Unguja/Pemba.
- Excellent written and verbal communication skills in English and Swahili.

**Desirable Skills/Experience (Nice-to-have to perform this job)**
- Experience in fisheries science, agricultural science or other natural science research.
- Coding experience in R or Python.
- Quantitative skills and experience in data science, management, databases, and statistics.
- Project management experience.
- A valid driving license.

**Key Responsibilities**
- Support research operations, data collection, validation, and reporting on project sites around Zanzibar.
- Monitor and guide fisheries data collectors' regular and timely collection and digital submission of fish landings and sales from remote sites; provide technical support and data validation.
- Update, deploy, and train local staff and partners in the use of digital data systems, data collection protocols, surveys, and basic data management.
- Be a point of contact for local community members, project partners, and interested stakeholders about project objectives and information.
- Facilitate community meetings and trainings related to project aspects in aquatic food systems.
- Prepare progress and fieldwork reports.

**Additional**
This position will be based in Unguja, Zanzibar, but with regular fieldwork travel (60%) to project sites around Zanzibar.

**General information:**
The duration of the contract for all the four positions is two years renewable subject to performance and availability of funds. These are nationally recruited position and IITA offers a competitive remuneration package.
The application pack should include an application letter, copies of certificates, and a curriculum vitae which contains a telephone number, email address, and contact details of two referees. Applications should be sent by email to **IITA-Tanzania@cgiar.org** and addressed to:

**The Country Representative, IITA-Tanzania,**
**Plot No. 25, Mwenge – Coca-Cola Road,**
**Mikocheni Industrial Area,**
**Dar es Salaam, Tanzania**

Applicants are requested to include the **reference number for the position** (as indicated on the heading of the announcement) in the subject of their application letter, as well as in the subject of their email. Please note that any applications without the reference number indicated will be automatically disqualified.

**Closing date for applications: Friday 24th May 2024.** Please note that only shortlisted candidates will be contacted.

# Nishati safi jikoni; Rais Samia nguzo ulinzi afya, mazingira ya Afrika

• Atua Ufaransa kuongoza mkutano wa kimataifa

**Na Mwandishi Wetu**

ULINZI wa afya ya mama, familia, mazingira na taifa dhidi ya mabadiliko ya tabianchi ni lazima uanzie jikoni.

Ndiyo maana Rais Samia Suluhu Hassan, 'champion' wa nishati safi ya kupikia, analiongoza taifa kufahamu kuwa ili raia wawe na afya na mazingira bora, lazima taifa lianze sasa kubadilisha nishati inayotumiwa kupikia.

Akiwa kwenye majukwaa mbalimbali ya matumizi ya nishati safi ya kupikia, Rais anasema huwezi kumaliza au kupunguza ukataji miti unaoangamiza misitu ili kupata kuni na mkaa kama hutaligusa jiko.

Kampeni ya Rais imefanya mengi, Watanzania wameelezwa umuhimu wa matumizi ya teknolojia za kupikia zinazopunguza madhara kiafya, athari kwa mazingira na kijamii.

Na sasa Rais amelifikisha taifa kwenye kutekeleza Mkakati wa Nishati Safi ya Kupikia 2024 - 2034, aliouzindua wiki iliyopita jijini Dar es Salaam.

Analenga kaya zenye 'jiko safi na salama', ambayo asilimia 80 ya Watanzania watakuwa wanatumia jiko lenye nishati safi ya kupikia ifikapo 2034.

Ofisi ya Takwimu ya Taifa (NBS) inaeleza kuwa Tanzania Bara ina takribani kaya milioni 13.9.

Anaeleza kuwa ili kufikia azma hiyo wakuu wa mikoa na wilaya wasimamie matumizi ya nishati safi ya kupikia na kuzihimiza wizara na taasisi za umma kadhalika na sekta binafsi kuzingatia matumizi ya nishati safi ya kupikia ili kulinda mazingira na kuepusha athari nyingi zinazotokana na kutumia nishati zisizo safi.

Pia Rais Samia anaitaka Ofisi ya Makamu wa Rais na Ofisi ya Waziri Mkuu kuandaa na kutoa katazo la matumizi ya nishati isiyo safi kwa taasisi zinazohudumia watu zaidi 100 na kwamba taarifa rasmi kuhusu utekelezaji wa agizo la kuandaa katazo iwasilishwe Agosti, mwaka huu.

Mkakati huo wa kitaifa utapunguza uharibifu wa misitu ikikadiriwa kuwa hekta 469,000 zinapotea kila mwaka kutokana na kuzalisha mkaa na kuni.

Anaiagiza Wizara ya Nishati kufikisha mkakati huo kwa wadau ikutumia Kiingereza na Kiswahili na kuuweka katika mitandao ili usomwe na Watanzania waupate kwa urahisi.

### CHAPUO UFARANSA

Rais ni Mwenyekiti Mwenza wa mkutano wa viongozi na wakuu wa nchi, unaohusika na nishati safi ya kupikia 'global clean cooking energy', kuanzia leo, anatarajiwa kuwaongoza wakuu wa mataifa mbalimbali wanaokutana Paris, nchini Ufaransa.

Mama Samia pamoja na kutetea, anachagiza matumizi ya nishati salama na safi hasa Afrika ambako takriban watu milioni 990 majiko yao hutumia nishati chafu. Anafanikisha jukumu hilo kupitia mradi wa African Women Clean Cooking Support Program (AWCCSP).



Rais Samia Suluhu Hassan akiwa pamoja na viongozi mbalimbali baada ya kuwasili katika Uwanja wa Ndege Paris nchini Ufaransa juzi. Anatarajiwa kushiriki Mkutano wa Kimataifa wa Nishati Safi ya Kupikia kwa Afrika unaofanyika leo jijini Paris. Pia atakuwa Mwenyekiti Mwenza.

### UTEKELEZAJI UNAPOANZA

Mwaka jana Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira inaagiza taasisi zote zinazohudumia watu zaidi ya 100, ifikapo Januari, mwaka huu, ziache kutumia kuni na mkaa kupikia.

Kaimu Mkurugenzi wa Mazingira Ofisi ya Makamu wa Rais, Paulo Deogratius, anaeleza kuwa hilo limefanyika na taasisi nyingi zikiwamo za umma kuanzia Magereza, kambi za majeshi, shule za sekondari, vyuo vya ualimu na vikuu vinatumia nishati safi ya kupikia.

Pia, juhudi zinafanywa na kila taasisi inayohusika na nishati na kwamba mbio za Mwenge wa Taifa 2024, zinabeba ujumbe wa kutumia nishati safi kupikia.

Kaimu Mkurugenzi Deogratius anataja gesi asilia, baiogesi, mkaa na kuni mbadala, umeme, majiko banifu ya aina mbalimbali zinatangazwa ili watu kutumia nishati safi iliyo kwenye mazingira yao.

Akizungumzia juhudi za utekelezaji, Kamishna Msaidizi wa Maendeleo ya Nishati katika Wizara ya Nishati, Styden Rwebangila, anataja mkakati wa kufikisha gesi kila wilaya.

Akizungumza na Nipashe mipango ya kuwapa Watanzania nishati safi ya kupikia, anaeleza kuwa serikali na wadau wanatengeneza mfumo wa usambazaji mitungi kwa kila wilaya ili iwe rahisi kuifikisha kwa mawakala wadogo watakaowauzia wateja vijijini.

Wizara inatarajia kila wilaya itakuwa na wakala wa kusambaza gesi ya kampuni mbalimbali, pamoja na sehemu ya kuipokea na kujaza tena mitungi gesi baada ya matumizi.

Anafafanua kuwa badala ya kuisafirisha mitungi kutoka vijijini hadi Dar es Salaam ili kujazwa tena, kazi hiyo itafanyika wilayani ili kupunguza gharama na kufanikisha upatikanaji kwa ufanisi.

Aidha, anasema wanakusudia pia mkakati ufanikishe kupatikana 'mobile refilling facilities' zitakazotembea maeneo mbalimbali na kujaza tena gesi kwenye mitungi iliyotumika.

Rwebangila anasema wanatarajia huduma itatolewa vijijini kwa kuwafuata wateja maeneo mbalimbali kila wakati, kazi itakayofanywa na kampuni wauza gesi kwa kushirikiana na serikali.

Kadhalika anasema baadhi ya mikoa imeanza kufanya usambazaji wa mitungi ya gesi kwa wananchi kwa majaribio na baadhi ya maeneo hayo ni Dar es Salaam, Mwanza, Morogoro na Dodoma.

"Ni katika juhudi za kupunguza gharama za kununua mtungi na gesi kwa mara ya kwanza ambako wanunuzi wanatumia zaidi ya Shilingi 100,000 na wakati mwingine hawana," anasema.

### JIKO SANIFU

Kamishna Msaidizi Rwebangila, anazungumzia kunufaika na kutumia majiko banifu, akisema ili kupata faida ni lazima ithibitike kitaalamu kuwa jiko hilo linatumia mkaa au kuni kidogo, kutoa kaboni kidogo pia kupika kiufanisi.

"Awali vipimo na kupata uthibitisho huo vilifanyika nje ya nchi. Lakini sasa tumeiwezesha TBS na Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda (TIRDO), kufanya vipimo na kutoa vibali vya uthibitisho wa ubora, ili huduma isambae na kuwafikia wanachi wengi kwa gharama nafuu."

### USHIRIKISHA VYUO VIKUU

Dk. Kamugisha Byabato, Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha SAUT Mwanza na mbobezi wa masuala ya nishati, anaunga mkono ujio wa mkakati wa matumizi ya nishati safi ya kupikia.

Anashauri wahandisi na wataalamu wa vyuo vikuu na taasisi za teknolojia kushiriki kwa kutengeneza vifaa vinavyotumika kuandaa vyakula mfano sufuria za majiko ya gesi na umeme, na zile zinazotumia mvuke au 'presha' badala ya vifaa hivyo kuagizwa nje.

Aidha, wataalamu hao watumike kutengeneza vichwa vya kuwashia majiko ya gesi ambavyo vimeundwa kuchanganya hewa na gesi kwa vipimo maalumu ili kuwezesha gesi kuwaka na kuleta moto badala ya kutegemea kiberiti, anasema.

Mkakati ushirikishe viwanda vya kuandaa wataalamu, wabunifu na wavumbuzi kwenye vyuo vikuu mfano 'incubation centres; kama kwenye Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, kuna Tachnology Development and Transfer Centre (TDTC) zitumiwe kuzalisha vifaa kama hivyo.

Pia viwanda na wataalamu watumike kutengeneza mitungi au mapipa ya gesi ya ujazo mbalimbali yatumiwe kujaza gesi asilia inayozalishwa nchini na kufikishwa kwa wateja kwa urahisi.

Dk. Byabato anaamini kuwa ni rahisi kutengeneza baadhi ya vifaa nchini kwa sababu matangi ya kubeba mafuta na gesi yanayotumiwa na malori yanaundwa nchini hivyo mkakati huo unaweza kutumia vyuo vikuu vya Dar es Salaam, SAUT, Mandela Taasisi za Teknolojia za Dar es Salaam na Arusha ili kuzalisha vifaa hivyo na kuajiri Watanzania.

Anazungumzia pia VETA, taasisi za ufundi na vyuo vikuu kuangalia matumizi ya mwanga wa jua kupata nishati safi ya kupiki akisema: "Jua linaweza kutumika kupika, kupasha moto au kuchemsha maji. Kwa kutumia vifaa ambavyo vinaweza kuundwa na taasisi hizo majiko ya vyuo vikuu, hospitalini, shuleni, hoteli, magereza, majeshi yakavitumia kuchemsha maji ili kupikia vyakula mbalimbali badala ya kuanza na maji ya nbaradi."

Anasema teknolojia ya kutumia joto la jua inaweza pia kutumiwa kufua, nguo na vyombo hospitalini na kwenye huduma za tiba badala ya kutegemea kutumia gesi au umeme kuchemsha maji au kutengeneza mvuke.

### SHULE ZISHIRIKI

Mwalimu Dk. Ruben Lumbagala wa Sekondari ya Mlali mkoani Dodoma, anasema shule za msingi na sekondari zishiriki kufikisha ujumbe kwa jamii kuhusu utekelezaji wa mkakati huo kwa kuwakumbusha mara kwa mara wanafunzi kuhusu nishati safi ili kuhimiza matumizi ya nishati safi jikoni. Anaamini wanafunzi watafikishia wazazi, walezi na jamii pia kuhamasisha utekelezaji kiufanisi wa mkakati huo.

Mama Lishe, mkazi wa Kigogo Posti, Bahati Boaz (38), anaunga mkono ujio wa nishati safi, akieleza kuwa amesikia habari mkakati wa nishati safi ya kupikia, lakini ana wasiwasi na mama lishe wadogo.

Anasema kwa siku anatumia Sh. 10,000 hadi 15,000 kununua mkaa ambayo ni gharama ya mtungi mdogo wa gesi wa kilo tatu, unaouzwa Sh. 19,000.

### NISHATI SAFI

Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira na Wizara ya Nishati, zinataja baadhi ya teknolojia za nishati safi kuwa ni mkaa na kuni mbadala, majiko ya gesi na umeme yanayotumia kiasi kidogo cha nishati hiyo, mafuta (bioethanol).

Bioethanol ni nishati inayotokana na kuchachushwa mabaki ya sukari na nafaka, wakati gesi ya mtungi au LPG ni ile inayohifadhiwa katika mitungi.

Nishati safi ya kupikia ni pamoja na gesi asilia, hii inapatikana nchini ikitumika kuzalisha umeme na matumizi ya viwandani, nyumbani na vyombo vya usafiri.

Kadhalika bayogesi inayotokana na kuchakata kinyesi cha wanyama na binadamu, mabaki ya vyakula au masalia ya mimea huzalisha nishati safi ya kupikia.

Umeme ni moja ya nishati safi na serikali imeendelea kujenga miundombinu ya uzalishaji, usafirishaji na usambazaji umeme ili kumfikia kila Mtanzania mijini na vijijini.

Nyingine ni matumizi ya majiko banifu na ya nishati ya jua yote hutumia teknolojia zenye ufanisi unaopunguza moshi wenye taka sumu zinazoathiri afya za watu na mazingira.

Nishati chafu inayoandaliwa katazo la kuachana nayo ni kinyesi cha wanyama na mabaki ya mimea, kuni, mkaa, mafuta ya taa yote haya huathiri watu na mazingira.



## KANDA KASKAZINI

# Waziri atangaza 'vita' wanaozuia watumishi kupanda vyeo

**Na Hamida Kamchalla,** TANGA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohamed Mchengerwa, ameapa kula sahani moja na viongozi wa sekta ya afya wanaoshiriki kuzuia watumishi na watendaji kutopanda madaraja.

Aidha, ametishia kuwaondoa kwenye nafasi zao viongozi wote wanaohusika kukwamisha watumishi kupanda madaraja katika ngazi mbalimbali, huku akisisitiza jambo la watumishi kupandishwa madaraja kuwa ndiyo kipaumbele chake.

Alitoa kauli hiyo mwishoni mwa wiki, wakati akifungua maadhimisho ya 51 ya Siku ya Uuguzi Duniani ambayo kitaifa yalifanyika mkoani Tanga.

Kutokana na malalamiko yaliyopo hivi sasa, Waziri Mchengerwa, alimwagiza Mkurugenzi wa Afya, kusimamia jambo hilo kwa haraka ili kila mmoja mwenye sifa ya kupanda daraja apandishwe kulingana na anavyostahili.

"Mkurugenzi wa Afya, nakukabidhi hili kama tumeweza katika maeneo mengine kwanini tushindwe kuwapandisha madaraja na kama kuna kiongozi yeyote anayekwamisha katika maeneo yenu anayezuia madaraja msipandishwe nitamuondoa kwenye nafasi yake," alisisitiza.

Aliongeza: "Rais Samia Suluhu Hassan, ametoa nafasi kwa kila mtendaji wale wenye sifa na hadhi ya kupandishwa madaraja wapandishwe mara moja, hayo ndio maelekezo".

Katika hatua nyingine, Waziri Mchengerwa, aliagiza kila halmashauri nchini, kutenga fedha kwa ajili ya posho za watumishi pindi wanapoandaa mikutano kama hiyo kwa kuwa mikutano hiyo ipo kisheria na kwenye bajeti kila mwaka.

Kabla ya ufunguzi huo, Mkuu wa Mkoa Tanga, Balozi Dk. Batilda Burian, alisema katika kipindi cha miaka mitatu katika sekta ya afya, mkoa huo ulipokea zaidi ya Sh. bilioni 67.9 kwa ajili ya ujenzi wa zahanati 72, huku bilioni tisa zikitumika katika ujenzi wa vituo vya afya 23.

Awali, Rais wa Chama cha Wauguzi Tanzania, Dk. Alexander Baluhya, alisema kumekuwa na changamoto katika baadhi ya maeneo kwenye halmashauri zao ikiwamo wauguzi kupangiwa majukumu yasiyo ya kwao yaliyopo nje ya taaluma yao hususani suala la kufanyishwa usafi.

Alisema: "Hili tumelifuatilia na tumeona ni miongoni mwa maeneo yanayoathiri utoaji wa huduma za afya mtu anajikita kutumia nguvu nyingi kwenye jambo, ambalo si la kitaaluma na haliko kwenye wito".

**Rais Samia Suluhu Hassan, ametoa nafasi kwa kila mtendaji wale wenye sifa na hadhi ya kupandishwa madaraja wapandishwe mara moja, hayo ndio maelekezo.**

# RC afichua biashara usafirishaji binadamu inavyofanyika mpakani

**Na Hamida Kamchalla,** TANGA

MKUU wa Mkoa wa Tanga, Balozi Batilda Buriani, amefichua siri kuhusu malori yanayobeba makontena ya mafuta ya kula, kutengenezewa viti maalum ndani yake ambavyo hutumika kwa biashara ya usafirishaji wa binadamu katika mipaka ya kimataifa.

Kutokana na udanganyifu huo, ameagiza kufanyika ukaguzi wa kina hatua kwa hatua ndani ya malori yote na magari ya kifahari ili kukabiliana na makosa ya usafirishaji wa binadamu.

Dk. Buriani alifichua hayo jana, alipotembelea mpaka wa Horohoro ulioko Wilaya ya Mkinga, mkoani hapa.

Aidha, ameziagiza mamlaka zinazosimamia Kituo Jumuishi cha Forodha Horohoro, kufuatilia na kudhibiti utoroshaji wa madini ya vito kwenye eneo hilo kwa kuwa kunaikosesha serikali mapato.

Awali, Ofisa Mfawidhi wa Kituo cha Horohoro, Shadrack Mbonea, alisema kituo hicho kinakabiliwa na tatizo la ukosefu wa baadhi ya vifaa kama scanner ya mizigo mikubwa, pamoja makazi ya watumishi.

"Pamoja na matatizo yanayotukabili lakini tumeweza kufanikiwa kuvuka lengo katika ukusanyaji wa mapato ambapo katika mwaka wa fedha 2023/2024 kituo kimekusanya Sh. bilioni 68.5, sawa na asilimia 117.18 ya lengo," alisema.

Naye Kaimu Meneja wa Mamlaka ya Bandari ya Tanga, Peter Milanzi, alisema uboreshwaji wa bandari hiyo, umefungua milango ya biashara katika Mkoa wa Tanga na kwa sasa, baada ya kuwa na uwezo wa kuhudumia meli tatu kwa wakati mmoja.

Milanzi alisema ndani ya kipindi cha miaka minne idadi ya meli zilizohudumiwa bandarini hapo imeongezeka kutoka kwa asilimia 16.2 ambapo mwaka 2018/19 kabla ya uboreshwaji zilihudumiwa meli 125 na mwaka 2022/ 23, zilihudumiwa meli 195 baada ya uboreshwaji.

Alibainisha kwamba ongezeko la abiria wanaotumia bandari hiyo ilipungua katika kipindi cha mwaka 2021/ 22 idadi ilipungua baada ya meli ya kampuni ya Azam iliyokuwa ikifanya safari zake kuharibika.



Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Queen Sendiga (aliyechuchumaa), akiwasalimia wagonjwa jana katika Hospitali ya Halmashauri ya Mji wa Babati maarufu Hospitali ya Mrara baada ya kuwapokea madaktari bingwa na bobezi 35 ambao ni maarufu kwa jina la madaktari wa Samia walioletwa mkoani Manyara kutoa huduma kwa halmashauri zote saba. **PICHA: JALIWASON JASSON**

# Mameneja rasilimali watu kusimamia utendaji

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MAMENEJA rasilimali watu wameagizwa kusimamia, kuimarisha utendaji kwa watumishi ili kuleta mabadiliko ya uendeshaji serikalini pamoja na kuondoa kero zinazohusu wananchi, ikiwamo kuepuka migongano isiyo ya lazima.

Agizo hilo lilitolewa jana jijini Arusha na Katibu Mkuu Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Zena Ahmed Said, wakati wa Mkutano wa Mtandao wa Mameneja Rasilimali Watu katika Utumishi wa Umma Barani Afrika, Tawi la Tanzania (TPSHRMNET).

"Endapo mameneja rasilimali watu watazingatia haki na kutumia kwa usahihi matumizi ya Tehama kupitia Mamlaka ya Serikali Mtandao (E-Goverment ) itawezesha maendeleo kupatikana, kwani Tanzania imefanya vizuri katika utoaji huduma kwa njia ya mtandao na kuwa ya pili katika nchi za Afrika na kwa upande wa Afrika Mashariki (EAC), kuwa ya kwanza katika matumizi ya TEHAMA," alisema.

Alisema matumizi ya TEHAMA katika utoaji huduma za serikali yameongezeka, hivyo ni lazima mameneja hao wakasimamia vizuri matumizi katika utoaji huduma nzuri kwa wananchi.

"Suala la kufanya tathmini na utendaji kazi ni lazima, hivyo waajiri wote wazingatie hilo kwa mujibu wa sheria na taratibu na mjaze fomu maalum za kupima ufanisi makazini," alisema.

Katibu Mkuu Mstaafu, Ofisi ya Rais -Utumishi wa Umma, George Yambesi, aliwaasa maofisa hao kuhakikisha wanafanya kazi kwa bidii katika mabadiliko ya kasi ya teknolojia, hususani akili bandia na uongozi katika utumishi wa umma, ikiwemo kuweka mawazo ya kimkakati.

Rais wa Mtandao wa Mameneja Rasilimali Watu, katika Utumishi wa Umma Barani Afrika, Xavier Daudi aliipongeza Tanzania kwa kupiga hatua katika utoaji huduma bora, kupitia kwa maofisa hao katika kuhakikisha maendeleo yanakua kwa kasi.

Alisema maofisa hao ni mojawapo kati ya kiungo kizuri kati ya serikali, watumishi na wananchi katika kuhakikisha wanaweka mikakati dhabiti ya ufanisi, ili kuhakikisha kazi zinafanyika ikiwamo kujiwekea mikakati dhabiti, ikiwamo kwenda sanjari na teknolojia ya akili bandia inayokuja kwa kasi, katika matumizi ya teknolojia.

Katibu Tawala Msaidizi Utawala na Usimamizi wa Rasilimali Watu, David Lyamongi, alisema mkutano huo utaleta tija na matokeo chanya katika kuwahudumia wananchi vizuri ikiwamo kujiwekea mikakati dhabiti ya kuwezesha kazi kufanyika kwa ufanisi.



# Hospitali yaomba msaada wa damu kunusuru wajawazito

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

HOSPITALI ya Halmashauri ya Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga, imewataka wananchi kujitokeza na kuchangia damu, ili kunusuru vifo vya wajawazito na watoto ambavyo vinatokea wakati wa kujifungua.

Mratibu wa Damu Salama wa Halmashauri hiyo, Noel Malaki, alitoa wito huo jana wakati wa uzinduzi wa kampeni ya 'Tujibebe andaa kesho yako' iliyoandaliwa na Shirika la Girl Efect kwa lengo la kuwafikia vijana na mabinti wenye umri wa miaka 18 mpaka 29 kwa kuwaelimisha afya ya uzazi, kiuchumi na kielimu.

Alisema uhitaji wa damu ni mkubwa kwa sababu hakuna sehemu ambayo wanaweza kwenda kuinunua, akisema kwa siku wanatumia chupa 15 hadi 20, kwa mwezi chupa 450 hadi 600, kwamba wenye uhitaji mkubwa ni wajawazito na watoto kulinganisha na kundi la watu wanaopata ajali.

Malaki alisema ili wafanikiwe kupata damu hizo wanalazimika kuwatembelea wanafunzi wa shule za msingi na sekondari, vyuo vya kati, kwenye mikusanyiko kama vile magulio na minada pamoja na madhehebu ya kidini.

Hivyo aliwataka wananchi kujenga tabia ya kujitolea damu ili kuendelea kunusuru vifo vya wajawazito na watoto.

"Kampeni hii imetusaidia tumepata chupa 14 za damu ambazo zitatumika kuokoa maisha ya wajawazito, watoto na waliopata ajali, kuwafikia watoto wenye umri wa miaka 10 na kuendelea na kuwapatia chanjo ya saratani ya mlango wa uzazi....Tujenge tabia ya kujitolea damu kwasababu haiuzwi sehemu yoyote," alisema Malaki.

Mkazi wa Kata ya Malunga, Paschal Unyango, alisema mwaka 2019 alimpoteza ndugu yake kwa ukosefu wa damu, hivyo amekuwa mtu wa kujitolea damu mara kwa mara ili iweze kuokoa maisha ya wengine hasa wajawazito.

Aliwataka watu kujitokeza na siyo kuchangia mpaka ndugu au jamaa zao wanapopata shida ya damu.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Dk. Yudas Ndungile, alisema uhitaji wa damu ni mkubwa katika hospitalini na vituo vya afya na kuomba kampeni hiyo iendane na kuwahimiza vijana kujitolea kuchangia damu pamoja na kuwaelimisha namna ya kujikwamua kiuchumi ili kuondokana na vijana tegemezi kwenye jamii.

Meneja wa Kanda ya Magharibi wa kampeni hiyo, Michael Luvanda, alisema kampeni hiyo inalenga kuwafikia vijana wa rika zote wenye umri wa miaka 18 mpaka 29 na kuwaelimisha juu ya masuala ya uzazi wa mpango, elimu na kichumi kwa kuwaunganisha na fursa mbalimbali.



Mwendesha bodaboda akisafirisha mzigo uliozidi uwezo wa chombo hicho eneo la Mwenge, Dar es Salaam juzi, kitendo ambacho kinaweza kusababisha ajali. **PICHA: SABATO KASIKA**

## Wadaiwa kukwamisha vita dhidi ya ukatili wa kijinsia

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

BAADHI ya wanawake kutoka Iselamagazi wilayani Shinyanga, wamedaiwa kukwamisha mapambano dhidi ya ukatili wa kijinsia kutokana na kugoma kutoa taarifa wanapopigwa na wenza wao.

Inadaiwa kuwa wanawake katika eneo hilo wamekuwa wakipigwa na wenza wao, huku wengine wakipigwa hadi kuzimia lakini wanapotakiwa kutoa taarifa wanakataa wakiogopa kupewa talaka.

Hayo yalibainishwa juzi na Mwenyekiti wa Jukwaa la Wanawake Kata ya Iselamagazi, Zainabu Jilumbe, wakati akizungumza na Nipashe kufuatia hali hiyo.

Alisema katika kata hiyo kuna ukatili wanawake umekithiri ambapo wanawake wanapigwa na wenza wao, huku wengine wakipigwa na kuzimia mara kwa mara lakini hawataki kutoa taarifa kuhusu ukatili huo wanaofanyiwa.

Alisema hivi karibuni wanatarajia kukaa vikao na wanawake wa kata hiyo na kuwapa elimu juu ya kupinga vitendo vya ukatili kutoka kwa waume zao pamoja na kutoa taarifa ili kudhibiti tatizo hilo la unyanyasaji.

Aidha, alisema tatizo ambalo limekuwa likisababisha ukatili dhidhi ya wanawake ni wanaume kuendekeza masuala ya mfumo dume ambapo licha ya vipigo sasa hivi wamekuwa wakichukua mavuno ya mpunga kwenda kuhonga wanawake wanaojiuza ambao hutoka mjini na kuiacha kaya kwenye umaskini.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Iselamagazi, Emmanuel Humba, alikiri kukua kwa kwa vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake katika eneo hilo, akisema baadhi yao wamekuwa wakitoa taarifa na kukaa nao pande zote mbili na kuwasuluhisha.

# Dola milioni 99,200 zapeleka kicheko kwa wenye ulemavu

**Na Mary Geofrey,** GEITA

KWA muda mrefu watoto wenye ulemavu mkoani Geita wamejikuta wananasa katika kilindi cha imani potofu kuhusu watu wenye ulemavu huku jamii kubwa ikiamini kwamba ulemavu ni laana.

Mradi wa 'Ondoa Imani Potofu dhidi ya Watoto Wenye Ulemavu' wa miaka miwili wenye thamani ya Dola za Marekani 99,200 sasa unabadili maisha ya watu wenye ulemavu na kuacha alama chanya za kudumu kwa watoto wenye ulemavu na kufungua milango ya fursa kwao.

Ni habari njema yenye kutia matumaini kwa waliokata tamaa na pengine kutengwa na jamii. Shujaa wa habari hiyo ni Mgodi wa Dhahabu wa Geita, kampuni tanzu ya AngloGold Ashanti.

Kwa kushirikiana na Kanisa Katoliki Jimbo la Geita na Baraza la Dhahabu Duniani (WGC), mgodi huo unaendesha mradi wa kusaidia watoto wenye ulemavu na kubadili mtazamo potofu wa jamii kuhusu ulemavu.

Kwa mujibu wa Mratibu wa Mradi huo, Joseph Massawe, imani hizo zimesababisha watoto wanaozaliwa na ulemavu kunyanyapaliwa, kutengwa na wakati mwingine kutelekezwa na hivyo kusababisha watoto hao kukosa haki zao za msingi kama watoto, pia kama binadamu.

Hali hii ndiyo ilisababisha GGML na Kanisa Katoliki kwa kushirikiana na Baraza la Dhahabu Duniani kufikia uamuzi wa kuanzisha mradi huo ambao unalenga kutetea ustawi wa watoto na kuondoa dhana hiyo potofu kuanzia katika ngazi ya chini kwenye jamii pamoja na kutoa elimu ya uelewa kuhusu haki za watu wenye ulemavu katika nyanja za ksiasa, kijamii, kiuchumi na kitamaduni ili hatimaye kuondokana kabisa na dhana potofu kuhusu walemavu mkoani humo.

Mradi huo unavyotekelezwa, Massawe ambaye ni Mkurugenzi wa Shughuli za Afya wa Jimbo Katoliki la Geita, anasema walianza kwa kubainisha familia zenye watoto wenye ulemavu mbalimbali na kuanza kutoa elimu kwa jamii kuhusu umuhimu wa kuwapa fursa ya kutimiza ndoto zao kupitia vipaji walivyojaliwa.

"Kwanza, tunabainisha familia zenye watoto wenye ulemavu, kisha tunaanza kutoa elimu ikiwa ni pamoja na kuwapeleka shule wale ambao wamefichwa nyumbani na kuhakikisha wanalindwa dhidi ya aina yoyote ya ukatili ili hatimaye waweze kutimiza ndoto zao," anasema.

Anaongeza kuwa malengo ya awali ni kuwafikia watoto wenye ulemavu 200 baada ya mwaka mmoja na kuhakikisha wanapewa mahitaji yao muhimu yatakayosaidia kukuza vipaji vyao katika elimu, michezo au shughuli zingine za kijamii.

Mratibu huyo anasema mbali na mradi huo wa kuondoa mila potofu kwa jamii dhidi ya watu wenye ulemavu, Kanisa Katoliki Jimbo la Geita kupitia Kituo cha Moyo wa Huruma pia wanatekeleza mradi wa kutunza watoto yatima ambao wazazi wao wamefariki dunia kutokana na Upungufu wa Kinga Mwilini (UKIMWI).

Kituo cha Moyo wa Huruma kilianzishwa mwaka 2004 kupitia kampeni ya Mgodi wa Dhahabu Geita dhidi ya UKIMWI inayohusisha watu kupanda Mlima Kilimanjaro (Geita Gold Mine Kilimanjaro Challenge Against HIV/AIDS), Halmashauri ya Wilaya ya Geita na Kanisa Katoliki Jimbo la Geita kimekuwa makazi ya watoto wenye uhitaji kuanzia mwaka 2006, malengo yake ya msingi yakiwa ni kuwalea watoto na kuwaandaa kuwa raia wema na wenye uwezo wa kujitegemea.

Nipashe
# TESA
Jumanne Mei 14, 2024
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI


Ukurasa 14

## Mitaala mipya, uwekezaji vitapunguza kukosa ajira


Ukurasa 12

Kuboresha sekta ya elimu wizara, wadau wanapoanika vipeumbele bajeti 2024/25


Ukurasa 13

Halmashauri inavyoongeza hamasa elimu, yashusha mimba, ndoa utotoni kwa wafugaji

ELIMU

NA RESTUTA JAMES

# Wahitimu SUA katika uwanja mpana kiujuzi, kitaaluma kutumika kimataifa



Wanufaika wa mradi wa SUGECO wakijumuika kwenye mjadala wa 'jiajiri', chuoni SUA. **PICHA: RESTUTA JAMES.**

MAFUNZO kwa vitendo yanayofanyika nje hasa Ulaya na Amerika ni mikakati mipya ya kuwaweka wahitimu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), katika ramani ya ubora zaidi kitaalamu na kiujuzi.

Kupitia mafunzo hayo ya vitendo kimataifa, licha ya wana SUA kukua kiubobezi wana uwanja mpana wa kuajiriwa ndani na nje ya mipaka.

Ni juhudi za Chama cha Ushirika cha Wajasiriamali Wahitimu wa SUA (SUGECO), kinachotoa fursa ya mafunzo kwa vitendo kimataifa (international internships) kwa wana SUA ili kuwaivisha zaidi.

Mpango huo humpika mnufaika ambaye ni mwanachama wa SUGECO, kumuimarisha kiuwezo, mazingira mapya, teknolojia na kumwezesha afanyekazi kwenye tamaduni mbalimbali, anasema Mkurugenzi Mkuu wa SUGECO, Revocatus Kimario.

"Kupitia international internship, wahitimu wanapata nafasi ya kujiimarisha kiuwezo, mazingira mapya, teknolojia na tamaduni mbalimbali za kigeni."

Kimario, anasema hayo kwenye mjadala wa 'jiajiri', unaofanyika SUA hivi karibuni na akiongeza: "Kwa kushirikiana na wadau wa ndani na nje, wanatoa fursa ya mafunzo ya umahiri kwa wahitimu na wanafunzi wa vyuo vikuu wa fani mbalimbali."

Aidha, wote wana fursa ya kujipatia mafunzo Ulaya na Marekani, ambako wanapata mawanda mapana ya kiteknolojia, kufahamiana na watu wa kada mbalimbali duniani ili kukuza ujuzi na kubobea kitaalamu.

Msingi wa SUGECO ni kuwaandaa wanafunzi na wahitimu kuajirika sehemu yoyote duniani baada ya kuingia kwenye programu ya mafunzo kwenye mataifa mengine, anaeleza.

"Nia ni kuwajengea uwezo wa kupambana kimataifa, mtaalamu wa sayansi ya chakula kutoka SUA tumwone akishuka Botswana kwa mfano, aweze kufanyakazi iliyotukuka na akalipwa ujira bora, tunawaandaa katika viwango vya kimataifa," anasema.

Kadhalika, anasema wanafunzi na wahitimu wa fani za sayansi wanapewa nafasi kubwa zaidi na kwamba waliopo kwenye kada za sheria, ualimu wa sayansi, utalii, usimamizi wa hoteli, sanaa ya upishi na usimamizi wa biashara pia wamo kwenye programu za mwaka huu.

Kozi za sayansi ni pamoja na kilimo, sayansi ya mifugo, ranchi, dawa za mifugo, ufugaji, afya ya mifugo, sayansi ya chakula na teknolojia, uhandisi mitambo, agronomia, kilimo cha bustani, sayansi ya mazao, sayansi ya mazingira na uhandisi wa ujenzi.

Anasema fursa hiyo ni kwa wanachuo ambao wanaendelea na masomo na kwa wahitimu wa kozi hizo kutoka vyuo vinavyotambulika na serikali ambao watapelekwa katika nchi za Denmark, Ujerumani, Sweden, Uholanzi, Israel, Norway na Marekani kwa miezi 18.

"Lengo letu ni kuhakikisha vijana wanapata ujuzi wa kutosha na kuwajengea uwezo zaidi kwenye kile walichojifunza ili kwanza waisaidie nchi na pia wawe na sifa ya kufanyakazi popote duniani. Tunataka tuboreshe kilimo nchini kiwe cha kibunifu na cha kibiashara, tuzalishe kwa tija ili tusaidie uchumi na maendeleo ya nchi yetu," anasema Kimario.

Kimario anasema walianza kupeleka wanafunzi 20 Israel mwaka 2015 na sasa wanaweza kupeleka zaidi ya wanafunzi 3,500 katika nchi ambazo wameingia nazo makubaliano.

Anataja mafanikio waliyoyapata kwa kueleza kuwa hivi sasa kuna vijana 500 wanaopata mafunzo kazini nchini Marekani na 600 katika nchi za Denmark, Ujerumani, Norway, Uholanzi, Israel na Sweden.

"Habari njema kwa wanavyuo ni kwamba baadhi ya vyuo vimekubali kuyatambua mafunzo haya na kutoa alama kwenye vyeti vyao, hii ni hatua kubwa kwa sababu itasaidia kuongeza sifa mahsusi kwa mhitimu," anasema.

Anasema changamoto ya fedha kwa ajili ya maandalizi muhimu ya awali kwa wanafunzi wanaopata nafasi hizo yametatuliwa na Taasisi ya CRDB ambayo imetenga EURO milioni 24 (takribani Sh. bilioni 67); ili kuyafanikisha pamoja na mtaji anzia wanaporejea nchini.

Meneja maendeleo wa biashara changa na uatamizi, kutoka CRDB Foundation, Sharon Sule, anasema lengo la kuingia ubia na SUGECO ni kuwapatia vijana fursa ya kuleta mageuzi kwenye sekta za kilimo na ufugaji.

"Kupitia programu yetu ya Imbeju tunawasaidia wanawake na vijana kupitia mtaji wezeshi na kubwa zaidi tunawapa mafunzo mbalimbali za kukuza biashara," anasema.

Anasema kupitia ubia huo, wanafunzi watapata mafunzo bobezi nje ya nchi kwenye fani walizosomea na watakaporejea watapata mtaji anzia kuanzisha biashara zao.

### KUATAMIA MAWAZO

Mbali ya mafunzo nje ya nchi, Kimario anasema programu nyingine waliyonayo ni ya kuatamia mawazo (kuyaendeleza) bunifu ya biashara na tafiti, ili kuchochea ukuaji wa kilimo na biashara kwa lengo la kuzalisha ajira za kutosha.

Anaongeza kuwa wahitimu wa fani za mifugo, ufugaji wa nguruwe, kuku, farasi, kilimo cha bustani na maziwa, wana nafasi ya kuongeza ujuzi kupitia programu ya kwenda kufanyakazi kwa muda mfupi nchini Norway.

Mwenyekiti wa Bodi ya SUGECO na mwanzishi wa ushirika huo, Dk. Anna Temu,

INAENDELEA UK.12

ELIMU

NA SABATO KASIKA

# Kuboresha sekta ya elimu wizara, wadau wanapoanika vipaumbele bajeti 2024/25

HIVI karibui Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ilitaja vipaumbele vikuu vitano kwa 2024/25, inavyovieleza kuwa vinalenga kuleta mageuzi katika sekta ya elimu, ikiwamo ujenzi wa shule mpya 100 za sekondari za ufundi.

Vipaumbele vya wizara vimetajwa baada ya vile vya wadau wa elimu ambavyo wanaamini kwamba vikizingatiwa, vinaweza kuboresha sekta hiyo, hata hivyo serikali haikuvitupia jicho.

Wadau wakiwamo Taasisi ya HakiElimu walitamani bajeti ya wizara hiyo kwa mwaka 2024/2025, itoe kiupaumbele eneo la kuboresho ya Sera ya Elimu na Mafunzo ambayo ni mpya, inayolenga kutoa elimu ya ujuzi badala ya elimu taaluma, licha ya utekelezaji wa maboresho hayo utaanza mwaka 2027.

Mkurugenzi Mtendaji wa HakiElimu, Dk. John Kallage, anashauri kwa wizara kupanga na kutenga bajeti mahsusi ili kufanikisha malengo ya sera hiyo ili kuleta ufanisi na kupata tija.

Hata hivyo, akiwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya wizara yake bungeni, jijini Dodoma, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Profesa Adolf Mkenda, anaeleza ujenzi wa shule mpya 100 za sekondari kuwa ni moja ya vipaumbele vitano.



Mkurugenzi Mtendaji wa HakiElimu, Dk. John Kallage.

> Mkurugenzi Mtendaji wa HakiElimu, Dk. John Kallage, anashauri kwa wizara kupanga na kutenga bajeti mahsusi ili kufanikisha malengo ya sera hiyo ili kuleta ufanisi na kupata tija.

Anasema vipaumbele hivyo vinavyolenga kuleta mageuzi katika sekta ya elimu ambavyo ni kujenga sekondari mpya 100 za za ufundi na kati ya hizo 26 zinatarajiwa kupokea wanafunzi wa kidato cha kwanza Januari mwakani.

Mbali na hicho, kipaumbele kingine ni kuongeza fursa za utoaji mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu ambayo ni kwa ajili ya wanafunzi wenye sifa na uhitaji kutoka 223,201 hadi 252,245 na wanafunzi 84,500 wa mwaka wa kwanza watanufaika.

Wamo pia wanafunzi wa shahada ya kwanza 80,000, shahada za juu 2,000, wanaosoma nje ya nchi 500 na Mfuko wa Ufadhili ya Samia (Samia Scholarship) 2,000 na wanafunzi 157,745 wanaoendelea na masomo.

Prof. Mkenda anataja vipaumbele vingine kuwa ni kuendelea na utekelezaji wa sera na mitaala, mapitio ya sheria na kuandaa miongozo ya utoaji wa elimu na mafunzo na pia kuongeza fursa na kuimarisha ubora wa elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi (amali na amali sanifu), pamoja na elimu ya msingi, sekondari na ualimu.

Lakini pia waziri huyo anataja kipaumbele kingine kuwa ni kuongeza fursa na uimari-

# Wahitimu SUA katika uwanja mpana kiujuzi, kitaaluma kutumika kimataifa

INATOKA UK.11

anasema ilianzishwa mwaka 2011 ili kuwezesha tafiti na wanasayansi wanaohitimu katika vyuo vikuu, wanatumika kuimarisha uchumi na maendeleo ya nchi.

Mkurugenzi wa operesheni na ubunifu wa SUGECO, Joseph Masimba, anasema dunia inataka ubunifu wa hali ya juu na mtaalamu mwenye upekee anayeweza kufanyakazi bila kusukumwa.

"Tunataka tukikushusha Afghanistan, Israel, Kenya, Botswana na kwingineko ufanyekazi inayohitajika...baadhi ya nchi jirani zinapeleka hadi vijana 200,000 kupitia programu kama hizi; jambo linalowajengea umahiri wa kuwa wataalamu wa kimataifa. Sisi bado tuko nyuma na ndio maana tumefungua wigo wa kozi ili vijana wengi zaidi waweze kwenda," anasema Masimba.

Anasema serikali imeingia makubaliano ya fursa za kazi na mataifa zaidi ya 10 duniani yanayotoa wigo kwa Watanzania kuajiriwa na kampuni na mashirika ya nchi husika.

SUGECO ina ofisi nne za kanda katika mikoa ya Arusha (Tengeru), Mbeya (Uyole), Pwani (Rufiji) na makao makuu yaliyopo SUA Morogoro na kwamba wanao wawakilishi mikoa ya Kigoma na Singida.

ELIMU

NA JUMBE ISMAILLY, IKUNGI

# Halmashauri inavyoongeza hamasa elimu, yashusha mimba, ndoa utotoni kwa wafugaji



Baadhi ya madiwani wilayani Ikungi wakiwa kwenye mkutano kujadili utekelezaji wa mipango ya elimu. **PICHA: JUMBE ISMAILLY**

UBORA wa elimu na kuongeza umahiri, uelewa kwa wanafunzi na kuleta mabadiliko kwenye matokeo ya mitihani kuanzia shule za msingi na kuendelea hususani kwa wasichana ni jambo linalopewa umuhimu kitaifa, hasa nyakati hizi za kuleta mapinduzi ya namna bora ya kujifunza na kufundisha.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Ikungi, mkoani Singida, Justice Kijazi, anasema kupitia mpango wa kuboresha elimu Tanzania (EQUIP Tanzania), unaoendeshwa kati ya Uingereza na Tanzania, unaolenga kuleta mabadiliko na kuboresha elimu shule za msingi zaidi ya 5,000 zitafikiwa.

EQUIP imejikita kwenye mfumo maalumu wa kuboresha elimu unaozingatia gharama ambazo zinaleta mabadiliko kwa njia zinazoweza kutumiwa nchi nzima na kwamba utekelezaji wa mpango huo ulianza tangu 2014 katika mikoa mitano na baadaye ukafikishwa Shinyanga, Simiyu, Kigoma, Lindi, Mara, Dodoma na Tabora.

Aidha, mwaka 2017 mikoa mingine miwili zaidi ya Singida na Katavi iliongezwa na hivyo kufanya zaidi ya shule 5,000 zenye zaidi ya wanafunzi milioni 2.3 kufikiwa na mipango ya EQUIP,kwa mujibu wa Kijazi.

Anasema mpango huo unaonyesha mafanikio ya kuboresha elimu kwenye kutekeleza mtaala wa elimu kwa kuwezesha wanafunzi wa madarasa ya msingi na awali, la kwanza na la pili, pia kuongeza matokeo ya ujifunzaji katika uwezo wa kusoma, kuandika na kuhesabu tangu mwaka 2014 na kwamba asilimia 43 ya wanafunzi wameongeza kasi ya kusoma zaidi ya alama zilizowekwa kitaifa.

Anaeleza kuwa zaidi ya walimu 49,000 wakiwamo walimu wakuu pamoja na maofisa elimu kata wanaelimishwa kuhusu mafunzo ya walimu kazini ili kukuza taaluma zao kazi inayokwenda pamoja na mpango wa kuwaandaa watoto kuanza shule unaohakikisha kuwa watoto wanaoishi mbali na shule za msingi na wamefikia umri wa kuanza shule kwa kujiunga na vituo vya utayari.

Aidha, Kijazi anasema mpango huo kwa kushirikiana pia na halmashauri unatoa mafunzo kwa walimu wasaidizi wa vituo vya utayari ambao mpaka sasa zaidi ya watoto 444,872 wameandaliwa katika zaidi ya vituo 3,031 kwenye mikoa tisa ili kujiunga na darasa la kwanza.

Kadhalika anasema mipango ya maendeleo ya shule imekuwa shirikishi zaidi na inayojikita katika kukuza ubora wa elimu kwenye mikoa mbali mbali, walimu wakuu wote, wasaidizi wao pamoja na maofisa elimu kata katika mikoa tisa wamepata mafunzo ya kuandaa mipango shirikishi ya maendelo ya shule, anasema.

Anazungumzia mfumo wa taarifa za shule ambao unatumia vishikwambi unaosaidia kutoa takwimu za uhakika na kwa wakati katika usimamizi wa utendaji katika ngazi zote, ambapo shule zote katika mikoa tisa ya mpango wa EQUIP zimeuunda Umoja wa Wazazi na Walimu ili kusaidiana na jamii katika kuboresha shule na maendeleo ya kujifundisha watoto.

Mpango wa EQUIP ulianza kutekelezwa katika Halmashauri ya Ikungi, mkoani Singida mwaka 2017 lengo likiwa ni kuhakikisha kuwa watoto wote wanaandikishwa kuanza shule katika wilaya hiyo.

Ofisa Elimu Msingi wilayani Ikungi, Margaret Kaponesya, akizungumzia mafanikio ya mpango wa EQUIP, anataja ongezeko la kiwango cha kuandikisha wanafunzi wanaoanza shule ni moja ya mambo ya kujivunia.

Margaret anasema kuanzia mwaka 2010 hadi 2015 kabla ya mpango huo uandikishwaji ulikuwa wanafunzi 23,026 lakini sasa wamefikia 33,264 likiwa ni ongezeko la wanafunzi 10,238.

Anafafanua zaidi kuwa kabla ya mpango huo kuanzia mwaka 2010 hadi 2015 kiwango cha uandikishaji wa watoto kutoka familia za wafugaji kilikuwa wanafunzi 450 wakati mimba za utotoni zilifikia 22 na kwa familia za wafugaji zilikuwa ni 29.

Ndoa za utotoni zilikuwa nne lakini kwa familia za wafugaji zilikuwa kati ya ndoa saba hadi tisa, aidha kwa upande wa uandikishaji darasa la kwanza baada ya mpango huo kuanza ulikuwa wanafunzi 33,264 wakiwamo wavulana 16,174 na wasichana 17,090 wakati baada ya mpango wa EQUIP kuanza ndoa za utotoni zilikuwa saba kwa wafugaji zilikuwa tisa na mimba za utotoni zilifikia 21.

"Tunatoa wito kwa wanafunzi kuzingatia masomo wanayofundishwa na waongeze bidii ili kufikia malengo waliyojiwekea na kwa wazazi na walezi wa wanafunzi hakikisheni mnawapatia watoto mahitaji, stahiki pamoja na kufuatilia na kusimamia maendeleo yao shuleni," anasema ofisa huyo wa elimu.

Anaeleza kuwa mabadiliko ya uandikishaji kabla na baada ya kuanza kwa mpango huo yalitokana na kuboresha miundombinu ya majengo na vitendea kazi na ushirikishwaji wa jamii.

Aidha anazitaja hatua za kisheria zitakazochukuliwa kuwa ni pamoja na kufikishwa mahakamani wazazi na walezi ambao watoto wao walipata ujauzito, kuolewa na kuacha masomo na hatua hizo zilipunguza mimba na ndoa za utotoni.

Kuhusu changamoto zilizokuwapo kwenye sekta ya elimu kabla ya mpango huo, Margaret anazitaja kuwa ni upungufu mkubwa wa vyumba vya madarasa na vitendeakazi, wanafunzi kuishi mbali na shule, jamii kutothamini elimu na kutokushiriki kikamilifu kwenye masuala ya elimu na shughuli za maendeleo.

Ofisa huyo wa elimu anasema ujio wa mpango huo umeondoa changamoto hizo na kuzitaja baadhi ya faida walizopata kuwa ni kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia, ongezeko la uandikishaji, kupungua mdondoko wa wanafunzi, jamii kuelewa na kushiriki katika shughuli za maendeleo ya elimu, kuongezeka kwa ufaulu shuleni na ari ya kazi kwa watumishi.

Aidha Margaret anatoa wito kwa kamati za shule kuzingatia miongozo yao katika kusimamia shule huku akiwataka walimu kujituma katika kazi kwa kuzingatia kanuni, sheria na taratibu za miongozo kazini.

Diwani wa Kata ya Iyumbu, iliyopo Ikungi, Peter Kuligwa, anasema kabla ya mpango huo kuanza hali ya elimu haikuwa ya mafanikio makubwa kwani kiwango cha ufaulu kilikuwa chini na miundombinu duni.

Anasema kuandikisha hakujafikia asilimia 100 kwa sababu miundombinu kama madawati na vyumba vya madarasa vilikuwa duni huku wanafunzi walio wengi wanaomaliza masomo walikuwa wakikatisha masomo yao na kwenda kufanya kazi za majumbani kutokana na changamoto.

Akizungumzia suala la utoro kwa wanafunzi, Kuligwa ambaye ni mwenyekiti wa kamati ya maendeleo ya kata hiyo anasema ulikuwa mkubwa wakati kwa upande wa walimu utoro pia ulikuwa umekithiri lakini baada ya mpango huo kuanza mabadiliko makubwa katika kila nyanja yameupungua.

Anafafanua kwamba hali ya uandikishaji iliongezeka hadi kufikia zaidi ya asilimia 100 wakati wanafunzi wanaomaliza shule walianza kutulia mashuleni kutokana na changamoto za ufundishaji na ujifunzaji kupungua, mimba za utotoni zilipungua, mimba za utotoni zilijitokeza kwa watoto ambao siyo wanafunzi huku utoro kwa wanafunzi nao ulipungua na walimu wameacha utoro ambapo kwa hivi sasa wanaipenda na kuifurahia sana kazi yao.

Kwa upande wake Ofisa Elimu Watu Wazima Wilaya ya Ikungi, Daudi Tikae, anasema Halmashauri ya wilaya ya Ikungi ina jumla ya shule shikizi nne ambazo ni Mtakuja, Kipompo, Sanya na Isalanda wakati kwa shule za utayari zipo tano za Mwankalaja, Makurunda, Mshungula, Makilawa na Mufumbu Ahumba na kwamba ni matokeo ya EQUIP.

"Kabla ya kuanza kwa mpango huo kulikuwa na wanafunzi 13,432 wasiojua kusoma, kuandika na kuhesabu lakini sasa wamepunguzwa hadi kubakia wanafunzi 8,751," anasema.

ELIMU

NA MWANDISHI WETU

# Mitaala mipya, uwekezaji vitapunguza kukosa ajira



Wanafunzi wafunzwe zaidi kile wanachokipenda na kukimudu ili kuendeleza ndoto zao na kuepuka shida ya ajira. **PICHA: MWANDISHI WETU**

UTANDAWAZI umekuwa na athari kwenye sekta ya ajira kutokana na idadi kubwa ya watu wanaosaka kazi kukutana na kiwango kidogo mno cha ajira au kazi rasmi za kufanya hasa ofisini.

Hii inamaanisha kuwa wasaka kazi ni wengi kupindukia na ajira au shughuli zakuwapa ajira ni chache mno. Zipo sababu nyingi zinazosababisha uhaba wa kazi kuanzia za ndani ya nchi na nje ya mipaka.

Hilo ndilo wanalokumbana nalo wafanyakazi na watafuta kazi wa Tanzania leo wanapoadhimisha Siku ya Wafanyakazi Duniani.

Kupata ajira ni kazi watu hutoka vijijini hadi mijini kutafuta kazi, hata wageni huvuka mipaka kutafuta kazi na hali bora ya maisha kwa mataifa jirani.

Mambo kama hayo yanashuhudiwa nchini ambako vijana hutoka mikoani kutafuta kazi rasmi na zisizo rasmi kuanzia ukarani, uhasibu ofisini, wapo wanaotaka kuwa walinzi nyumbani na viwandani, kusimamia mifugo, vibarua maeneo mbalimbali, wajenzi na watumishi nyumbani.

Mfano wa kuvuka mipaka upo Afrika Kusini, inayopokea wahamiaji kutoka Ethiopia na mataifa jirani ya kusini mwa Afrika, wanaomiminika kutafuta kazi kuanzia za mashambani, viwandani na ajira wazawa wanazozikimbia.

Fatma Baraka maarufu. Bi Kidude.

Kwa Tanzania ukosefu wa ajira kwa vijana ni mkubwa, ripoti za Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) mwaka 2015, ilikadiria kuwa wasaka ajira wapya kati ya 800,000 hadi 1,000,000 huzalishwa kila mwaka kutoka kwenye taasisi mbalimbali za elimu kuanzia shule za msingi hadi vyuo vya elimu ya juu.

Kiwango hicho ni kikubwa kupita kiasi kwa wana taaluma hivyo kuzidisha ukosefu wa ajira, kwani nafasi za kazi haziwezi kuchukua nguvu kazi inayokua kila mwaka.

Changamoto za ukosefu wa ajira zinaelezwa kuwa ni pamoja na mfumo wa elimu, ukosefu wa ujuzi katika mafunzo ya biashara, uhaba wa mikopo, mkazo katika sekta rasmi pekee kuwa kijana anaajiriwa serikalini na au kwenye kampuni linalojulikana.

Lakini pia kilimo kwa miaka mingi hakiwavutii, vijana na kwa upande wa wanawake ni matokeo ya kukosekana usawa wa kijinsia unaowabagua na kuajiri zaidi wanaume.

Kwa ujumla siku ya Mei Mosi au ya Wafanyakazi inazidi kupungua 'utamu' barani Afrika ambako idadi kubwa ya vijana hawana ajira kwa sababu ya ukosefu wa elimu na mafunzo, lakini hata kwa waliosoma wana ujuzi usiotosha kuajirika au kuchukuliwa kwenye soko la ajira.

Zaidi ya hayo mashirika ya kimataifa kama World Bank (WB) na Shirika la Kazi Duniani ( ILO) vinagusa pia suala la vyuo vya juu, kati na sekondari kushindwa kutoa mwongozo wa kutosha baada ya wanafunzi kuhitimu na kuwaacha bila kuwaandaa kuwa nguvu kazi inayoweza kuajirika au kujiajiri.

Sababu nyingine kubwa ya ukosefu wa ajira ni kukosekana uwiano kati ya idadi ya kazi zilizopo na jeshi la vijana wanaoingia kwenye soko la ajira kila mwaka, kama ilivyo kwa Tanzania.

Rushwa na uhujumu uchumi ni tatizo kwa sababu ufisadi na usimamizi mbovu wa fedha hukwamisha miradi ya uchumi ambayo ingefanikisha kupatikana ajira kwa vijana.

Kama ripoti ya mkaguzi na mdhibiti wa fedha za serikali (CAG), kila mwaka inavyoonyesha upotevu wa fedha za umma, ni kweli kuwa ni mambo yanayoweza kudhoofisha ukuaji wa viwanda, miradi ya umma, kampuni na uchumi kwa ujumla.

Ni kwa sababu rasilimali zinatumiwa vibaya na kupunguza nafasi za ajira badala ya kuzalisha kazi hivyo kuchangia ugumu wa maisha kwa vijana.

Kwa mfano baadhi ya taasisi za umma kama mashamba ya mifugo na kilimo, yangeendelezwa huenda vijana wangekuwa na kazi lakini hata sasa zinasuasua.

Upotevu wa mabilioni ya fedha za umma kama CAG anavyoonyesha huchangia kupunguza ajira kwa sababu miradi haiendelei kwa kasi na kuzalisha fursa hivyo ajira nazo hazipatikana kwa vijana.

**UFUMBUZI**

Juhudi zimeanza kufanyika mfano kuboresha mitaala ili kukidhi mahitaji ya sekta mbalimbali na maendeleo ya kiteknolojia ili kuandaa wahitimu wenye ujuzi unaohitajika na soko la ajira kwa wakati wote.

Masuala mengine kama kujifunza kwa vitendo ili kuziba pengo kati ya maarifa ya kinadharia darasani na matumizi ya elimu kulingana na hali halisi ilivyo 'duniani.'

Programu za uanagenzi zinafanyika ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Ajira na Vijana ikisimamia jukumu hilo.

Kukuza elimu ya ufundi na mafunzo ya amali ni jambo jipya kwenye mtaala linaloboresha hadhi ya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi kwa kutoa njia mbalimbali za kuajiriwa na kujiajiri kwa wanafunzi au wahitimu.

Lakini, pia wakati umefika wakushirikiana na viwanda ili kutengeneza programu za mafunzo ya ufundi stadi zinazoshughulikia mahitaji mahususi ya soko la ajira kwenye viwanda nchini.

Kwa mfano kiwanda cha kutengeneza marumaru, vioo na hata vifaa vya TEHAMA vinapoanzishwa nchi wamiliki, taasisi za mafunzo, wadau na serikali wachambue nafasi za kazi zitakazopatikana kwenye uwekezaji huo ili vijana waandaliwe na kufundishwa kuchukua ajira viwandani.

Katika kukabiliana na tatizo hilo kujumuisha elimu ya ujasiriamali katika mtaala ili kukuza utamaduni wa uvumbuzi na kujiajiri ni muhimu zama hizi. Yote hayo yaendane na kutoa mafunzo kwa vitendo namna ya kupanga biashara, kutunza fedha, kusimamia miradi na ulinzi wa mtaji na zaidi kuainisha masoko.

Kuhimiza wanafunzi kukuza na kutekeleza mawazo yao ya biashara kwa vitendo kupitia ushauri na programu za wataalamu, AZAKI kuwasaidia na pia kusisitiza kukuza ujuzi na kujitegemea, mathalani Taasisi ya Great Hope Foundation (GHF) ya Dar es Salaam, inahamasisha utambuzi wa vipaji na uwezo wa wanafunzi shuleni.

Mratibu wa tuzo hizo, Noelle Mahuvi, anasema nia ni kuwafikirisha vijana wadogo walipo shuleni kutumia vipaji na ugunduzi na kufanya kazi wanazozimudu.

Kuruhusu wanafunzi kuchagua kutoka aina mbalimbali za masomo na ujuzi kuendana na mambo yanayowavutia na uwezo wao, lakini pia kutoa elimu kulingana na umahiri kama mwanafunzi ni bingwa wa kemia, muziki, upishi, kandanda aendelee kwenye ujuzi huo mahususi badala ya kukamilisha muda uliowekwa wa kukaa darasani kuanzia msingi hadi chuo kikuu.

Aangaliwe kwa umahiri na atayarishwe na kuhakikisha kuwa amejitayarisha vyema kwa ajili ya kufanya kile anachokitaka, kimudu na kukipenda.

Wakati huo huo uanzishwa ushirikiano kati ya taasisi za elimu na viwanda ili kuwezesha kubadilishana maarifa na kukubaliana kuwa wasomi au wataalamu wa namna gani wanaohitajika kwa nyakati tofauti waandaliwe.

Kuanzisha miradi ya pamoja ya utafiti na mafunzo kazini ambayo huwapa wanafunzi fursa ya kukabili changamoto halisi na kuboresha uwezo wa kuajiriwa.



# Kampeni kukabili tabianchi kuanzishwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KATIBU Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Cyprian Luhemeja amesema serikali inatarajia kuja na kampeni mahsusi ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, ili wataalamu waeleze mbinu mbadala za kukabiliana nayo.

Akizungumza jana baada ya kufungua mkutano wa nchi zaidi ya 30 duniani ulioratibiwa na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) wa masuala ya mazingira, Luhemeja alisema serikali inaendelea na jitihada za kupambana na mabadiliko hayo ikiwamo kuanzisha biashara ya hewa ya ukaa.

**Wajumbe wa mkutano huo watapelekwa kwenye miradi na kuoneshwa namna wanavyopambana na mabadiliko hayo kwenye maeneo yenye ukame.**

Alisema kupitia mkutano huo serikali imeomba mfuko huo kuongeza fedha kwa NEMC, kuanzisha kampeni ya kitaifa ya mapambano ya mabadiliko ya tabianchi badala ya kulalamika.

Alisisitiza utendaji wa NEMC umeendelea kuimarika hasa kwenye usimamizi wa mazingira na imeratibu mkutano huo kwa kushirikiana na mfuko wa mazingira wa mabadiliko ya tabianchi.

"Hawa wageni wamekuja kujifunza kazi zinazofanywa na NEMC, mafanikio na changamoto ambazo NEMC inapitia, lakini kuna miradi mingi inafanyika ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi katika Wilaya ya Kongwa, Bahi na Arusha," alisema.

Naye Mratibu wa Mfuko wa Kimataifa wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi, kutoka NEMC, Fredrick Mulinda, alisema baraza hilo ndiyo linalosimamia fedha za kuhimili mabadiliko hayo nchini na mkutano huo umejumuisha taasisi zilizopata ithibati ya mfuko huo kutekeleza miradi kwenye nchi mbalimbali.

Alisema wajumbe wa mkutano huo watapelekwa kwenye miradi na kuoneshwa namna wanavyopambana na mabadiliko hayo kwenye maeneo yenye ukame.

Nao washiriki wa mkutano huo walisema wamechagua kuja kukutana nchini na kujifunza namna Tanzania inavyoshirikisha wananchi wake kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi.

## Katibu afya aagiza kukarabatiwa karakana za vifaa tiba

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Afya, Dk. John Jingu, ameagiza kuimarishwa kwa karakana za wizara hiyo ili ziweze kutumika kutengeneza vifaa tiba.

Dk. Jingu alisema hayo juzi jijini hapa, wakati akipokea vifaa vya hewa tiba ya oxygen vilivyotolewa na Shirika la Clinton Health Access Initiative (CHAI) kwenye Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma.

Alisema karakana zote ambazo zinatumika kutengeneza vifaa tiba zinapaswa kuimarishwa ili kuondokana na changamoto iliyopo hivi sasa.

Alisema kama karakana zilizopo nchini zitatumika kikamilifu zitasaidia kuondokana na tatizo la uhaba wa vifaa tiba, ambavyo vimekuwa vikihitajika kwa wingi nchini.

Aidha, katika msaada huo shirika hilo limetoa vifaa mbalimbali vikiwamo handheld pulse ox meters, oxygen analyzers na oxygen wallflow meters.

Akipokea msaada huo Dk. Jingu alisema vifaa hivyo watavitumia vizuri lakini ni lazima waimarishe karakana zilizopo ili waweze kutengeneza vifaa tiba nchini.

Kadhalika, alisema uboreshaji wa huduma za afya ni jukumu la wadau wote ikiwamo sekta binafsi ili huduma ziwe za uhakika na ubora.

"Lazima tujiulize je kuna uendelevu katika utumiaji wa hivyo vifaa, uwepo wa vifaa tiba ni msingi wa huduma bora na za uhakika," alisema Dk. Jingu.

Mkurugenzi wa Shirika la CHAI, Dk. Ester Mtumbuka, alisema taasisi hiyo ilianzishwa na aliyekuwa Rais wa Marekani, Bill Clinton mwaka 2002.

Alisema mwaka 2002 walianza shughuli hizo na walisajiliwa na huduma wanazofanya ni pamoja na kushiriki kutoa huduma za malaria, chanjo tangu mwaka 2013.

"Kwenye chanjo tulishirikiana na serikali kwa kuleta majokofu yasiyotumia umeme, tuliweza kufanya majaribio ya vifaa vya kupima joto kutokea mbali," alisema Dk. Ester.



Mkuu wa Wilaya ya Simanjiro, mkoani Manyara, Fakii Raphael Lulandala (kulia), akiangalia mgodi wa Kampuni ya Franone Mining LTD uliopo kitalu C mji mdogo wa Mirerani, alipofanya ziara ya kutembelea migodi ya Tanzanite juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

## Madaktari bingwa watua Singida kutoa huduma

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

MADAKTARI bingwa 40 wameweka kambi ya siku saba mkoani Singida kwa ajili ya kutoa huduma za matibabu katika hospitali zote za wilaya mkoani hapo.

Ofisa Programu kutoka Wizara ya Afya, Idara ya Afya ya Uzazi, Mama na Mtoto, Joachim Masunga, akizungumza jana wakati wa kuwatambulisha madaktari hao kwa uongozi wa Mkoa wa Singida, alisema watatoa huduma mbalimbali zikiwamo za upasuaji.

Alisema lengo kubwa la madaktari kutoa huduma za kibingwa ni kuwapunguzia wananchi mzigo wa kufuata matibabu sehemu nyingine na kutumia gharama kubwa na sasa watapata huduma hizo katika maeneo yao.

Masunga alisema madaktari bingwa hao watakapokuwa wanatoa huduma hizo watawajengea uwezo watumishi wa afya waliopo kwenye vituo vya kutolea huduma ambapo watanufaika na ujuzi na maarifa.

Masunga alisema utaratibu huu wa kupeleka madaktari bingwa kwenye vituo vya kutolea huduma utapunguza adha za rufaa na wananchi mzigo wa kwenda kutafuta huduma za kibingwa katika maeneo mbalimbali.

Katibu Tawala Mkoa wa Singida, Dk.Fatuma Mganga, alisema hospitali zote zilizopo mkoani Singida zina vifaa vyote vya matibabu na kuwahakikishia madaktari bingwa kuwa watapata ushirikiano kutoka serikali ya mkoa.

Hivyo, aliwataka madaktari bingwa hao kuhakikisha wanatoa huduma vizuri kwa wananchi na kutozua sintofahamu zozote ambazo zinaweza kusababisha malalamiko ya wananchi.

## TALIRI, NARCO kuendesha kilimo cha malisho

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

TAASISI ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (TALIRI) kwa kushirikiana na NARCO inatarajia kuendesha kilimo cha malisho kitakacholimwa kwa njia ya umwagiliaji.

Katika ushirikiano huo ekari 5,000 zitatumika kunenepesha mbuzi katika eneo la Kongwa.

Mkurugenzi Mkuu wa TALIRI, Prof. Eric Komba, aliyasema hayo jana jijini hapa kwenye hafla ya makabidhiano ya kituo atamizi cha vijana cha ufugaji mbuzi kibiashara kilichojengwa kwa ufadhili wa Serikali ya Denmark kupitia Mfuko Binafsi wa Kusaidia Wakulima (PASS TRUST).

"Leo tunapopokea kituo hiki, TALIRI tayari tumeweka mpango wa matumizi kwa kupitia mkopo kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) tumejipanga kutoa mafunzo kwa vijana 200 kwa mwaka katika nyanja za unenepeshaji na biashara ya mbuzi, kilimo cha malisho na vyakula vya mifugo na eneo hili la Kongwa kwa kushirikiana na wenzetu wa NARCO tunatarajia kuendesha kilimo cha malisho na ekari 5,000 zitalimwa na kuwekewa miundombinu ya umwagiliaji na pia ekari 5,000 zitatumika kwa kazi ya unenepeshaji wa mbuzi," alisema.

Alisema vijana watakaopata mafunzo katika kituo hicho, watanufaika na kujiajiri, kufuga kibiashara, kufuga kisasa bila kuhama hama.





# Majaliwa ashtukia mchezo mchafu mnada wa kakao

**Na Nebart Msokwa,** KYELA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ameshtukia mchezo mchafu unaofanywa na wasimamizi wa mnada wa kakao wakati wa ushindanishaji wa wanunuzi wilayani Kyela mkoani Mbeya.

Akiwa wilayani Kyela, Majaliwa alishuhudia wasimamizi wa mnada huo wakishindanisha wanunuzi wawili pekee kwa njia ya mtandao. Alibaini hali hiyo jana kwenye mnada uliofanyika katika ghala la chama kikuu cha wakulima wa kakao katika Kata ya Ipinda.

Hata alipohoji kuhusu idadi hiyo ya wanunuzi kushindanishwa alijibiwa kuwa wengine walishindwa kuingia kwa sababu ya mtandao.

Kutokana na hali hiyo, aliagiza wasimamizi wa mfumo huo wa uuzwaji wa kakao kwa njia ya mnada kuhakikisha wanauendesha kwa uwazi, ili kuongeza idadi ya wanunuzi watakaoshindana na kupata bei ambayo itawanufaisha wakulima.

"Hapa toka mmeanza wanaonekana wanunuzi wawili pekee ndiyo wanashindana, sasa kwanini msiwaite hao wanunuzi hapa washindane kwa uwazi? Kama shida ni mtandao kwanini msiweke wazi ili na hao wanunuzi wengine wajiunge nayo?" Alihohi Majaliwa.

Vilevile, aliwataka viongozi wa serikali, vyama vya ushirika pamoja na wananchi kushirikiana kuwadhibiti walanguzi wa kakao maarufu kwa jina la 'Njemke' ambao wamekuwa wakiwalangua wananchi zao hilo na kuharibu soko.

Pia, aliwataka viongozi wa serikali katika Wilaya ya Kyela kuhakikisha wanawatembelea wakulima kwenye maeneo yao kwa lengo la kutoa elimu ya kilimo bora cha zao hilo pamoja na faida ya kuuza mazao yao kupitia mfumo wa stakabadhi ghalani.

"Lakini naagiza AMCOS zote na chama kikuu cha wakulima wa kakao kuwa na mashamba darasa kwa ajili ya kuwafundishia wakulima mbinu bora za uzalishaji wa zao hili," aliagiza Wzairi Majaliwa.

Naibu Waziri wa Kilimo, David Silinde alisema wizara hiyo inakusudia kuanzisha vitalu vya kuzalishia miche ya kisasa ya kakao katika Wilaya ya Kyela na kuigawa bure kwa wakulima ili kuongeza tija uzalishaji wa zao hilo.

Alisema wanachohitaji ni eneo kwa ajili ya kuanzisha vitalu hivyo na kwamba suala la upatikanaji wa fedha ni jukumu la wizara hiyo na hivyo akaiomba Halmashauri ya Kyela kuandaa eneo hilo. Alisema pia wanakusudia kuongeza uzalishaji wa miche na kuigawa bure kutoka 34,000 ya sasa mpaka miche 100,000 hali ambayo alisema itawasaidia wananchi kuhamasika kuzalisha zao hilo.

Alisema pia wanapambana kuimarisha uzalishaji wa zao hilo kutokana na sekta ya kilimo kuwa sekta inayoongoza kwa uzalishaji wa ajira nchini kwa maelezo kuwa inaajiri zaidi ya asilimia 65 ya wananchi.

"Lakini pia tumeielekeza Taasisi ya Utafiti wa Kilimo (TARI) kuja huku kufanya utafiti ili kubaini magonjwa na wadudu wanaoshambulia kakao na namna ya kukabiliana nayo na tunasisiziza kama zitatumika dawa basi ziwe za asili," alisema Silinde.

Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe, alisema wanaendelea kusimamia mfumo wa uuzaji wa kakao kupitia mfumo wa stakabadhi ghalani kwa kuhakikisha wanatatua kero zinazoukabili.

Alisema kutokana na mfumo huo kutumika bei ya zao hilo imepanda kutoka Sh. 2,500 kwa kilo kabla ya kuanza mfumo huo mpaka Sh. 32,000 kwa kilo.

## Polisi waomba ushirikiano na w'biashara kuzuia uhalifu

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

JESHI la Polisi mkoani Mbeya, limewataka wafanyabiashara wa masoko mbalimbali kushirikiana na jeshi hilo kuzuia, kudhibiti na kutokomeza uhalifu katika maeneo ya biashara zao na makazi.

Mkuu wa Operesheni wa jeshi hilo, Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi (SACP), Abdi Issango, aliyasema hayo wakati akizungumza kwenye kikao na viongozi na wafanyabiashara wa Soko Kuu la Mwanjelwa.

Kamanda Issango alisema jeshi hilo linathamini mchango unaotolewa na wafanyabiashara, hivyo litaendelea kuhakikisha ulinzi na usalama unaimarishwa katika maeneo yao ya biashara ili kukuza uchumi wa mtu mmoja mmoja na mkoa.

Hivyo, aliwataka wafanyabiashara hao kuweka ulinzi wa kidigitali kwa kuhakikisha wanafunga kamera za usalama kwenye maduka yao ili kuzuia uhalifu na unapotokea kurahisisha kazi ya upelelezi.

"Ulinzi wa mali zako unaanza na wewe mwenyewe, sasa kwenye haya maeneo yenu ya biashara ni vema sana mkafunga kamera ili zisaidie inapotokea uhalifu, mkifanya hivyo mnatusaidia hata sisi kurahisisha kazi," alisema Kamanda Isango.

Mkuu wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi wa Polisi (ACP), Andrew Kantimbo, aliwataka wafanyabiashara wa Soko Kuu la Mwanjelwa kutoa ushirikiano kwa Jeshi la Polisi kwa kwenda kutoa ushahidi mahakamani inapotokea uhalifu.



Wawindaji jamii ya Wahadzabe wakishirikiana kuandaa kitoweo walichowinda katika pori lililoko karibu na Ziwa Eyasi mkoani Arusha hivi karibuni. **PICHA:JAMES LANKA**

# Rais Samia kutoa tuzo maalumu kwa wizara, mikoa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

RAIS Samia Suluhu Hassan anatarajiwa kutoa tuzo maalumu kwa wizara na mikoa itakayofanya vizuri kwenye uboreshaji wa mazingira ya biashara, kukuza uwekezaji na uchumi nchini.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Baraza la Biashara la Taifa (TNBC), Godwil Wanga, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki jijini Mbeya kwenye mkutano kati ya sekta ya umma na sekta binafsi uliokuwa na lengo la kujadiliana namna ya kutatua kero zinazowakabili wafanyabiashara.

Alisema tuzo hiyo itaanza kutolewa Mei 29 mwaka huu kwenye mkutano wa taifa wa majadiliano kati ya sekta ya umma na sekta binafsi, ambao utafanyika jijini Dar es Salaam.

Alisema vimeandaliwa vigezo mbalimbali ambavyo ndivyo vitatumika kuwapata washindi wa tuzo hiyo ambayo inaitwa 'Tuzo ya Rais' ambayo alisema imeandaliwa mahsusi kwa lengo la kuhamasisha utendaji kazi.

Pia alisema kigezo cha kwanza kitakachotumika kumpata mshindi ni uongozi katika utatuzi wa kero za wafanyabiashara, kuimarisha mazingira ya biashara na uchumi endelevu na kukuza uhusiano kati ya sekta ya umma na sekta binafsi kupitia majadiliano.

Kigezo cha pili alikitaja ni kupungua kwa gharama za kuanzisha ama kuhuisha biashara kwa mujibu wa taratibu zilizopo kwenye biashara husika.

Kigezo kingine ni kupungua kwa gharama za kukidhi matakwa ya sheria na kanuni za biashara pamoja na muda unaopotea wakati wa ufuatiliaji na uendeshaji wa shughuli hizo.

Alitaja kigezo kingine ni mwelekeo na msimamo wa kisera na kimkakati kuhusu kuboresha mazingira ya biashara ili kukuza uwekezaji na uchumi kupitia maendeleo ya sekta binafsi.

"Lakini pia lazima kuwapo na sera, mikakati na mafunzo ya kuendeleza wafanyabiashara na wafanyakazi katika sekta binafsi, kuwepo kwa ufanisi wa kitaasisi na taratibu za kisheria kwenye utatuzi wa migogoro," alisema Wanga.

Vilevile alisema lazima kuwepo na urahisi wa kupata ardhi kwa ajili ya uwekezaji na maeneo salama ya kufanyia biashara pamoja na kupungua kwa gharama zisizo rasmi za kibiashara, ikiwamo rushwa na makato yasiyokuwa na ulazima.

Kigezo cha mwisho ni uwazi na utoaji wa taarifa za maboresho ya mazingira ya biashara na uchumi katika eneo husika na nchini kwa ujumla.

Waziri wa Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu Kijaji, alisema Rais Samia amekuwa akiongoza kwenye uhamasishaji wa ukuaji wa biashara na uwekezaji nchini kwa kuhakikisha kunakuwa na uhusiano mzuri kati ya sekta binafsi na sekta ya umma.



## Jamii yatakiwa kuondoa utofauti jinsia katika elimu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

OFISA Elimu wa Wilaya ya Kusini Unguja, Mussa Nahoda Makame, amesema elimu ya jinsia ni msingi wa kujenga jamii jumuishi kwa wanafunzi wa kike na kiume bila ya kujali utofauti wa jinsia zao.

Aliyasema hayo jana wakati akifunga mafunzo ya jinsia yaliyotolewa na shirika linalotekeleza mradi wa kutengeneza mazingira safi kwa watoto wa kike (KFHI) chini ya ufadhili wa KOICA, kwa wazee wa wanafunzi wa Shule ya Mtule huko Kitogani Mkoa wa Kusini Unguja.

Alisema katika kufikia malengo ya usawa kwa watoto wa kike kukamilisha ndoto zao za kupata elimu lazima jamii ibadilishe mtazamo wa kumwona mtoto wa kike ni dhaifu dhidi ya mtoto wa kiume.

Alisema wazazi na jamii wanatakiwa kufahamu kuwa suala la kupata elimu kwa watoto halina ubaguzi wa aina yoyote.

Makame alisema kuwa ni ukweli usio pingika kuwa mtoto wa kike anakumbana na changamoto mbalimbali wakati anapotafuta elimu ikiwamo ya kutumikishwa kazi za nyumbani.

Alisema wazazi majukumu yao kwa sasa ni kuhakikisha wanatokomeza mila potofu ambazo zinamkandamiza mtoto wa kike katika kupata haki yake ya msingi ikiwamo kupata elimu ili kuwawezesha kuwa viongozi wazuri wa baadaye.

Makame alisema kwa vile wazazi hao wameshapatiwa mafunzo hayo ni vizuri kuwa mabalozi kwa jamii na wazazi wenzao katika kufukia ndoto ya mtoto wa kike ikiwamo kumwondolea vikwazo vya kupata elimu.

Alisema kuwa licha ya serikali na taasisi mbalimbali kufanya kazi kubwa ya kuelimisha umma juu ya kumpunguzia majukumu mtoto wakike, lakini bado kuna badhi ya wazazi wanaendelea kufanya hivyo.

Meneja wa Shirika la KFHI, Taewan Park alisema wanaunga mkono juhudi zote zinazochukuliwa na Serikali ya Zanzibar katika kuhakikisha mtoto wa kike anasoma bila ya changamoto yoyote.

Alisema katika kuunga mkono hilo ndiyo maana shirika hilo likaanzisha mafunzo hayo kwa wanafunzi na wazazi wa wanafunzi ili kuona watoto hao wapo salama na kutobaguliwa kijinsia.

Ofisa Jinsia, Udhalilishaji, Ukimwi na dawa za kulevya kutoka Wizara ya Elimu, Riziki Mhammed Juma, alisema wazazi wanajukumu kubwa katika kumlea mtoto wa kike katika maadili mazuri.

Alisema familia nyingi zinamtazamo finyu wa kumuona mtoto wa kike hana haki ya kupata elimu wala kusikilizwa ndani ya jamii wakati mtazamo huo umeshapitwa na wakati kwa sasa.

# Ubinafsishaji wa Bandari ya Malindi waanza kuzaa matunda

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Mawasiliano na Uchukuzi Zanzibar, Dk. Khalid Mohammed Salum, amesema hatua ya serikali kukabidhi shughuli za uendeshaji wa Bandari ya Malindi kwa Kampuni ya Ufaransa ya Global Logistics Ltd umeanza kulipa.

Amesema kampuni hiyo imetoa gawio la Sh. bilioni 10, pamoja na kuleta vifaa vya kisasa kwa ajili ya kuongeza kasi ya ufanyaji kazi katika bandari hiyo.

Alitoa kauli hiyo wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mafanikio yaliyopatikana kutokana na uwekezaji huo, sambamba na kutolea ufafanuzi juu ya upotoshaji wa taarifa kwamba mapato kwenye bandari hiyo yameshuka kwa asilimia 95.

Alisema muda mfupi baada ya uendeshaji wa Bandari ya Malindi kukabidhiwa kwa Kampuni ya AGL, ufanisi umeongezeka ikiwamo udhibiti wa mapato ambayo yameongezeka kwa asilimia 17.

Alisema pia kumekuwapo na udhibiti wa uingiaji na utokaji holela wa mizigo, huku usalama wa bandari ukiwa mkubwa kinyume na ilivyokuwa kabla ya uwekezaji.

"Lakini pia kulikuwa na ufinyu wa nafasi na sasa hali ipo tofauti na hata ushushaji wa makontena umekuwa wa ufanisi zaidi," alieleza Dk. Khalid.

Alisema awali meli zililazimika kusubiri kwa siku 30 hadi 42, ambapo kwa sasa zinakaa kwa siku 15 na ushushaji wa makontena ukichukua si zaidi ya siku mbili.

"Meli nyengine zilikuwa zikishusha makontena Bandari ya Dar es Salaam na hata Mombasa kutokana na ugumu uliokuwapo. Sasa hali haipo hivyo," alisema Dk. Khalid.

Alisema mbali na mafanikio hayo, AGL imeendelea na wafanyakazi wote 392 waliokuwa wakifanyakazi sambamba na kuongeza ajira nyingine 40 mpya kwa ajili ya kuongeza ufanisi.

Akizungumzia juu ya maendeleo ya ujenzi wa bandari nyingine, alisema mipango inakwenda vizuri kwa ajili ya Bandari ya Mangapwani, Fumba, Mpigaduri na Shumba Vyamboni.

Alisema, serikali pia inakusudia kuziimarisha bandari za mkoani Wete, Pemba ambapo kwa sasa imeanza kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa bandari hizo.



Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Muheza, mkoani Tanga, Serapion Bashange, akifungua mafunzo juzi yalioandaliwa na Shirika Lisilo la Kiserikali la CAMFED Tanzania yaliyohusisha maofisa elimu kata, wakuu wa shule na walimu yaliyoendeshwa kwa siku mbili. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Mkutano 15 Baraza la Wawakilishi kuanza kesho

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKUTANO wa 15 wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar wa Bajeti ya Mwaka 2024/2025, unatarajiwa kuanza kesho visiwani hapa.

Akitoa taarifa kwa vyombo vya habari jana katika ukumbi wa Baraza la Wawakilishi Chukwani, Mkurugenzi wa shughuli za Baraza la Wawakilishi, Othman Ali Haji alisema kuwa kazi kubwa ya kikao hicho itakuwa ni kujadili makadirio na matumizi ya bajeti ya serikali kwa wizara zote na bajeti kuu.

Alisema katika mkutano huo maswali 291 yatajadiliwa na kujibiwa ili kupatiwa ufumbuzi wake.

Aidha, alisema kikao hicho pia kitahusisha miswada miwili ya sheria itakayowasilishwa na kujadiliwa na mswada mmoja uliyosomwa kwa mara ya kwanza katika Mkutano wa 14, utajadiliwa katika mkutano huo.

Alisema kikao hicho pia kutakuwa na Muswada wa Sheria ya Fedha. Muswada wa Sheria ya Kuidhinisha Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2013 hadi 2024 na Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali na kuweka masharti bora ndani yake.

Alisema vile vile mkutano huo utakuwa wa marekebisho ya Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi la Zanzibar Toleo la 2020.

Pia, alisema serikali kupitia Wizara ya Fedha inatoa mafunzo kwa wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ili kuwaongezea ujuzi wa utekelezaji wa majukumu yao.

# CAG: Vigogo serikalini wananiingilia kiutendaji

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**



MDHIBITI na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) Zanzibar, Dk. Othman Abasi Ali (pichani), amesema anaingiliwa kiutendaji na baadhi ya viongozi wa juu serikalini.

Kutokana na taarifa hiyo, Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi ameonya kuwa taasisi hiyo haipaswi kuingiliwa na kiongozi yoyote, bali inapaswa kuwa huru, hivyo viongozi wenye tabia hiyo waache mara moja.

Akikabidhi kwa Rais Dk. Mwinyi ripoti yake ya ukaguzi wa hesabu za serikali kwa mwaka 2022/23 jana visiwani hapa, CAG Othman, pamoja na mambo mengine, alieleza kero hiyo ya kuingiliwa kiutendaji kunakofanywa na “viongozi wa juu serikalini”.

CAG alisema anasikitishwa na kitendo cha baadhi ya wateule wa Rais kuingilia majukumu yake na baadhi yao kutoa vitisho dhidi ya watendaji wa ofisi yake.

Kutokana na kauli hiyo, Rais Dk. Mwinyi alimtaka CAG kuwasilisha majina ya wateule wake ambao wanaingilia majukumu ya taasisi hiyo na wateule hao na viongozi hao wanapaswa kujua kuwa kuwapo taasisi hiyo ni kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar na imepewa majukumu kisheria na mamlaka kamili.

“Niwatake wote ambao hawajatajwa majina yao, lakini CAG anawajua wana tabia ya kuingilia taasisi hii kuacha mara moja, na ningependa nimtake CAG niletee majina ya watendaji hao na mimi niwajue,” Rais aliagiza.

Rais Dk. Mwinyi pia alimtaka Katibu Mkuu kiongozi kuunda kamati maalum ya kuzifanyia kazi kasoro za kiutendaji zilizowasilishwa na CAG.

Alisema kuwa mbali na upungufu uliobainishwa katika ripoti hiyo, kuna tatizo la baadhi ya taasisi za serikali kuingia katika mikataba ya utekelezaji miradi bila ya kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, jambo ambalo ni kinyume na sheria.

“Ninapenda nisisitize kwamba mikataba yote ya serikali lazima ihusishe Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na maelekezo yake yazingatiwe na kutofanya hivyo ni kosa kisheria,” alionya.

Rais alisema pia bado kuna changamoto kubwa kwenye miradi ya maendeleo, hivyo ni vyema kupata utaratibu maalum wa kupata maoni kutoka katika kamati na kuishirikisha Ofisi ya CAG na pale ambapo hakuna maelezo, lazima hatua za kinidhamu na kijinai zichukuliwe.

Kuhusu mashirika ya umma yanayosuasua, Dk. Mwinyi alisema serikali inaangalia namna ya kuyaondoa yasiyoweza kujiendesha kuliko kuendelea kutengeneza hasara.

Rais, akizungumzia ukusanyaji mapato alisema umeimarika na kufikia asilimia 96, akitaja ni mafanikio makubwa, ingawa bado kuna taasisi chache ambazo hazijajiunga katika mfumo wa ukusanyaji mapato kwa mifumo ya kidigiti.

“Hii nayo ni faraja nidhamu ya matumizi imeimarika, haya ninayasema kwa sababu kwenye ripoti hayajaelezewa kwa kina na ununuzi wa umma umeimarika kwa mujibu wa ripoti ya CAG licha ya kuwapo dosari chache,” alisema.

Dk. Mwinyi alisema anahitaji kupatiwa kwa undani ni waziri gani ambaye anaingilia utaratibu wa ununuzi. Awali CAG alieleza masikitiko yake hayo kwa baadhi ya mawaziri kuingilia utaratibu wa ununuzi, jambo ambalo ni kosa kisheria.

Awali, akisoma ripoti hiyo CAG Dk. Othman alisema kuna dosari nyingi katika mifumo ya ulipaji kodi kwa njia ya kieletroniki kwa kuwa na malipo yasiyo na tija kwenye utekelezaji miradi ya TEHAMA yenye thamani ya Sh. bilioni 23.76.

CAG alisema kwamba miongoni mwa dosari kubwa katika usimamizi wa fedha za umma ni baadhi ya wateule wa Rais kuendelea kutumia mafuta ya uendeshaji kazi za taasisi zao kwa matumizi yao binafsi huku serikali ikiendelea kuwalipa fedha maalum za ununuzi wa mafuta kwenye mishahara yao, jambo ambalo linarudisha nyuma juhudi za serikali katika kufikia malengo.

CAG huyo pia alisema hofu ya Uchaguzi Mkuu wa mwakani imeanza kutanda kwa wanasiasa walio wengi visiwani humo, wakiwa na dhana potofu kuwa CAG anataka kuingia katika nafasi za kisiasa hasa pale hivi karibuni alipokwenda Dodoma kukutana na CAG mwenzake, Charles Kichere.


## TANGAZO LA MNADA

**Arm ,Crisam, Dar state, Freemind, Marmboto, Raissa, Workethic** Kwa idhini tuliyopewa na **FANIKIWA MICROFINANCE COMPANY** tunapenda kuutarifu umma kuwa Tutafanya Jijini Dar es salaam na Mteja anashauriwa kulipa deni ndani ya siku 14 kutoka ya hili Tangazo vinginevyo Mnada utaendelea kama Tarehe ya Mnada inavyoonekana hapa chini.

| | Jina la Mdaiwa | Dhamana | Tarehe ya Mnada |
|---|---|---|---|
| 1 | George Jackson Msowoya | Toyota Corolla T998DMT | 28.05.2024 |
| 2 | Kihiri Mboyi Juma | Subaru forester T986 EBJ | 28.05.2024 |
| 3 | James Mmanyi Gikene | Mercedes Benz T915 BAQ | 28.05.2024 |
| 4 | PAUL MIZZAH CHARES | Subaru Forester ,T538EBB | 28.05.2024 |
| 5 | Raphael Costantine Bandiho | Toyota Land cruiser T578 AVX | 28.05.2024 |
| 6 | Baraka Nyang'anyi Marela | Toyota Passo T698DWD | 28.05.2024 |
| 7 | Samson Alphonce Mushi | Mercedes Benz T192 CBV | 28.05.2024 |
| 8 | John Mathias Mushi | Toyota Mark x T909DKU | 28.05.2024 |
| 9 | Abdulaziz Mikidadi Juma | Toyota Carina T485 ADA | 28.05.2024 |
| 10 | Salmin kasimu Maengo | LandRover sports T917CMW | 28.05.2024 |

**Masharti ya Mnada.**
1. Mnunuzi atakeyeshinda atalipa 25% (au Zaidi) ya bei iliyofikwa kwenye mnada na salio la (75%) litalipwa ndani ya siku kumi nne(14) kuanzia tarehe ya mnada.
2. Endapo mnunuzi atashindwa kulipa salio kwa mda uliotolewa atakuwa amepoteza haki zote na mali itauzwa upya.
3. Ukaguzi unaruhusiwa kuanzia tarehe yaTangazo.

**Kwa Mawasiliano Piga 0677014355 (Fanikiwa)**



## KUPOTEA KWA CHETI



**FRANK FROLENS WIKESY,** Anatangaza kupotelewa na cheti chake cha kidato cha Nne chenye **Index no S1327-0149,** Kilichotolewa na baraza la Mitihani la Taifa kupitia shule ya Sekondari Mazoezi Klerruu Mwaka 2018. Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo cha Polisi. TAARIFA YA POLISI: **PHQ/DOD/DOD/17511/2024**



## KUPOTEA KWA PASSPORT



**SHAMSA SALIM JUMA** anatangaza kupotelewa na hati ya kusafiria 'PASSPORT' yenye namba **TAE380552,** iliyotolewa na Wizara ya Mambo ya Ndani Januari 18 mwaka 2021 na kuisha muda wa matumizi Januari 17 mwaka 2031, Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote Cha polisi kilichopo karibu nae. TAARIFA YA POLISI: **LUSH/PS/B.I/29/749/2024**



## KUPOTEA KWA CHETI



**BEATRICE SAMWEL NTULILA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S4969/0009** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **QUEEN OF PEACE SEC SCHOOL** mwaka 2016. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/TEM/86337/2024.**



## KADI YA GARI IMEPOTEA

**LENNIE MWAMPETA HOLM** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NO YA USAJILI **T592 AMV.** CHASSIS NO: **SALLDHMC7BA248316.** ENGINE NO: **11L17938A.** YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI: **PHQ/ARU/ARU/ 14773/2024.**



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA TANZANIA

Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya DODOMA MJINI

Kituo cha MAKOLE Mkoa DODOMA

Usimamizi wa mirathi Na.32/2024

KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU CLEOPHACE BUHELE MTOBI

KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA KAMALAMO CLEOPHACE MTOBI

**TANGAZO**
(Kanuniya 5(2) ya Kanuniza Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya Marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 23 Mwezi 05 Mwaka 2024 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Zingatia;
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
Imetolewa leo Tarehe 06 Mwezi 05 Mwaka 2024.



## KUPOTEA KWA KADI ZA PIKIPIKI

**DENIS KASINJA RUTTA** anatangaza kupotelewa na kadi za pikipiki zenye namba za usajili **MC 575 DHA – BOXER, MC 526 DBE – BOXER, MC 809 BEF – BOXER na MC 341 DEG – BOXER.** Yeyote atakayeziona atoe taarifa kituo chochote che polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/ILA/85769/2024.**



## KUPOTEA KWA KADI ZA PIKIPIKI

**DENIS KASINJA RUTTA** anatangaza kupotelewa na kadi za pikipiki zenye namba za usajili **MC 893 CKW – TVS, MC 818 CUR – BOXER, MC 410 CUR BOXER, MC 650 CXC – BOXER na MC 871 CXR** – BOXER. Yeyote atakayeziona atoe taarifa kituo chochote che polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/ILA/85769/2024.**



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA TANZANIA

Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya DODOMA MJINI

Kituo cha CHAMWINO Mkoa DODOMA

Usimamizi wa mirathi Na.16/2024

KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU WILLIAM KISESEGELE wa MSALATO

KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA BERNADETA MPUNGA

**TANGAZO**
(Kanuniya 5(2) ya Kanuniza Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya Marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 27 Mwezi 05 Mwaka 2024 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Zingatia;
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
Imetolewa leo Tarehe 10 Mwezi 05 Mwaka 2024.



JAMHURI YA MUUNGANO TANZANIA
KUITWA SHAURINI MDAIWA
(MCA)

Mahakama ya mwanzo ya............................ARUSHA MJINI
Wilaya ya ARUSHA

TALAKA NAMBARI 24 YA 2024

Mdai PENDO JOHN KISIOKI

Amdai

Mdaiwa ........................................HEZRON ZABLON MUNISI

Kwa ............................HEZRON ZABLON MUNISI WA MWANZA

Kwa kuwa Mdai/Wadai ameleta/wameleta madai yake/yao kwamba (Elez a hapa habari za madai): FIKA MAHAKAMANI BILA KUKOSA KUJIBU MADAI YA TALAKA MGAWANYO WA MALI NA MATUNZO YA WATOTO.

Kwa hiyo unahitajiwa/mnahitajiwa kuhudhuria mahakama hii siku ya JUMATATU tarehe 27/5/2024 saa 2:30 asubuhi kwa kujibu madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kukatwa shauri hilo ni lazima kuleta mashahidi wako/wenu na hati zote zinazohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea katika shaur i hilo.
Angalia kama hukuhudhuria/hamkuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu mahakama ikithibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa shaurini hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa /mmeshindwa. Hati hii ya tolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 29/4/2024
Hakimu/Hakimu Mkazi/Mahakama ya Mwanzo

# 'Ole wake atakayempa ujauzito mwanafunzi'

**Na Mwandishi Wetu, KYELA**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa amekemea kadhia ya kuharibu ndoto za watoto wa kike kwa kuwapa ujauzito wakiwa wanafunzi, akionya kuwa „jela inawaita kwa miaka 30".

Alikemea hilo juzi alipokagua ujenzi wa Shule mpya ya Sekondari ya Wasichana ya Mkoa wa Mbeya (Mbeya Girls) na kuweka jiwe la msingi kwenye shule hiyo.

Akizungumza na wakazi wa Kata ya Busale, Halmashauri ya Wilaya ya Kyela, Waziri Mkuu alisema ujenzi wa shule hiyo ni utekelezaji uamuzi wa serikali baada ya kubaini kuwa watoto wengi wa kike hawafanyi vizuri kwenye masomo ya sayansi.

"Shule hizi za wasichana zilianza kujengwa kwa sababu tumegundua kuwa tuna idadi ndogo sana ya watoto wa kike ambao wanasoma masomo ya sayansi. Kwa hiyo, kila mkoa ulipatiwa fedha kwa ajili ya shule hizi," alisema.

Majaliwa alisema Rais Samia Suluhu Hassan analinda watoto wote, hasa watoto wa kike na akatumia fursa hiyo kuonya vijana wasijaribu kukatisha ndoto za watoto hao kwa kuwaharibia masomo yao.

Alitaka vijana wakae mbali na watoto wa kike, akionya kuwa wakizima ndoto zao kwa kuwapa mimba na kuwakatisha masomo, wataishia jela ambako kifungo chake ni miaka 30.

"Ole wenu vijana, ole wenu mharibu au mkatize ndoto ya mtoto wa kike. Yeyote atakayehusika kukatiza ndoto ya mtoto wa kike, kwanza ujiulize una miaka mingapi halafu ujumlishe na miaka 30," alisema.

Akitoa taarifa ya ujenzi wa mradi huo, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kyela, Flora Luhala alisema Mei 2023, walipokea Sh. bilioni tatu kutoka Serikali Kuu kwa ajili ya ujenzi wa shule hiyo chini ya mradi wa SEQUIP.

Alisema utekelezaji wa mradi umefikia asilimia 80 na hadi kukamilika kwake utakuwa na jengo moja la utawala, madarasa 12, matundu ya vyoo 16, maabara nne, bwalo moja, jengo moja la huduma ya kwanza, mabweni manane na nyumba mbili za walimu.

Waziri Mkuu pia alisema serikali imeendelea na mpango wa kuboresha huduma za afya kwa kujenga miundombinu kuanzia ngazi ya kanda, mkoa, wilaya, halmashauri hadi kata.

"Dhamira ya Rais Samia ni kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora za afya katika maeneo yao," alisema na kuongeza kuwa pamoja na maboresho ya miundombinu, serikali pia itaendelea kuajiri watoa huduma na wataalamu wa sekta ya afya.

Waziri Mkuu pia aliweka jiwe la msingi kwenye jengo la Mama na Mtoto katika Hospitali ya Wilaya ya Kyela. Huko alielezwa kuwa jengo hilo ambalo ujenzi wake umefikia asilimia 85, hivi sasa liko kwenye hatua ya ukamilishaji ikiwamo kupiga plasta.

Kazi zingine zinazofanyika ni uwekaji fremu za vioo na madirisha, uwekaji marumaru, mifumo ya TEHAMA, umaliziaji mfumo wa maji safi na maji taka na uwekaji wa taa pamoja na viyoyozi.



Wapalestina wakiendelea kukimbia mji wa kusini mwa Ukanda wa Gaza, Rafah, baada ya operesheni ya kijeshi ya Israel kuanza juzi. **PICHA: MTANDAO**

# Israel yapuuzia wito kusitisha vita

**JERUSALEM, Israel**

JESHI la Israel limepuuza wito wa mataifa mbalimbali ikiwamo Marekani kuhusu kusitisha mashambulizi yake dhidi ya mji wa Rafah katika mpaka wa kusini wa Gaza, huku idadi ya Wapalestina waliouawa ikiongezeka na kukiwa hakuna dalili ya kupatikana kwa makubaliano ya amani.

Ilibainishwa jana kwamba, anga la Gaza lilikuwa limetanda moshi kutokana na mashambulizi ya mabomu na mizinga yaliyofanywa na Jeshi la Israel, wakati likijaribu kujipenyeza ndani ya mji wa kusini wa Rafah.

Msemaji wa Serikali ya Israel, Daniel Hagari, alisema kinachofanyika ni operesheni maalum inayowalazimu wakimbizi wa ndani wa Kipalestina kukimbia huku na kule kutoka kwenye eneo hilo ambalo awali walilitumia kama hifadhi yao.

Jeshi la Israel linadai kuwa mji huo ulio mpakani mwa Gaza na Misri ni ngome ya mwisho ya wapiganaji wa Kipalestina na kwamba lazima likamilishe operesheni yake ya kuwamaliza wapiganaji hao na kuwakomboa mateka waliosalia mikononi mwao.

Aidha, ilielezwa kuwa siku chache zilizopita jeshi hilo lilivamia kitongoji cha Zaitun ambako lilidai kuwaua wapiganaji kadhaa wa Kipalestina.

Ilibainishwa kuwa Wapalestina takribani 300,000 kati ya raia milioni 1.3 wanaojihifadhi huko, wamesha ukimbia mji huo kutokana na amri iliyotolewa na Israel.

Mmoja kati ya wakimbizi hao, Ummi Juma alisema "Hatujuwi wapi tuelekee. Tumekuwa tukikimbia kutoka mahala pamoja kwenda kwengine, na sasa tumeondoka Rafah, lakini hatujui twende wapi. Tunakimbia kimbia tu mitaani. Nimeona kwa macho yangu vifaru na matingatinga ya majeshi ya Israel. Yapo mitaani".

Ilielezwa kuwa jeshi la Israel pia liliushambulia upande wa kaskazini katika kambi ya Jabalia, ambako wapiganaji wa Hamas wamejikusanya tena kwenye maeneo ambayo jeshi hilo liliwahi kudai kuwa lilishayasafisha miezi kadhaa iliyopita, huku likisema liliwaua pia wapiganaji kadhaa wa Kipalestina kwenye operesheni hiyo.

Hamas, ilisema kwamba wapiganaji wake walishambuliana na jeshi la Israel kwenye upande wa mashariki wa kambi hiyo ya Jabalia.

Video iliyotolewa na tawi la kijeshi la kundi hilo, al-Qassam Brigades, ilionesha wapiganaji wake wakirusha droni iliyodondosha mabomu kwenye kifaru cha Israel karibu na kambi hiyo.

Taarifa ya al-Quds, ambalo ni tawi la kijeshi la Islamic Jihad, ilisema kwamba wapiganaji wao walipambana na wanajeshi wa Israel mashariki mwa mji wa Rafah.

Israel inasema imeshawaua wanamgambo 13,000 hadi sasa, ingawa haijatowa ushahidi wowote.

**DW**

## Manispaa yaanza uboreshaji sanamu la Mwalimu Nyerere

**Na Benny Kingson, TABORA**

MANISPAA ya Tabora inatarajia kuboresha majengo yaliyopo eneo la Sanamu la Mwalimu Julius Nyerere kwa lengo la kuwapatia wajasiriamali wafanye shughuli zao pamoja na kuwa eneo la kivutio.

Mkuu wa Wilaya ya Tabora Mjini, Deudedith Kitwale, aliyasema hayo juzi wakati wa uzinduzi wa kikundi cha wanawake cha tanzanite, kuiagiza manispaa hiyo kufanya marekebisho ya majengo kwenye eneo hilo, ili kuongeza fursa za utalii mkoani hapa.

Kitwale aliitaka Halmashauri ya Manispaa ya Tabora kuhakikisha inatoa eneo hilo kwa wajasiriamali ili wafanye shughuli zao, kuwapa fursa kujitangaza kwa kuwa ni eneo nyeti ambalo litakuwa linatembelewa na watu kujifunza historia ya nchi ilipotokea.

"MKurugenzi kaeni mrekebishe majengo ya eneo hili ambalo ni nyeti na lina historia kubwa sana ya ukombozi wa taifa letu, hapa panastahili pawe na hadhi inayofanana na Hayati Julius Nyerere na ndiyo alama ya nchi," alisisitiza Katwale.

Diwani wa Kata ya Chemchem, Alhaji Amrani Kasongo, alisema tayari wametenga fedha kufanya ujenzi na ukarabati huo ili kuboresha eneo hilo ambalo ni la kihistoria.

Alisema eneo hilo ndilo Hayati Julius Nyerere alitoa hotuba huku akitokwa na machozi wakati akidai uhuru wa nchi kutoka kwa wakoloni.

Alisema pia eneo hilo ndipo palipigwa kura tatu za uamuzi wa busara na kwamba wataweka na maktaba itakayokuwa na vitabu vya kuelezea harakati za ukombozi wa nchi.

Mwenyekiti wa kikundi cha tanzanite, Mwanahamisi Juma, alisema kikundi hicho kinajishughulisha na ushonaji vikapu, mikeka, kutengeneza majiko banifu, kutengeneza batiki, sabuni za kufanyia usafi wa nyumba, vyoo pamoja na kazi nyingine za mikono.

Alisema: "Tulianza na mtaji wa Sh.500,000 kwa kujichangisha wenyewe, tumekuwa tukinunua ukindu wa kutengenezea vikapu na mikeka toka Uganda tunauza na kupata vipato na tulishika nafasi ya tatu kwa kuwa na vikapu na majiko bora, tukiiwakilisha nchi kwenye maonyesho ya kimataifa Ubelgiji."

# SIMBA YATUA KWA KIPA MATAMPI WA COASTAL

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya taarifa za kumpa mkataba wa awali beki wa kati ya Coastal Union, Lameck Lawi, klabu ya Simba imeendelea kuiganda timu hiyo na sasa wanafanya mpango wa kumsajili golikipa Ley Matampi raia wa Jamhuri ya Kidemkokrasi ya Congo, ambapo kama mambo yatakwenda vyema anaweza kuvaa uzi mwekundu msimu ujao.

Habari kutoka ndani ya zinasema Matampi, ameonekana kulivutia benchi la ufundi la timu hiyo pamoja na mabosi wake, hivyo kumuweka kwenye orodha ya wachezaji wanaowahitaji kama itashindikana kumbakisha golikipa wao Ayoub Lakred raia wa Morocco.

Awali klabu hiyo ilikuwa na mpango wa kumsajili kipa Mcameroon, Joseph Fabrice Ondoa ambaye anacheza soka lake nchini Ufaransa katika klabu ya Nimes Olympique inayoshiriki ligi ya National, ambayo ni Ligi Daraja la Pili nchini humo.

"Hakuna uhakika wa moja kwa moja kama Lakred anaweza kubaki au la. Hata kama anataka kubaki, lakini klabu nayo inaweza kuweka masharti ambayo tunaweza kushindwana, kwa hiyo kama ikitokea hatukuelewana, basi mbadala atakuwa ni Matampi, benchi la ufundi na uongozi umeridhishwa na kiwango chake," kilisema chanzo chetu ndani ya klabu hiyo.

Chanzo hicho kinasema tayari mazungumzo yameanza na yeye mwenyewe ameonekana kuvutiwa na ofa, huku klabu ya Simba ikiamini hakutokuwa na kipingamizi chochote kutoka kwenye klabu yake ya Coastal.

Kipa huyo ambaye aliwahi kuidakia timu ya taifa ya DR Congo, anashika nafasi ya pili nyuma ya kipa wa Yanga, Djigui Diarra, kukaa langoni mechi nyingi bila kuruhusu bao, ,clean sheets,' akiwa nazo 12, nyuma ya raia huyo wa Mali ambaye ana ,Clean sheet' 13.

Coastal, ilimsajili kipa huyo kutoka klabu ya Renaissance ya DR Congo, ambapo mbali na klabu hiyo, amezichezea klabu zote kubwa nchini humo, AS Vita, TP Mazembe, na DC Motema Pembe , pia aliwahi kucheza soka la kulipwa nchini Lebanon kwenye klabu ya Al-Ansar.

Meneja Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, amesema ingawa wanatarajia kufanya usajili mkubwa mara tu Ligi Kuu msimu huu itakapomalizika, lakini kwa sasa siyo wakati wa kuzungumzia chochote kuhusu hilo.

"Kwa sasa bado tupo kwenye ligi, hatuzuii tetesi za usajili, lakini ukweli wa kila kitu utabainika pale ligi itakapomalizika, nani atatoka na nani ataingia Simba, ila ukweli kwamba tunataka kufanya usajili mkubwa," alitamba Ahmed.




Mwenyekiti wa Timu ya Bulls, Fatema Haji (mbele kushoto), akiwakabidhi ngao timu ya Bulls ambao waliibuka mabingwa wa mashindano ya 'DarYC Mini' chini ya umri wa miaka 11, yaliyofanyika jijini Dar as Salaam juzi. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Minziro afurahishwa na sare ya Simba

**Na Faustine Feliciane**

KOCHA wa Kagera Sugar, Fred Felix 'Minziro' amesema amefurahishwa na namna wachezaji wake walivyopambana kwenye mchezo wao wa Ligi Kuu juzi dhidi ya Simba na kufanikiwa kuondoka na pointi moja.

Minziro alisema matokeo hayo yataongeza hamasa kwa wachezaji wake kuelekea kwenye mchezo ujao dhidi ya Coastal Union utakaochezwa Mei 21.

Minziro alisema wachezaji wake walifuata malekezo yake kwenye mchezo dhidi ya Simba na kufanikiwa kuwabana wapinzani wao hao wasiondoke na pointi zote tatu.

"Wakati wa mapumziko niliwaambia wachezaji wangu waende wakapambane, tunao huo uwezo wa kupambana, niliwapa na maelekezo mengine ya kifundi na kweli walipambana na kufanikiwa kusawazisha goli," alisema Minziro.

Alisema kwa sasa wanaelekeza nguvu zao kwenye mchezo unaofuata ambao nao watapambana kuhakikisha wanapata matokeo mazuri ili kutoka sehemu walipo sasa kwenye msimamo wa ligi kuu Tanzania Bara.

"Kwa sasa kila mchezo ni mgumu, imebaki michezo michache na kila timu inataka kupambana kupata matokeo mazuri ili kujiweka katika nafasi nzuri kabla ligi haijamalizika, hata mchezo na Coastal Union hatutegemei wepesi, utakuwa mchezo mgumu lakini tutapambana kama tulivyofanya kwa Simba," alisema Minziro.

Matokeo ya juzi yameifanya Coastal Union kufikisha pointi 30 na kushika nafasi ya tisa kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara baada ya kucheza michezo 26 mpaka sasa wakiwa wamebakiza michezo miwili kumaliza ligi.

## Uhamiaji haishikiki netiboli Afrika Mashariki

**Na Shufaa Lyimo**

TIMU ya Uhamiaji imeendelea kuonyesha uwezo mkubwa kwenye mashindano ya netiboli kwa Afrika Mashariki yanayoendelea kwenye Uwanja wa Benjamini Mkapa jijini Dar es Salaam.

Uhamiaji imeshinda michezo yake miwili ambapo ilianza michuano hiyo kwa kuifunga KIUT kwa magoli 60-25 na juzi Jumapili ilifanikiwa kuifunga Warriors kwa magoli 56-21.

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha Mkuu wa Uhamiaji, Winfrida Emmanuel, alisema kuwa siri ya ushindi huo umetokana na juhudi ya kufanya mazoezi pamoja na ushirikiano uliopo katika timu hiyo.

Alisema kuwa malengo yao ni kuhakikisha wanachukua ubingwa wa michuano hiyo na kuliheshimisha Taifa na Idara ya Uhamiaji kwa ujumla.

"Jana (juzi) na leo (jana) tumeanza vyema mashindano haya, huu ni mwendelezo tupo tayari kukutana na yeyote ambaye tutapangiwa kucheza naye kwani tumejipanga vizuri," alisema Winfrida.

Alisema wamefanya maandalizi makubwa kwa ajili ya mashindano hayo na bado wanaendelea kujituma kwenye mazoezi kwa ajili ya kufanya vizuri katika michezo iliyobaki ya michuano hiyo mikubwa katika ukanda wa Afrika Mashariki.

Naye Mwenyekiti wa Chama cha Netiboli Tanzania (CHANETA) Dk. Devotha Marwa, alisema kuna ushindani mkubwa kwenye mashindano hayo kutokana na namna timu zilivyofanya maandalizi yake.

"Tunashuhudia upinzani mkubwa kutoka kwa timu shiriki, kila timu imejiandaa na kwa kweli kila timu inapambana kupata ushindi," alisema Devotha.

Aidha, amewataka wachezaji wanaoshiriki mashindano hayo kucheza kwa nidhamu, umahiri na umakini ili kutoa ushindani na burudani kwa wapenzi wa mchezo huo.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Kamati ya mashindano wa CHANETA, Lucy Silyvester, alisema timu 13 za wanawake na wanaume zinashiriki kutoka Tanzania Bara, Zanzibar, Kenya pamoja na Uganda.

Alibainisha kuwa kati ya timu hizo tisa ni za wanawake na nne za wanaume.

Matokeo mengine kwenye michezo iliyochezwa juzi, JKT ilitoshana nguvu na KVZ kwa kufungana magoli 37-37, NIC ya Uganda iliibuka na ushindi wa magoli 58-22 dhidi ya Zimamoto ya Zanzibar.

Kwa upande wa wanaume, Wob ya Uganda iliibuka na ushindi wa magoli 40-39 dhidi ya ndugu zao Kampala Stars.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### TEN HAG BADO YUPO
KLABU ya Manchester United haina nia ya kumfukuza Kocha Erik ten Hag kabla ya fainali ya Kombe la FA Mei 25. ***(Telegraph)***

### TUCHEL AITAKA MAN UNITED
KOCHA wa Bayern Munich, Thomas Tuchel ana nia ya kuwa kocha wa Manchester United iwapo klabu hiyo itaamua kumfukuza Erik Ten Hag. (Telegraph)

### MOURINHO NAYE AITAKA
KOCHA wa zamani wa Manchester United, Jose Mourinho, angependa kurejea kwa kipindi cha pili lakini klabu hiyo haitaki kumteua tena Mreno huyo mwenye umri wa miaka 61, ambaye alitimuliwa na Roma Januari. ***(Manchester Evening News)***

### MARC GUEHI KUUZWA
KLABU ya Crystal Palace iko tayari kumuuza mlinzi wa England, Marc Guehi mwenye umri wa miaka 23, badala ya kumtoa winga wa Ufaransa Michael Olise mwenye miaka 22, au winga wa Uingereza Eberechi Eze mwenye miaka 25, msimu huu. ***(Givemesport)***

### GASSOVA ATAKIWA
WEST Ham imeanza mazungumzo ya kumsajili winga wa Corinthians mwenye umri wa miaka 19 raia wa Brazil, Wesley Gassova, ambaye analengwa na Liverpool. ***(Standard)***

### BROJA KUUZWA
CHELSEA inatafuta mnunuzi wa mshambuliaji wa Albania, Armando Broja kufuatia kipindi cha mkopo cha mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22 na Fulham. ***(Fabrizio Romano)***

### WILLIAN AWINDWA
CHELSEA ipo kwenye mazungumzo ya kumsajili winga, Estevao Willian mwenye umri wa miaka 17 kutoka Palmeiras . ***(Mail)***


### PICKFORD AWINDWA DARAJANI
CHELSEA pia wamemtambua mlinda mlango wa Everton, Jordan Pickford mwenye umri wa miaka 30 kama wanayemlenga zaidi katika usajili wa majira ya joto. ***(Football Insider)***

### KELLY HUYO NEWCASTLE
KLABU ya Newcastle United imefikia makubaliano ya kumsajili beki wa Bournemouth, Lloyd Kelly mwenye umri wa miaka 25. ***(Foot Mercado)***

### DORTMUND YAMTAKA HALL
MLINZI wa kushoto wa Newcastle United, Lewis Hall mwenye miaka 19, ameibuka kama nyota anayelengwa na Borussia Dortmund msimu wa joto. ***(Givemesport)***

### LAPORTA AMTAKA GREENWOOD
RAIS wa Barcelona, Joan Laporta amewasiliana na Getafe kuhusiana na hali ya mshambuliaji wa Manchester United Mwingereza anayecheza kwa mkopo, Mason Greenwood mwenye umri wa miaka 22. ***(Radio Marca)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




## WESLEY AWINDWA WEST HAM

**Uongozi wa timu hiyo umepanga kukiimarisha kikosi chao baada ya kuthibitisha kuachana na...**

**LONDON, England**

BAADA ya kuthibitisha wataachana na kocha wao kutoka nchini Scotland, David Moyes, mwishoni mwa msimu huu 2023/24, imefahamika kuwa uongozi wa klabu ya West Ham United umepanga kukiimarisha maradufu kikosi chao chini ya benchi jipya la ufundi litakalotangazwa baadaye.

Gazeti la Daily Mail limeripoti kuwa, uongozi wa klabu hiyo umedhamiria kufanya hivyo, ili kuwa na kikosi imara kwa msimu ujao 2024/25.

Mchezaji wa kwanza anayetajwa kuwindwa klabuni hapo kwa mujibu wa gazeti hilo ni kinda kutoka nchini Brazil na klabu ya Corinthians, Wesley Gassova Ribeiro Teixeira 'Wesley'.

Thamani ya mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 19 inatajwa kufikia pauni milioni 21, lakini inadaiwa kuwa tayari uongozi wa Corinthians umeanza kuiwekea ngumu West Ham.

Gazeti hilo limeandika: "West Ham United inajipanga kumsajili kinda wa Klabu ya Corinthians Wesley, kama sehemu ya harakati za klabu hiyo kuimarisha kikosi chake kuelekea msimu ujao 2024/25.

"Mail Sport inaelewa kuwa wawakilishi wa 'The Hammers' walimfuatilia kinda huyo wakati wa mchezo wa ufunguzi wa msimu wa Ligi Kuu ya Brazil 'Serie A' mwezi uliopita ili kujiridhisha.

"Wesley, ambaye anaweza kucheza kama kiungo mshambuliaji ama mshambuliaji wa kati, thamani yake inatajwa kufikia pauni milioni 21 na tayari uongozi wa klabu ya Corinthians umeanza kuiwekea ngumu West Ham.

# Neymar awaahidi raha mashabiki

**RIYADH, Saudia Arabis**

NEYMAR amesema ana hamu kubwa ya kurejea uwanjani baada ya kusherehekea taji la Al Hilal la Saudi Pro League (SPL) na wachezaji wenzake siku ya Jumamosi.

Kikosi cha Jorge Jesus kilifanikiwa kunyakua taji lao la 19 la ligi lililoongeza rekodi siku ya Jumamosi kwa ushindi wa mabao 4-1 dhidi ya Al Hazem na kuwafanya wabaki pointi 12 mbele ya Al Nassr ya Cristiano Ronaldo ikiwa imesalia mechi tatu kumalizika kwa msimu.

Nyota huyo wa Brazil aliahidi furaha msimu ujao huku akiwamwagia sifa wachezaji wenzake.

„Nina furaha sana bila shaka. Kushinda mataji siku zote ni vizuri. Jambo bora zaidi lingekuwa uwanjani, lakini nina furaha sana kwa wachezaji wenzangu," Neymar alisema.

„Niko sawa. Najisikia vizuri. Nina hamu kubwa kurejea uwanjani.

„Kwa bahati mbaya, sijaweza kuwapa furaha wanayostahili lakini unaweza kuwa na uhakika kwamba msimu ujao tutakuwa na furaha nyingi."

Neymar mwenye umri wa miaka 2, alichezea Al Hilal mechi tatu pekee za SPL kabla ya kuumia Oktoba na kufanyiwa upasuaji muda mfupi baadaye.





# HAVERTZ: NITAKUWA SHABIKI MKUBWA WA TOTTENHAM

**LONDON, England**

MSHAMBULIAJI wa Arsenal, Kai Havertz ametangaza kuwa atakuwa ‚shabiki mkubwa' wa wapinzani wao Tottenham Hotspurs ili washikabunduki hao waweze kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu ya England.

Kinyang'anyiro cha kuwania taji hilo kitaenda hadi siku ya mwisho ya msimu baada ya vijana wa Mikel Arteta kushinda 1-0 dhidi ya Manchester United Jumapili na kusonga mbele kwa pointi moja na Manchester City katika nafasi ya pili.

Hata hivyo, City bado wana mchezo mkononi wa kucheza na huo unakuja ugenini kwenye Uwanja wa Tottenham Hotspur leo Jumanne kwenye uwanja ambao wamepoteza mechi zote za Ligi Kuu bila kufunga bao.

Havertz, ambaye alitoa pasi ya bao la ushindi kwa Leandro Trossard kwenye Uwanja wa Old Trafford, aliiambia Sky Sports kwamba anatumaini wapinzani wa Arsenal wa London kaskazini watawafanyia neema.

„Nitakuwa shabiki mkubwa wa Tottenham milele!" Alisema. „Wacha tutegemee bora.

„Lazima tushinde kwani City wanazidi kuweka presha.

„Inapendeza sana kuwa katika mbio za taji na kila wiki lazima ucheze kwa ubora wako. Unapofanya hivyo, unajisikia vizuri zaidi. Tuna mchezo mmoja na tunahitaji klabu nzima nyuma yetu - chochote kinawezekana. „

Tottenham wanaweza kuhitaji ushindi dhidi ya City ili kuweka hai matumaini yao ya kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Iwapo City watatoka sare na Tottenham, watakaa nyuma ya Arsenal kwa tofauti ya mabao pekee.

City watawakaribisha West Ham United siku ya mwisho, huku Arsenal wakiwakaribisha Everton kwenye Uwanja wa Emirates.

# Ten Hag alia na majeruhi Man U

**MANCHESTER, England**

ERIK ten Hag alisema kuiongoza Manchester United ni kama „kuogelea huku mikono nyuma" baada ya ushindi wa 1-0 wa Arsenal kwenye uwanja wa Old Trafford na kuwaweka rekodi ya kushindwa nyumbani kwa mara ya tisa.

Bao la Leandro Trossard katika kipindi cha kwanza liliifanya Arsenal kuwa kileleni mwa jedwali la Ligi Kuu ya England hadi wiki ya mwisho ya msimu huu, lakini waliofika fainali ya Kombe la FA United sasa wameshinda mchezo mmoja tu kati ya tisa za mwisho katika mashindano yote.

Ten Hag kwa mara nyingine alilazimika kumpanga kiungo Casemiro katika nafasi ya kati kwa sababu ya majeraha ya safu ya ulinzi, wakati Bruno Fernandes, Marcus Rashford, Harry Maguire na Mason Mount walikuwa miongoni mwa majeruhi.

Baada ya kutaja matatizo ya majeruhi ya timu kwa msimu mbaya wa klabu, kocha huyo wa zamani wa Ajax, alisema kazi yake imekuwa ngumu zaidi.

„Kocha yeyote anaweza kufanya kitu bora zaidi, lakini niko hapa kwa miaka miwili na nilikuwa na kundi zima la wachezaji mara moja tu, na huwezi kuendeleza timu yenye majeraha mengi," Ten Hag alisema.

„Ni kama kuogelea na mikono yako nyuma ya mgongo wako. Lazima uweke kichwa chako juu ya maji na tunajaribu kufanya hivyo."

"Isiwe hivi, lakini narudi kwenye matatizo yote tuliyonayo halafu nyie mchambue utendaji kazi, ni lazima muone tulikuwa washindani, lakini sivyo unavyotaka, la hasha, lazima tushinde kila mchezo.

„Lakini kwa sasa, hatuko katika nafasi hii na hakika si timu hii yenye majeraha."

United inaweza kufuzu kwa Ligi ya Europa kama itaifunga Manchester City katika fainali ya Kombe la FA baadaye mwezi huu.

Njia nyingine ya kuelekea kwenye mchuano wa daraja la pili barani Ulaya itakuwa kuwashinda Newcastle walio katika nafasi ya sita kwenye uwanja wa Old Trafford siku ya Jumatano kabla ya wikendi ya mwisho, lakini Chelsea walio nafasi ya saba wanaweza pia kuitoa United hadi nafasi ya Ligi ya Europa kulingana na matokeo.

Ten Hag alisema itakuwa huzuni kwa United kukosa kabisa kucheza Ulaya kwa mara ya kwanza baada ya miaka 10.

HABARI MICHEZO

# KOUASSI, TSHABALALA VITA KALI YA MABEKI VINARA WA ‘ASISTI’

**Na Adam Fungamwango**

MPIRA wa adhabu alioupiga na kusababisha bao la pili dhidi ya Azam FC, Alhamisi iliyopita kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, akiwezesha timu yake ya Simba kushinda mabao 3-0, umemfanya beki wa kushoto wa timu hiyo, Mohamed Hussein ‚Tshabalala‘, kufikisha idadi ya pasi za mabao sita mpaka sasa na kumsogelea kwa karibu kinara wa ‚asisti‘ upande wa walinzi Ligi Kuu Tanzania Bara, Yao Kouassi wa Yanga.

Kwa mujibu wa dawati letu la takwimu, Kouassi, raia wa Ivory Coast, anayecheza beki wa kulia, anaongoza kwa ‚asisst‘ kwa mabeki, akiwa ametoa pasi saba mpaka sasa, lakini tayari ameanza kuwekwa kwenye hali ya hatari na Tshabalala ambaye, faulo yake iliyofungwa kwa kichwa na Fabrice Ngoma imemfanya kumsogolea kwa karibu.

Wakati kukiwa na vita ya kuwania kiatu cha dhahabu kati ya Stephane Aziz Ki wa Yanga na Feisal Salum, ‚Fei Toto‘, tayari kumezuka nyingine ya ‚asisti‘ upande wa mabeki, huku Ligi Kuu ikielekea ukingoni ambapo imeingia raundi ya 27.

Nafasi ya tatu inashikiliwa na mabeki wawili wa Azam FC, Pascal Msindo anayecheza beki wa kulia, Lusajo Mwaikenda na Rahim Shomari wa KMC wenye ‚asisti‘ tano kila mmoja.

Nickson Kibabage wa Yanga na Shomari Kapombe wa Simba, ambao wote wanacheza beki wa kulia, wana ‚asisst‘ nne mpaka sasa.

Wachezaji wanaoongoza kwa ‚asisti‘ za jumla ni Kipre Junior wa Azam FC na Aziz Ki wa Yanga, ambao wote wana ‚asisst‘ nane kila mmoja, wakifuatiwa na Fei Toto wa Azam na Kouassi wa Yanga, ambao wote wana ‚asisti‘ saba kila mmoja.



Beki wa Simba, Kennedy Juma (kushoto), akimiliki mpira mbele ya mshambuliaji wa Kagera Sugar, Obrey Chirwa, wakati wa mchezo wao wa Ligi Kuu juzi kwenye Uwanja wa Kaitaba, Bukoba. Timu hizo zilifungana bao 1-1.
**PICHA: BINZUBEIRY**

# Feitoto abadili ‘gia’ angani

**Na Saada Akida**

KIUNGO wa Azam FC, Feisal Salum ‚Feitoto‘ amesema kwa sasa lengo lake kubwa kama mchezaji ni kuisaidia timu yake kumaliza katika nafasi ya pili ili kupata nafasi ya kushiriki Ligi ya Mabingwa Afrika.

Feitoto, alisema apigii mahesabu kutwaa tuzo ya mfungaji bora bali akili yake anaielekeza kuisaidia timu yake kumaliza katika nafasi hiyo ya pili.

Fei Toto anakimbizana na mshambuliaji wa Yanga, Stephane Aziz Ki katika kuwania kiatu cha ufungaji bora ambapo wote wakiwa wamefunga mabao 15 katika msimamo huo.

Akizungumza na Nipashe jana, Fei Toto alisema kila anachokifanya uwanjani ni kwa ajili ya timu yake na anapofunga hakuna anayeshindana naye, bali ni kuipa matokeo mazuri timu yake.

Alisema anafurahi kuona anaisaidia zaidi timu yake kuweza kupata matokeo mazuri katika kila mchezo ili kufikia malengo ya kumaliza katika nafasi ya pili kwenye msimamo ili kupata nafasi ya kushiriki Ligi ya Mabingwa Afrika.

“Kila ninachokifanya uwanjani ni kwa ajili ya timu yangu, sichezi kwa kushindana na mtu, nacheza kuisaidia timu kufanya vizuri, nashukuru Mungu kwa kila kitu kizuri ninachokifanya kwa ajili ya timu yangu.

„Ushindi tunaopata niwe nimefunga mimi au mtu mwingine unatokana na jitihada na juhudi za wachezaji wote,” alisema Fei Toto.

Alisema kipaumbele chake ni kuhakikisha wanamaliza kwenye nafasi ya pili na suala la ufungaji bora ni jambo la pili kwake.

Nyota huyo alisema atahakikisha anaipambania timu yake katika kila mchezo kuweza kupata matokeo ambayo yatawasaidia kuweza kumaliza katika nafasi hiyo.

## Simba bado ina matumaini kumaliza nafasi ya pili ya ligi

INATOKA UK. 24

kufikisha pointi 57 pointi tatu nyuma ya Azam FC inayoshika nafasi ya pili lakini wakiwa wamecheza mchezo mmoja zaidi ya Simba inayoshika nafasi ya tatu.

Mchezo unaofuata, Simba itasafiri mpaka Dodoma kucheza na Dodoma Jiiji FC Mei 17 huo utakuwa mchezo wake wa 17.

## Yanga yatwaa ubingwa wa 30 Tanzania Bara

INATOKA UK. 24

toa kipa, Diarra baada ya dakika 45 za kwanza kumalizika na kumwingiza kipa Aboutwalib Mshery kipindi cha pili ambaye alisajiliwa kutoka Mtibwa.

Musonda alifunga bao la kusawazisha, baada ya pasi safi ya mpenyezo kutoka kwa Mudathir Yahaya iliyomkuta akiwa kwenye nafasi nzuri dakika ya 62, akaukwamisha wavuni.

Dakika nne baadaye, beki Kombo aliwapa Yanga zawadi ya bao la pili, katika harakati za kutaka kuokoa, kwa kuuweka mpira wavuni akiunganisha shuti la Nickson Kibabage, aliyeingia kipindi cha pili kuchukua nafasi ya Joyce Lomalisa.

Mzize, ambaye aliingia badala ya Joseph Guede aliihakikishia Yanga ushindi na kuwa mabingwa msimu huu, alipopachika bao dakika 10 kabla ya mechi kumalizika akimalizia kwa urahisi kazi iliyofanywa na Bakari Mwamnyeto, ambaye alimlamba chenga kipa, Toba Reuben na kutoa kwa mfungaji.

Mabadiliko ya kuwaingiza, Mzize, Kibabage na Pacome Zouzoua kipindi cha pili yalionekana kuibadilisha Yanga na kufanya mashambulizi makali langoni mwa Mtibwa.

Mechi ilianza taratibu, timu zote zikifanya mashambulizi ya kushtukiza, lakini walikuwa Mtibwa waliofanya shambulizi kubwa la kwanza baada ya mshambuliaji Nassor Kapama kuachia shuti lililodakwa na Diarra.

Ilamfya alifanya jaribio la kwanza langoni mwa Yanga dakika ya 10, ambapo krosi ya Kassim Haruna ilitua kichwa kwake, lakini mpira ukatoka nje.

Shambulizi kali la Yanga langoni mwa Mtibwa lilifanywa dakika ya 22 na Maxi Nzengeli, ambaye aliambaa na mpira kwenye wingi ya kushoto akiwaacha mabeki lakini kabla hajafanya chochote, golikipa wa Mtibwa, Tona alitokea na kumnyima fursa ya kuliona lango vizuri na mpira kutoka nje.

Baada ya matokeo hayo, Mtibwa Sugar inaendelea kuburuza mkia, ikibakiwa na pointi zake 20 ambapo kipigo hicho kinaipeleka karibu kabisa na shimo ya kuangukia Ligi ya ‚Championship‘ msimu ujao.

==

HABARI MICHEZO

# KOUASSI, TSHABALALA VITA KALI YA MABEKI VINARA WA 'ASISTI'

**Na Adam Fungamwango**

MPIRA wa adhabu alioupiga na kusababisha bao la pili dhidi ya Azam FC, Alhamisi iliyopita kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, akiwezesha timu yake ya Simba kushinda mabao 3-0, umemfanya beki wa kushoto wa timu hiyo, Mohamed Hussein 'Tshabalala', kufikisha idadi ya pasi za mabao sita mpaka sasa na kumsogelea kwa karibu kinara wa 'asisti' upande wa walinzi Ligi Kuu Tanzania Bara, Yao Kouassi wa Yanga.

Kwa mujibu wa dawati letu la takwimu, Kouassi, raia wa Ivory Coast, anayecheza beki wa kulia, anaongoza kwa 'asisst' kwa mabeki, akiwa ametoa pasi saba mpaka sasa, lakini tayari ameanza kuwekwa kwenye hali ya hatari na Tshabalala ambaye, faulo yake iliyofungwa kwa kichwa na Fabrice Ngoma imemfanya kumsogolea kwa karibu.

Wakati kukiwa na vita ya kuwania kiatu cha dhahabu kati ya Stephane Aziz Ki wa Yanga na Feisal Salum, 'Fei Toto', tayari kumezuka nyingine ya 'asisti' upande wa mabeki, huku Ligi Kuu ikielekea ukingoni ambapo imeingia raundi ya 27.

Nafasi ya tatu inashikiliwa na mabeki wawili wa Azam FC, Pascal Msindo anayecheza beki wa kulia, Lusajo Mwaikenda na Rahim Shomari wa KMC wenye 'asisti' tano kila mmoja.

Nickson Kibabage wa Yanga na Shomari Kapombe wa Simba, ambao wote wanacheza beki wa kulia, wana 'asisst' nne mpaka sasa.

Wachezaji wanaoongoza kwa 'asisti' za jumla ni Kipre Junior wa Azam FC na Aziz Ki wa Yanga, ambao wote wana 'asisst' nane kila mmoja, wakifuatiwa na Fei Toto wa Azam na Kouassi wa Yanga, ambao wote wana 'asisti' saba kila mmoja.



Beki wa Simba, Kennedy Juma (kushoto), akimiliki mpira mbele ya mshambuliaji wa Kagera Sugar, Obrey Chirwa, wakati wa mchezo wao wa Ligi Kuu juzi kwenye Uwanja wa Kaitaba, Bukoba. Timu hizo zilifungana bao 1-1.
**PICHA: BINZUBEIRY**

# Feitoto abadili 'gia' angani

**Na Saada Akida**

KIUNGO wa Azam FC, Feisal Salum 'Feitoto' amesema kwa sasa lengo lake kubwa kama mchezaji ni kuisaidia timu yake kumaliza katika nafasi ya pili ili kupata nafasi ya kushiriki Ligi ya Mabingwa Afrika.

Feitoto, alisema apigii mahesabu kutwaa tuzo ya mfungaji bora bali akili yake anaielekeza kuisaidia timu yake kumaliza katika nafasi hiyo ya pili.

Fei Toto anakimbizana na mshambuliaji wa Yanga, Stephane Aziz Ki katika kuwania kiatu cha ufungaji bora ambapo wote wakiwa wamefunga mabao 15 katika msimamo huo.

Akizungumza na Nipashe jana, Fei Toto alisema kila anachokifanya uwanjani ni kwa ajili ya timu yake na anapofunga hakuna anayeshindana naye, bali ni kuipa matokeo mazuri timu yake.

Alisema anafurahi kuona anaisaidia zaidi timu yake kuweza kupata matokeo mazuri katika kila mchezo ili kufikia malengo ya kumaliza katika nafasi ya pili kwenye msimamo ili kupata nafasi ya kushiriki Ligi ya Mabingwa Afrika.

"Kila ninachokifanya uwanjani ni kwa ajili ya timu yangu, sichezi kwa kushindana na mtu, nacheza kuisaidia timu kufanya vizuri, nashukuru Mungu kwa kila kitu kizuri ninachokifanya kwa ajili ya timu yangu.

„Ushindi tunaopata niwe nimefunga mimi au mtu mwingine unatokana na jitihada na juhudi za wachezaji wote," alisema Fei Toto.

Alisema kipaumbele chake ni kuhakikisha wanamaliza kwenye nafasi ya pili na suala la ufungaji bora ni jambo la pili kwake.

Nyota huyo alisema atahakikisha anaipambania timu yake katika kila mchezo kuweza kupata matokeo ambayo yatawasaidia kuweza kumaliza katika nafasi hiyo.

## Simba bado ina matumaini kumaliza nafasi ya pili ya ligi

INATOKA UK. 24

kufikisha pointi 57 pointi tatu nyuma ya Azam FC inayoshika nafasi ya pili lakini wakiwa wamecheza mchezo mmoja zaidi ya Simba inayoshika nafasi ya tatu.

Mchezo unaofuata, Simba itasafiri mpaka Dodoma kucheza na Dodoma Jiiji FC Mei 17 huo utakuwa mchezo wake wa 17.

## Yanga yatwaa ubingwa wa 30 Tanzania Bara

INATOKA UK. 24

ga ilimtoa kipa, Diarra baada ya dakika 45 za kwanza kumalizika na kumwingiza kipa Aboutwalib Mshery kipindi cha pili ambaye alisajiliwa kutoka Mtibwa.

Musonda alifunga bao la kusawazisha, baada ya pasi safi ya mpenyezo kutoka kwa Mudathir Yahaya iliyomkuta akiwa kwenye nafasi nzuri dakika ya 62, akaukwamisha wavuni.

Dakika nne baadaye, beki Kombo aliwapa Yanga zawadi ya bao la pili, katika harakati za kutaka kuokoa, kwa kuuweka mpira wavuni akiunganisha shuti la Nickson Kibabage, aliyeingia kipindi cha pili kuchukua nafasi ya Joyce Lomalisa.

Mzize, ambaye aliingia badala ya Joseph Guede aliihakikishia Yanga ushindi na kuwa mabingwa msimu huu, alipopachika bao dakika 10 kabla ya mechi kumalizika akimalizia kwa urahisi kazi iliyofanywa na Bakari Mwamnyeto, ambaye alimlamba chenga kipa, Toba Reuben na kutoa kwa mfungaji.

Mabadiliko ya kuwaingiza, Mzize, Kibabage na Pacome Zouzoua kipindi cha pili yalionekana kuibadilisha Yanga na kufanya mashambulizi makali langoni mwa Mtibwa.

Mechi ilianza taratibu, timu zote zikifanya mashambulizi ya kushtukiza, lakini walikuwa Mtibwa waliofanya shambulizi kubwa la kwanza baada ya mshambuliaji Nassor Kapama kuachia shuti lililodakwa na Diarra.

Ilamfya alifanya jaribio la kwanza langoni mwa Yanga dakika ya 10, ambapo krosi ya Kassim Haruna ilitua kichwa kwake, lakini mpira ukatoka nje.

Shambulizi kali la Yanga langoni mwa Mtibwa lilifanywa dakika ya 22 na Maxi Nzengeli, ambaye aliambaa na mpira kwenye wingi ya kushoto akiwaacha mabeki lakini kabla hajafanya chochote, golikipa wa Mtibwa, Tona alitokea na kumnyima fursa ya kuliona lango vizuri na mpira kutoka nje.

Baada ya matokeo hayo, Mtibwa Sugar inaendelea kuburuza mkia, ikibakiwa na pointi zake 20 ambapo kipigo hicho kinaipeleka karibu kabisa na shimo ya kuangukia Ligi ya 'Championship' msimu ujao.

Michezo
Nipashe

## Neymar awaahidi raha mashabiki

UKURASA 22





Mshambuliaji wa Yanga, Clement Mzize (kulia), akipongezwa na kiungo wa timu hiyo, Stephane Azizi Ki, baada ya kuifungia timu hiyo bao kwenye ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya Mtibwa Sugar jana uwanja wa Manungu, Morogoro. **PICHA:BINZUBEIRY**

# YANGA YATWAA UBINGWA WA 30 TANZANIA BARA

### Imeutangaza baada ya kuifunga Mtibwa Sugar jana huku ikiwa na...

**Na Adam Fungamwango**

HATIMAYE mabingwa watetezi Yanga, wamefanikiwa kutetea ubingwa wao wa Ligi Kuu Tanzania Bara kwa mara ya tatu mfululizo, baada ya kuitwanga Mtibwa Sugar mabao 3-1, katika mechi iliyochezwa jana jioni kwenye Uwanja wa Manungu Complex, Turiani, Morogoro.

Ubingwa huo unakuwa wa 30 kwa timu hiyo, tangu ilipotwaa kwa mara ya kwanza mwaka 1968, ikiwa ni mara ya tatu kutwaa mfululizo.

Ilifanya hivyo mwaka 1991, hadi 1993, ikatwaa tena mara tatu mfululizo mwaka 1996 hadi 1998, ikarudi tena msimu wa 2014/15, hadi 2016/17, na hii ni mara ya nne, kuanzia 2021/22.

Yanga walitangaza ubingwa huku ikiwa na michezo miwili mkononi baada ya kufikisha pointi 71 ambazo haziwezi kufikiwa na timu yoyote zikiwamo Azam FC na Simba zinazoshika nafasi ya pili na ya tatu.

Timu hiyo pia ina rekodi ya kutwaa ubingwa mara tano mfululizo kuanzia mwaka 1968 hadi 1972, kama ilivyokuwa na watani zao wa jadi Simba ambao walifanya hivyo pia kuanzia mwaka 1976 hadi 1980.

Mabao mawili ya washambuliaji, Mzambia, Kennedy Musonda, Clement Mzize aliyeingia kipindi cha pili, pamoja na bao la kujifunga la beki wa Mtibwa, Nasry Kombo, yaliifanya timu hiyo kutimiza lengo la kutwaa ubingwa kwenye mechi ya jana, hasa baada ya Simba kulazimishwa sare ya bao 1-1, Jumapili iliyopita dhidi ya Kagera Sugar na kuirahisishia Yanga kazi.

Ubingwa huo haukuja kirahisi, ilibidi wachezaji wa Yanga kupambana hasa baada ya kutang[illegible]a bao la dakika ya 32 lililofungwa na Charles Ilamfya ambalo lilidumu mpaka mapumziko.

Ilamfya aliwashtukiza Yanga kwa kutanguliza Mtibwa, akiunganisha krosi ya mchezaji anayeichezea timu hiyo kwa mkopo akitokea Simba, Jimson Mwanuke.

Mpira mrefu ulipigwa kutoka nyuma, ulikwenda winga ya kulia na kumkuta mchezaji huyo aliyekuwa peke yake akakimbia karibu na kibendera kabla ya kupiga krosi ya juu iliyomkuta mfungaji aliyeunganisha kwa kichwa na mpira kujaa wavuni na kuitanguliza Mtibwa.

Baada ya bao hilo, Mtibwa walionekana kurudi nyuma na kuzuia zaidi badala ya kushambulia, wakiuacha mpira kwa Yanga kwa muda mwingi wa mchezo na Yanga kuanza kuutawala mchezo.

Katika hali isiyokuwa ya kawaida, Yan-

INAENDELEA UK. 23

# Simba bado ina matumaini kumaliza nafasi ya pili ya ligi

**Na Faustine Feliciane**

WAKATI jana Yanga ikitangaza ubingwa wake wa tatu mfululizo baada ya kuifunga Mtibwa Sugar mabao 3-1 jana, Kocha wa Simba, Juma Mgunda, amesema timu hiyo bado ina nafasi ya kumaliza ligi nyuma ya Yanga licha ya sare waliyoipata juzi dhidi ya Kagera Sugar.

Simba ilikuwa na nafasi ya kupanda mpaka nafasi ya pili kama ingefanikiwa kupata ushindi kwenye mchezo huo uliochezwa Uwanja wa Kaitaba, mjini Bukoba na kuambulia sare ya bao 1-1.

Akizungumza na Nipashe, Mgunda alisema licha ya sare hiyo dhidi ya Kagera Sugar, bado hawajakata tamaa kumaliza katika nafasi hiyo na kupata tiketi ya kushiriki Ligi ya Mabingwa Afrika msimu ujao.

„Bado hatujamaliza michezo yote, tumepanda kwenye mchezo dhidi ya kagera lakini bahati haikuwa kwetu, tunajipanga kwa ajili ya mchezo ujao, kwangu mimi bado haijaisha, bado tuna nafasi ya kumaliza kwenye nafasi ya pili, kikubwa tunatakiwa kufanya kazi mapungufu tuliyaona ili michezo iliyobaki tupate alama tatu," alisema Mgunda.

Aidha, alisema wachezaji wake wanapambana sana uwanjani kwa ajili ya kupata alama tatu lakini wamekuwa wakikosa bahati ya kuondoka na ushindi kwenye baadhi ya michezo yao.

„Tutaendelea kupambana, nimewaambia wachezaji wangu wasikate tamaa, waendelee kupambana na kuweka mkazo kwenye michezo yote iliyobakia, hatutaki kuangalia matokeo ya timu nyingine, tupambane sisi kushinda michezo yote, naamini tunaweza kufanya vizuri kwenye mechi zote zilizobakia," alisema Mgunda.

Matokeo ya juzi yameifanya Simba

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >